Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# MKUTANO WA KUMI NA NANE

## Kikao cha Pili – Tarehe 27 Januari, 2010

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):**

Taarifa ya Mwaka ya Utendaji wa Soko la Bima Nchini kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2008 (*The Annual Report of Insurance Market Performance for the year ended 31st December, 2008).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 14

### Mvua ya Kutengeneza

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, katika utawala wake tuliarifiwa kwamba, alikwenda Malaysia kujifunza namna ya kutengeneza mvua ili isaidie wakati wa ukame:-

(a) Je, alifanikiwa kupata taaluma hiyo?

(b) Kama taaluma hiyo itakuwa ya manufaa kwetu; je, Serikali imeshapeleka wanafunzi wangapi kujifunza taaluma hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mbunge wa Chake Chake, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Edward Lowassa, wakati akiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hakuwahi kwenda Malaysia kujifunza namna ya kutengeneza mvua ili isaidie nchi yetu wakati wa ukame.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachofahamu ni kwamba, mwishoni mwa mwaka 2006, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, alifanya ziara ya kikazi nchini Thailand. Wakati wa safari hiyo, nchi yetu ilikuwa inakabiliwa na tatizo la ukame lililotokana na ukosefu wa mvua kwa muda mrefu. Baada ya Waziri Mkuu kutembelea Wizara ya Kilimo na Ushirika ya Thailand inayosimamia uzalishaji wa mvua kwa kutumia teknolojia ya Mfalme wa Nchi hiyo (*Royal Rainmaking Technology),* aliona kwamba ipo haja ya kujifunza juu ya Teknolojia hiyo mpya. Hivyo, aliyekuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu aliiomba Serikali ya Thailand kupitia Wizara ya Kilimo na Ushirika ya Thailand kuisaidia Serikali ya Tanzania katika Teknolojia ya kurutubisha mawingu na kuongeza mvua. Serikali ya Thailand ilikubali ombi hilo na kuahidi kutuma wataalamu wake nchini kwetu.

Baada ya majadiliano, mahitaji ya rasilimali zilizohitajika wakati wa kufanya jaribio yalihusisha mambo yafuatayo:-

(a) Ndege mbili hadi nne za kukodi kwa siku saba kwa ajili ya kupeleka kemikali zinazohitajika kwenye mawingU angani.

(b) Gharama ya kutoa mizigo bandarini na kusafirisha malighafi na vifaa vingine hadi kituo cha majaribio.

(c) Gharama za kukodi maghala ya kuhifadhi malighafi na vifaa muhimu katika zoezi hilo.

(d) Malipo ya posho ya kujikimu na malazi kwa wataalamu kutoka Thailand.

(e) Gharama za tiketi za ndege na posho kwa wataalamu wa Tanzania watakaochaguliwa kwenda kupata mafunzo ya awali ambayo yangetolewa nchini Thailand kabla ya zoezi la majaribio kufanyika.

(f) Jumla ya gharama kwa ajili ya kufanya zoezi la majaribio ilionekana kuwa kubwa sana kufikia kiasi cha Shilingi za Kitanzania 1.5 bilioni kwa wakati huo na kama mradi ungetekelezwa basi gharama halisi zingekuwa shilingi bilioni 14.5. Kwa kuwa Serikali haikuwa imeweka fedha hizo kwenye bajeti yake ya mwaka 2006/2007, iliamua kulisitisha zoezi hilo kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali haikufanikiwa kupata taaluma ya kutengeneza mvua kutoka Thailand wala kupeleka wanafunzi nchini Thailand kujifunza taaluma hiyo.

Na. 15

**Barabara ya Mpwapwa – Lumuma Kutengenezwa**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya kutoka Mpwapwa hadi Lumuma kupitia Vijiji vya Manghangu, Kimagai, Godegode na Pwaga inahitaji matengenezo makubwa na kwamba Serikali ilishatoa ahadi ya kutengeneza barabara hiyo:-

Je, katika bajeti ya mwaka 2008/2009 Serikali imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Mpwapwa – Godegode - Lumuma yenye urefu wa kilomita 60 ni mojawapo kati ya barabara muhimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa. Ni kweli kuwa Serikali ilishatoa ahadi kuitengeneza barabara hii ili iweze kupitika kwa kipindi chote cha mwaka. Barabara hii ni kiungo muhimu kinachoharakisha ukuaji wa uchumi wa Wananchi wa Lumuma na Pwaga ambao wanategemea kilimo cha mazao ya chakula na biashara kama vile mpunga, mahindi, maharage, vitunguu, kunde, alizeti na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa barabara hii, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa imekuwa ikiifanyia matengenezo barabara hii ili iweze kupitika wakati wote kutegemeana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2006/07, Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ilitenga na kutumia shilingi milioni 20.8 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya sehemu korofi kati ya Godegode na Pwaga kwa kilomita 20.

Katika mwaka wa fedha 2007/08, Serikali ilitumia shilingi milioni 81.2 kufanya matengenezo ya muda maalum kati ya Pwaga hadi Lumuma kilomita 20. Katika mwaka wa fedha 2008/09, Halmashauri ilitumia kiasi cha shilingi milioni 60 kufanya matengenezo ya maeneo korofi kati ya Godegode na Pwaga.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais Wilayani Mpwapwa aliagiza Halmashauri iweke kipaumbele katika kuifanyia matengenezo

barabara hiyo ambayo inapita kwenye bonde kubwa la Godegode. Katika kuitikia agizo hilo hadi sasa Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa inaendelea na mchakato wa kuifanyia upembuzi yakinifu ili kujua gharama halisi za mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Serikali kwa kuzingatia agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imetenga kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Chinyasungwa na makalavati katika Bonde la Godegode. Mpaka hivi sasa Halmashauri imeshapokea kiasi cha shilingi milioni 450 kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo na mchakato wa kumpata Mkandarasi umeanza. Aidha, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 184.5 kutoka Mfuko wa Barabara za Maendeleo ili kufanya ukarabati mkubwa katika Barabara ya Mpwapwa - Lumuma. Vile vile Serikali imetenga shilingi milioni 948.5 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ya Barabara za Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ikiwemo Barabara ya Mpwapwa - Lumuma.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, Mheshimiwa Naibu Waziri ana taarifa kwamba katika mafuriko ambayo yametokea katika Wilaya ya Mpwapwa, Daraja la Godegode limesombwa na maji, Daraja la Gulwe limesombwa na maji na kusababisha Wananchi wa Tarafa za Kibakwe, Rudi na Kata za Lumuma na Berege kukosa mawasiliano. Lakini kwa kuwa Serikali yetu ni sikivu, tayari wameshapeleka wanajeshi na wanafanya kazi nzuri sana ya kujenga daraja hilo. Ushauri wangu ni kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu atembelee maeneo hayo ili aweze kuwapa wananchi hao pole kama walivyofanya Kilosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakiri kwamba Halmashauri ya Mpwapwa imeshapokea shilingi milioni 500 sio shillingi 450. Kwa kuwa hivi sasa mkandarasi anatafutwa; je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba ipo haja ya kujenga Daraja hilo kwa haraka ili kuboresha mawasiliano hasa katika eneo la Godegode ambalo hivi sasa liko Kisiwani?

**NAIBU SPIKA:** Haya Mheshimiwa Waziri nadhani ujibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo yeye mwenyewe ametoa ushuhuda hapa ndani kwamba Serikali yetu ni sikivu na imefuatilia tatizo hili la daraja limeondoka. Namshukuru sana.

Kipekee, ningependa kumpongeza sana kwa sababu katika haya maafa yaliyotokea Mheshimiwa Lubeleje alisimama mstari wa mbele kwa kushirikiana na wananchi wake kuona kwamba tatizo hili linaondoka. Kwa hiyo, napenda kumshukuru sana kwa niaba ya Serikali.

Hili la Mheshimiwa Waziri Mkuu, bahati nzuri wakati nilipokuwa naandaa majibu ya hili swali nilizungumza na Mheshimiwa Waziri Mkuu na alinieleza kwamba, atakuwa tayari kwenda Mpwapwa kufuatilia na kuona nini kilichotokea pale kama alivyofanya Kilosa.

Pili, amezungumzia kuhusu shilingi milioni 500, *documents* zetu kwa sababu zile fedha ziliondoka kwanza shilingi milioni 450 na halafu baadae ndio zikaondoka hizo milioni 50 ambazo yeye anafahamu kwa sababu yuko kwenye *centre* ya jambo hilo. Sasa kazi imekwisha hela zimeshakwenda kule, kwa hiyo, nitakachofanya ni kusukuma wale walioko kule kuhakikisha kwamba wanaharakisha mpango huu. Kwa hiyo, shida ilikuwa ni fedha tu.

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo maana nikakwambia ujibu kwa kifupi kwa sababu mambo yote yamewekwa sawa.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa vile haya mafuriko yameathiri nchi nzima, je, Serikali itakuwa tayari kuzungukia mikoa yote na kuona athari zilizojitokeza kama vile Barabara za Iramba Mashariki na kwingineko ili waweze kutafuta fedha kusaidia nchi nzima kutengeneza barabara zilizoathirika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. PHILIP S. MARMO):** Mheshimiwa Naibu Spika, Maofisa wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa, sasa hivi wanazunguka nchi nzima na Kamati mbalimbali za Maafa kwa ngazi ya Kata na Wilaya. Tanzania nzima huwasilisha taarifa zao katika Kitengo cha Maafa na tathmini inafanyika na katika Bunge hili tutatoa taarifa nzima ya maafa hapa nchini.

Na. 16

**Fedha za Miradi ya Barabara Vijijini - Wilayani**

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kwenye Bajeti yake ya mwaka 2008/2009 ilitenga shilingi milioni 431 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Barabara Vijijini chini ya Mpango wa (LGTP) katika Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe; na kwa kuwa kutokana na maelekezo ya Serikali utekelezaji wa miradi hii ulishaanza na takriban 70% ya kazi imekamilika kwa kuwatumia wakandarasi kwa mikataba maalum lakini hadi sasa fedha hizo hazijapelekwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe kwa ajili ya kuwalipa wakandarasi:-

(a) Je, ni lini Wilaya ya Korogwe itapewa fedha hizo ili iweze kuwalipa wakandarasi waliofanya kazi hizo ambao wanatishia kuipeleka Halmashauri Mahakamani?

(b) Je, Serikali haioni kuwa huo ni udhaifu kupanga bajeti na kutoa ahadi zisizotekelezeka kwa wakati uliopangwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Bajeti yake ya mwaka 2008/2009, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya barabara chini ya Programu ya Usafiri katika Serikali za Mitaa. Programu hii ilianza kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 na inafadhiliwa na Serikali za Norway na Denmark. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Serikali ya Norway ilibadilisha utaratibu wa kutoa fedha zake, badala ya kupeleka fedha moja kwa moja kwenye Miradi sasa fedha hizo zinapitia kwenye Mfuko wa kusaidia Serikali, yaani *General Budget Support.* Kutokana na hatua hii, hata fedha za Programu hii nazo zinatumia utaratibu huu. Mabadiliko haya, yamesababisha fedha za LGTP kutokuelekezwa katika Programu kama ilivyotarajiwa na hivyo kuathiri utekelezaji wa Programu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, *(General Budget Support*) ni utaratibu ambao Serikali imekubaliana na Wadau wa Maendeleo na ndio ambao Serikali inaupendelea zaidi. Taratibu nyingine ni zile za kupeleka fedha moja kwa moja kwenye Mradi na ule wa Kapu la Pamoja *(Common Basket Fund*). Utaratibu wa kusaidia Bejeti huisaidia Serikali kuelekeza rasilimali kwa kuangalia vipaumbele vya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kweli kwamba, kulikuwa na udhaifu katika kupanga bajeti bali ni upungufu uliojitokeza kwa kubadilisha utaratibu wa upatikanaji wa fedha za misaada. Hata hivyo, Serikali inaendelea kufanya jitihada za kuhakikisha kwamba Wakandarasi wanalipwa fedha zao.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ihakikishe kwamba, inaandaa Mpango wake wa Maendeleo wa Mwaka 2010/2011 kwa kutoa vipaumbele kwa Miradi ambayo imeanza na haijakamilika. Pia kutumia fedha za *Local Government Development Grant (LGDG)* katika kukamilisha miradi hiyo.

Na. 17

**Wawekezaji wa Hoteli za "Five Star"**

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni kumetokea mtindo wa watu wasio wageni na wageni wanaojiita ni wawekezaji wa Hoteli za Nyota Tano *(Five Stars Hotels)* na kuchukua ardhi kubwa kandokando ya Bahari ya Hindi kupitia wenyeji wa maeneo hayo lakini badala yake hujenga hoteli za gharama ndogo za kuezeka makuti:-

Je, Serikali inalifahamu tatizo hilo; na kama inalifahamu ni hatua gani zinachukuliwa ili kudhibiti hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii imekuwa ikitekeleza Mpango Kamambe wa kuendeleza Utalii (*Tourism Master Plan*), ambapo utalii wa fukwe ni moja ya maeneo yaliyotiliwa mkazo. Katika kutekeleza mpango huu, kuanzia mwaka 2007 -2009 Wizara ilifanya zoezi la kubaini maeneo ya fukwe katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Tanga, Pwani na Dar es Salaam. Zoezi hili limeshirikisha Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, pamoja na wananchi wa maeneo husika.

Zoezi lilibaini kuwa maeneo mengi hayajaendelezwa na umiliki wake upo mikononi mwa watu binafsi na machache yanamilikiwa na mamlaka zinazosimamia maeneo hayo. Wizara imekuwa na jukumu la kuelimisha wananchi kuepuka uuzaji wa maeneo ya fukwe kiholela na pia kuwataka wawekezaji kumiliki maeneo kwa kufuata taratibu stahili.

Aidha, Wizara ina jukumu la kusimamia Sheria na Kanuni za Utalii zilizopo na vile vile kuweka hoteli katika daraja za nyota kwa kufuata vigezo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Zoezi la uwekaji nyota katika hoteli nchini lilianza mapema mwaka 2009 katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Katika mikoa hii jumla ya hoteli 203 zilihakikiwa, ambapo hoteli 98 zilionekana kufaa na zilipewa daraja za nyota kuanzia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Upokeaji wa maombi ya wawekezaji na uidhinishwaji wa miradi hiyo hufanywa na Kituo cha Uwekezaji (TIC). Hapo awali hapakuwepo na vigezo vinavyoonesha daraja za nyota kwa hoteli. Hivi sasa Wizara yangu imepata vigezo vinavyoonesha daraja za nyota kwa aina mbalimbali za hoteli. Vigezo hivi viliandaliwa na kupitishwa na Jumuiya

ya Afrika Mashariki.  Katika kipindi cha 2008/09, Wizara ilisambaza nakala za vijitabu vya vigezo zaidi ya 2,000 kwa wawekezaji wa hoteli.

Lengo kuu ni kuelimisha na kutoa mwongozo kwa wawekezaji wapya na hata wale waliotangulia.  Hivyo, Wizara itaendelea kusambaza nakala zaidi za vigezo na kutoa ushauri kwa wawekezaji ili kufikia lengo la kuwa na hoteli zenye ubora.

Aidha, suala la uezekaji wa kutumia makuti katika hoteli huzingatia zaidi aina ya hoteli inayojengwa, pamoja na mandhari ya eneo.  Uezekaji wa hoteli kwa makuti si nafuu kama inavyodhaniwa na haushushi ubora wa hoteli au *lodge* na pia una faida nyingi za kimazingira.

Wizara yangu hufanya ukaguzi wa hoteli zilizokamilika na kuziweka katika daraja na taarifa hizi huwasilishwa Kituo cha Uwekezaji (TIC) ili kujiridhisha kwamba uwezekaji unafanyika kwa mujibu wa mikataba ya uwekezaji ambayo mwekezaji husika alipewa na kituo hicho.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:**  Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nashukuru kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa.  Pamoja na hayo, naomba kuuliza maswali madogo mawili:-

(i) Kwa kuwa imekwishajitokeza kwamba kwa wale ambao tayari wamekiuka taratibu na wamejenga hoteli katika maeneo ambayo siyo rasmi wanajenga hoteli hizo haraka haraka sana; je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba hoteli hizo zinazojengwa zimefanyiwa tathmini ya athari kwa mazingira (EIA)?

(ii) Kwa kuwa wawekezaji ambao wamepewa kujenga hoteli hizo katika fukwe za bahari wengi wamekiuka utaratibu wa kuacha mita 60 kabla ya fukwe hizo na kuwanyima wananchi kwenda kufaidi fukwe zao; je, Serikali inachukua hatua gani dhidi ya watu hao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**  Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa uwekezaji unamtaka mwekezaji kufanya tathmini ya athari kwa mazingira kwenye eneo linalofanyika uwekezaji na jambo hili linasimamiwa na mamlaka nyingine katika Serikali hususan Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira).

Kwa maeneo yote ambayo uwekezaji umekuwa ukifuata utaratibu huu hiyo ilikuwa ikifanyika na maeneo ambayo imekuwa haifanyiki hatua zimekuwa zikichukuliwa kadiri sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba kuna watu wamekiuka sheria inayosema kuacha mita 60.  Kadhalika suala hili linasimamiwa na Mwongozo wa Matumizi ya Ardhi ya Fukwe ya Mwaka 1992 na Sheria ya Mipango Miji ya Mwaka 1993. Mwongozo wa Mwaka 1992 unasema mita 60 ziachwe lakini mwekezaji anaruhusiwa kutumia lile eneo kwa kuweka *luxury hotels*.  Kwa maana hiyo, matumizi yanayoruhusiwa katika hizo

mita 60 ni pamoja na kuwa *public beaches* au kuwa na *luxury hotels*. Kwa maana hiyo sheria haikatazi kabisa isipokuwa inaweka mwongozo ambao mtu anapaswa kuufuata.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa maeneo mengi ya fukwe mara nyingi huwa yanambaatana na visiwa lakini pia visiwa hivyo huwa vinamilikiwa na wawekezaji kutoka nje au pengine hata Watanzania; ninavyofahamu ni kwamba sheria hairuhusu; je, ni kwa nini hasa maeneo hayo huwa yanamilikiwa na baadae Serikali inakubali kuwapatia hatimiliki; kwa nini hilo linafanyika?

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hairuhusu mtu kumilikishwa kisiwa na kama kuna mtu amemilikishwa kisiwa mahali basi tupewe taarifa ili hatua stahiki zichukuliwe.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Lengo la Serikali ni kuongeza Pato la Taifa kupitia watalii lakini hoteli nyingi zilizoezekwa kwa makuti sasa hivi zinaungua moto. Je, Serikali haioni kwamba itawapa hofu watalii kufikia kwenye hoteli hizo zilizoezekwa kwa makuti; na je hamuwezi kutafuta mbadala wa kuezeka nyumba hizo za watalii?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Afadhali leo umevaa gauni jana ulivaa suti.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ajali za moto zinazotokea kwenye hoteli kwa kiasi kikubwa zinaathiri utulivu na furaha ya wageni wanaokuwepo kwenye maeneo hayo. Sisi kama Wizara tumekuwa tukiwashauri sana wawekezaji kwamba wazingatie utaratibu au uezekaji ambao hautakuwa na madhara ya moto.

Kwa hiyo, maeneo mengi wawekezaji wengi wameanza kulizingatia hili, lakini ieleweke kwamba *property* hizi zinamilikiwa na watu binafsi; kwa hiyo, sisi tunawashauri na wao wanazingatia kwa kuzingatia utaalamu mwingine unaohusu usalama kwenye maeneo yao ya uwekezaji ambao wameufanya.

Na. 18

**Serikali Kusaidia Juhudi za Kutengeneza Filamu ya Utamaduni**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA (K.n.y. MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO)** aliuliza:-

Kwa kuwa nyakati za kiangazi hasa miezi ya Agosti hadi Novemba Wananchi wa Mbinga hujishughulisha pia na michezo ya utamaduni:-

(a) Je, Serikali inawasaidiaje Wananchi wa Mbinga katika juhudi zao za kutengeneza filamu ya utamaduni huo ili kuvutia watalii?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyatambua na kuyatangaza maeneo mbalimbali ya kihistoria yaliyoko Mbinga kama vile yale ya Litembo, Jiwe la Mbuji na Malango ya Lilangangondu Kata ya Mswea?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, lenye vipengele (a) na (b), napenda kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Sheria ya Mambo ya Kale ya Mwaka 1964 kifungu cha 16 (1) - (2) na marekebisho yake ya mwaka 1979, inazipa Mamlaka za Miji na Halmashauri za Wilaya uwezo wa kuweka sheria ndogo ndogo ambazo zitatumika kuhifadhi, kulinda na kuratibu uingiaji katika maeneo yenye historia. Serikali Kuu kwa upande wake ina jukumu la kutoa utaalamu na mafunzo yanayohusu fani mbalimbali za utamaduni, kugharamia uendeshaji wa shughuli za utamaduni katika ngazi ya taifa na kimataifa na kusimamia utekelezaji wa sera, pamoja na kuweka taratibu za uendeshaji na usimamizi wa utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Kayombo, yenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kwa kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga imeanza kazi ya kupiga picha za kawaida za maeneo ya kihistoria na vikundi vinavyoshughulika na utamaduni Wilayani Mbinga. Hatua itakayofuata ni kutengeneza filamu itakayoonesha Utamaduni wa Watu wa Mbinga, kazi ambayo inaratibiwa na Afisa Utamaduni wa Wilaya ya Mbinga.

Hii ni katika kutambua juhudi za Wananchi wa Mbinga kuinua utamaduni ili kuvutia watalii. Baada ya hatua hiyo kukamilika, kazi ya kutangaza kazi na Utamaduni wa Watu wa Mbinga itafuatia na Wizara yangu itahusika moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, naomba kumshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Ofisi ya Utamaduni Wilaya, kuweka mikakati ya kuvisaidia vikundi vinavyojishughulisha na utamaduni ili viweze kusajiliwa na kutambuliwa na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Wizara yangu itaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu.

(b) Serikali ina Mpango wa Kudumu wa Uhifadhi wa Utamaduni ambao umegawanywa katika Kanda. Chini ya Mpango huu, Wataalamu wa Idara ya Utamduni wameanza kufanya utafiti ili kupata taarifa kuhusu ukuzaji na uendelezaji wa urithi wa utamaduni unaohamishwa na usiohamishika ili taarifa hizo zitumike katika kuyaboresha maeneo ya kihistoria yakiwemo Jiwe la Mbuji, Litembo na Mapango ya Lilangangondu kuwa miongoni mwa vivutio vya vya utalii nchini. Tayari Wizara yangu imewasiliana na Uongozi wa Mkoa wa Ruvuma ili maeneo hayo yaingizwe kwenye orodha ya vivutio vya

utalii katika Mkoa ili hatimaye kazi ya kutangaza maeneo hayo na vivutio vingine vilivyoko Mkoa wa Ruvuma iweze kufanyika kwa tija.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize maswali ya nyongeza. Namshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo naamini yamejitosheleza kwa kiasi.

(i) Pamoja na majibu hayo mazuri kwa kuwa hivi karibuni Wizara ya Maliasili na Utalii imewezesha Mkoa wa Ruvuma hususan Mji wa Songea kuwa Mji wa Kihistoria na kishujaa na hivyo kuadhimisha makumbusho yake tarehe 27 Februari 2010; na kwa kuwa maeneo yaliyotajwa na swali la Mheshimiwa Kayombo yanajihusisha katika circuit ya utalii huu; je, utakubaliana nami kwamba ni vema sasa katika kufikia kilele cha siku hiyo ukatusaidia kuwashawishi watu ambao wanaweza kutusaidia katika kufanikisha tamasha hilo na hivyo kujionea hali halisi ya utamaduni wa Mkoa wa Ruvuma?

(ii) Kwa kuwa Mbuga za Wanyama za Luhila ni sehemu mojawapo ya vivutio hivyo vya Mkoa wa Ruvuma; na kwa kuwa Mbuga hizo sasa hivi zinakabiliwa na uhaba wa wanyama; kuna pundamilia wawili ambao ni majike na hawana dume kiasi kwamba hawaongezeki lakini pia kuna *cage* ambayo inaweza kutunza wanyama kama paka, aina ya simba au chui lakini hakuna wanyama hao na *cage* inayowezesha kufanya hivyo tayari tunayo; je, Mheshimiwa Naibu Waziri utaungana nami kwamba ni vema sasa utaratibu huo ukafanyika kwa kutumia Chuo cha Mweka ili kuweza kuwakamata hao wanyama na kuwapeleka huko?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Eng. Manyanya kwa msukumo aliouweka katika kutambua historia ya Mji wa Ruvuma hadi kufikia hatua ambayo sasa mji huo unatambuliwa kama Mji wa Kihistoria. Nimhakikishie kwamba, Wizara yangu itaendelea kushirikiana naye na kwa hili ambalo mimi naliona ni kama ombi, Wizara iweze kuona namna ya kusaidia katika kufanikisha sherehe, namhakikishia kwamba Wizara tutakuwa tayari kushirikiana naye kuona kwamba sherehe hizi zinafanikiwa kwa sababu ni kusudi la kila mmoja wetu kuhakikisha kwamba historia ya eneo hilo inaimarishwa.

Kuhusu swali la pili, sasa hivi tunafanya sensa ya wanyama ambayo karibia takwimu zake zimeshakamilika ambazo zimeshawasilishwa Wizarani Mwezi Desemba, 2009. Katika sensa hii tunajaribu kuainisha wingi wa wanyama kwa kila eneo na kwa maana hiyo tunafikiri kwamba, ushauri huu wa Mheshimiwa Mbunge tutauzingatia katika utekelezaji wa Ripoti hiyo tutakayokuwa tumeipata kutokana na hiyo Sensa ya Wanyama. Kwa hakika ombi la kwamba wanyama wapelekwe kwenye eneo hilo tutalizingatia ilimradi tufanye utafiti wa kujiridhisha kwamba ni mazingira gani yanaweza yakasababisha wanyama hawa waweze ku-*survive* zaidi.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Wilaya ya Kahama ina vivutio vingi vya utalii ikiwa ni pamoja na maeneo ya kihistoria, na kwa kutambua kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri anatoka maeneo ya

Kahama, maeneo haya ambayo nimeyataja ya kihistoria bado hayajatambuliwa na hayajatangazwa; je, Serikali inasema nini kuhusu hili?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna maeneo mengi ya kihistoria nchini ambayo hayajatambuliwa, Wizara imekuwa ikifanya mpango wa kuyatambua maeneo haya kwa kushirikiana na Serikali za maeneo hayo kwa maana ya Serikali za Mikoa na Wilaya. Hivi sasa tunashirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga kuweza kubainisha maeneo ya vivutio vya utalii kwa lengo la kuandaa *Investors Forum* kwa Mkoa wa Shinyanga, ambayo pia pamoja na maeneo mengine italenga pia kwenye eneo la utalii. Kwa hiyo, kazi hii inaendelea.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo sana. Napenda kuuliza kwamba; kwa vile Serikali inaweka mpango wa kuyatambua na kuyatangaza maeneo mbalimbali nadhani utaratibu kama huu ungepaswa uzingatiwe sana; kwa mfano katika Kisiwa cha Ukerewe kuna jiwe ambalo huwa linacheza likiimbiwa wimbo *(a dancing rock)* na lipo katika kisiwa kidogo cha Ukara. Sasa ni kitu ambacho ni kizuri kuibuliwa kama kama moja ya vivutio vya historia katika nchi hii. Kwa hiyo, naomba basi Mheshimiwa Naibu Waziri katika kuyatambua maeneo hayo, akumbuke na jiwe linalo-*dance* kule Ukara liweze kuwa sehemu ya makumbusho.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kutambua maeneo ya kihistoria kwenye Mkoa wa Mwanza ilishakamilika. Hatua ambayo inafuata sasa ni kuyatunza maeneo hayo. Wananchi wa eneo husika ndiyo wanahusika na utunzaji wa utamaduni na vivutio vingine vya kihistoria kwenye maeneo hayo. Sisi kama Wizara sasa hivi tunashirikiana na Mkoa wa Mwanza kuhamasisha wawezekezaji, kwa sababu changamoto inayokuwepo ni kuweka miundombinu stahili ili watu waweze kutembelea eneo hilo. Kwa hiyo, utunzaji upo unaendelea, changamoto ambayo ni ya kutangaza pia tumeanza kuikabili.

Na. 19

**Vyakula Vinavyouzwa Bila Kuwekwa Muda wa Ubora**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MHE. RUTH B. MSAFIRI)** aliuliza:-

Kwa kuwa bidhaa za chakula zinazouzwa nchini kama vile mikate, uyoga, nyama na samaki haziwekewi muda wa ubora wa matumizi (*expiring date*); na kwa kuwa baadhi ya vyakula hivyo huwa vimeharibika vinapofikishwa nyumbani:-

(a) Je, Serikali inasemaje juu ya tatizo hilo?

(b) Je, Serikali inatolea kauli gani kuhusu ilani ya wafanyabiashara kuwa "mali ikishauzwa hairudishwi"?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, lipo tatizo la muda wa ubora wa matumizi (*expiring date*) kutowekwa kwenye baadhi ya vyakula. Kwa mujibu wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Na. 1 ya Mwaka 2009 na Kanuni za Vielezo *(Food Labelling Regulations, 2006*), zilizotungwa chini ya Sheria hiyo, vyakula vilivyosindikwa na kufungashwa vinapaswa kuwekewa muda wa matumizi. Aidha, hitaji hilo limewekwa wazi katika viwango husika kwa bidhaa za vyakula ambavyo vinafungashwa *(pre-packaged food)* ikiwemo mikate, samaki na uyoga ni lazima muda wa ubora unahitajika uwekwe wazi kwenye vifungashio vya vyakula hivyo ni jina la chakula, malighafi zinazotumika, uzito, jina na anuani ya mzalishaji, nchi bidhaa hiyo ilipotengenezwa, pamoja na maelekezo ya matumizi. Shirika la Viwango Tanzania linaendelea kuwaelimisha wazalishaji wa vyakula kuhusu umuhimu wa kuweka taarifa hiyo muhimu kwenye vifungashio.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la ilani ya wafanyabiashara kuwa mali ikishauzwa hairudishwi linatokana na sababu kwamba mtu anaweza kununua bidhaa akaiharibu mwenyewe kwa sababu moja au nyingine halafu akataka kuirudisha dukani. Hata hivyo, Sheria inasema kwamba, kila kitu kinachouzwa ni lazima kiwe na ubora unaotakiwa ili kiweze kukidhi mahitaji yaliyokusudiwa. Sheria hizo zinajulikana kama *The Law of Contact Act Cap. 345 of 2002* na nyingine ni *Sales of Goods Act Cap. 214 of* 2002. Kwa hiyo, kwa mnunuzi ina maana kuwa ukinunua bidhaa ukaharibu usirudishe. Aidha, kwa muuzaji ina maana kwamba, asiuze kitu ambacho hakitakidhi haja ya matumizi yaliyokusudiwa. Ili kuondoa mvutano kati ya muuzaji na mnunuzi, baadhi ya watengenezaji wa bidhaa huuza bidhaa zao na kuingia makubaliano ya kuweka dhamana ya muda maalum *(guarantee)* na mnunuzi ya kurudisha bidhaa dukani endapo itagundulika kuwa bidhaa hiyo ina kasoro kutoka kwa mtengenezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kulielezea Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali itaendelea kuwaelimisha wananchi juu ya kuwa makini wanunuapo bidhaa madukani kuepuka madhara yanayoweza kuwapata kwa kutumia bidhaa zilizokwisha muda wake. Ni matumaini yangu kuwa, Waheshimiwa Wabunge watasaidia pia kutoa elimu hii katika maeneo yao ili tuweze kunusuru afya za wananchi wetu.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo tu. Kwa kuwa vyakula hivi vilivyotajwa katika swali la msingi wananchi wa hali ya chini wengi ndiyo wanaotumia na utaalam huo hawaujui; je, TBS itawasaidiaje sasa hawa wananchi ili na wao wapate haki kwa sababu hivi vyakula vinaleta athari kwenye afya zao?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO**: Mheshimiwa Naibu Spika, ni elimu ndiyo ambayo itasaidia wananchi kujua madhara ya kununua bidhaa

ambazo kwanza katika vifungashio havijaonesha muda wa kwisha matumizi yake. Kwa hiyo, nitaielekeza TBS na Wizara itasaidiana nayo kuona kwamba wananchi wanapata elimu hiyo ili kunusuru afya zao kama nilivyojibu kwenye swali la msingi.

Na. 20

**Kiwanja cha Ndege cha Tabora**

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Uwanja wa Ndege wa Tabora ni moja kati ya viwanja vikongwe hapa nchini na kwa kuwa kina umuhimu wake kwa ajili ya usalama wa nchi kwa sababu kipo katikati ya njia za kimataifa zinazotoka Kaskazini kwenda Kusini na Mashariki kwenda Magharibi; na kwa kuwa mwaka 1978 Serikali iliingia mkataba wa ujenzi mkubwa wa uwanja huo na Kampuni ya Malaudad & Rose ya Nairobi Kenya, ujenzi ambao ulisitishwa ili kukabiliana na dharura ya vita dhidi ya uvamizi wa nchi yetu uliofanywa na Nduli Idd Amin wa Uganda hapo mwaka 1979:-

Je, kwa nini mpaka leo Serikali inaendeleza viwanja vipya kwenye maeneo mengine ya nchi na kutelekeza matengenezo ya Kiwanja cha Ndege cha Tabora kwa kiwango cha lami na lini Serikali itafanya hivyo kwa uhakika?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga kama ifuatavyo:-

Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (*TAA*), imekuwa ikitekeleza mipango mbalimbali ya kuendeleza viwanja vya ndege katika maeneo mbalimbali ya nchi kulingana na mahitaji na uwezo wa Serikali. Aidha, Serikali inatambua umuhimu wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora katika kuchangia Pato la Taifa na kukuza uchumi na imekuwa ikikifanyia matengenezo ya mara kwa mara ili kukiweka katika hali nzuri kiuendeshaji na kuhakikisha kwamba usalama kwa ndege na abiria unazingatiwa wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango wa kukiimarisha Kiwanja cha Ndege cha Tabora kwa kukarabati miundombinu ya kiwanja ikiwemo njia ya kurukia na kuondokea ndege (*runway*), pamoja na jengo la abiria (*terminal building*). Kiwanja hiki

ni miongoni mwa viwanja saba ambavyo vimefanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa msaada wa fedha kutoka Benki ya Dunia kwa lengo la kukarabati miundombinu ya kiwanja. Usanifu huo umekamilika na Mhandisi Mshauri amekabidhi Ripoti Serikalini. Kwa kutumia Ripoti hiyo, Serikali imefanya mazungumzo na Benki ya Dunia ili kupata fedha za usanifu wa Viwanja vya Bukoba, Mafia, Arusha, Sumbawanga, Shinyanga na Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi, Benki ya Dunia imekubali kufadhili ukarabati wa barabara ya kurukia na kutua katika Kiwanja cha Ndege cha Tabora kwa kiwango cha lami. Kwa sasa Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege iko kwenye mchakato wa kumpata mkandarasi wa ujenzi. Fedha zitaanza kutolewa kuanzia mwezi Julai 2010 baada ya Serikali kukamilisha mchakato wa kupata mkandarasi na kusaini mkataba wa ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa baadae wa kuimarisha Kiwanja cha Ndege cha Tabora ni kujenga jengo la abiria ambalo usanifu wake na gharama za ujenzi tayari zimeainishwa. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kuhakikisha kuwa jengo hilo linajengwa.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuishukuru Serikali kwa mpango mzuri wa kukitengeneza Kiwanja cha Tabora ambacho kilisahauliwa muda mrefu. Naomba Mwenyezi Mungu aiwezeshe Serikali yetu kutekeleza mpango huo.

Baada ya maelezo hayo, ninaomba niongeze maswali mawili. La kwanza ni kwamba; Uwanja wa Tabora uko wazi sana kwa hiyo wafugaji wana tabia ya kupitisha mifugo bila kujali kwamba ndege zinatua na kuruka kwa hiyo tunahitaji uzio vilevile.

La pili ni kwamba; matengenezo aliyoeleza Mheshimiwa Waziri hayaoneshi kama *the taxi way* pamoja na *apron* navyo ni sehemu ya mradi ambao Serikali inakusudia kuutengeneza. Naomba maswali hayo mawili yajibiwe.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, matengenezo haya pia yatajumuisha pia *apron* na *taxi ways* ambazo zitatufikisha kwenye jengo hili la abiria. Kwa hiyo, matengenezo hayo yatahusisha pia maeneo hayo kama Mheshimiwa Mbunge alivyouliza.

Suala la uzio, kama nilivyojibu swali jana nilisema suala hili tumelipa umuhimu mkubwa kwa viwanja vyetu vyote Tanzania. Kwa hiyo, nitaiomba Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, kwa mafungu mengine wakati wa ujenzi wa runway Tabora basi pia suala la uzio liweze kukamilishwa katika kipindi hicho hicho.

Na. 21

**Kuweka Lami Barabara ya Hungumalwa – Magu**

**MHE. BUJIKU P. SAKILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Barabara ya Hungumalwa – Ngudu – Magu yenye urefu wa kilomita 60 ni ya Mkoa na haina lami; na kwa kuwa barabara hiyo hutumiwa na wasafiri wengi na magari makubwa kutoka sehemu mbalimbali ndani na nje ya nchi (kama Kenya):-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni vema kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kuokoa fedha nyingi zinazotumika kwa ukarabati wa kila mara?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kujenga barabara hiyo kwa lami kutarahisisha usafiri kwa Wananchi wa Tarafa za Mwamashimba na Nyamilama kwenda Ngudu yalipo Makao Makuu ya Wilaya?

(c) Je, Serikali haioni kuwa ikijenga barabara hiyo haraka kwa kiwango ha lami itapunguza msongamano wa magari uliokithiri Jijini Mwanza?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mbunge wa Kwimba, lenye sehemu (a), (b) na (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ingependa kujenga kwa kiwango cha lami barabara zote muhimu na zinazokidhi vigezo kama wingi wa magari na kadhalika, ambazo hivi sasa ni za changarawe lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali ni barabara chache tu zinazojengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, kutokana na kutambua umuhimu wa Barabara ya Hungumalwa – Ngudu – Magu, Wizara ya Miundombinu imeipandisha hadhi sehemu ya Barabara ya Hungumalwa – Ngudu (km 20) kutoka kuwa ya Wilaya na kuwa ya Mkoa mwezi Juni, 2009. Hivyo, Barabara hiyo itaanza kuhudumiwa na Wizara ya Miundombinu kupitia Wakala wa Barabara. Aidha, sehemu ya barabara ya kutoka Ngudu – Magu (km 44.8) imewekwa kwenye Mpango wa PMMR ili kuifanyia ukarabati unaotakiwa kwa kiwango cha changarawe. Mpango huu unahusisha mkataba wa matengenezo ya barabara hii kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2008 hadi 2013.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, napenda kutoa shukrani kwa Serikali kwa kukubali mambo mawili; kwanza, kuipandisha hadhi Barabara ya Hungumalwa kwenda Ngudu kuwa ya Mkoa na Ngudu kwenda Magu kuhudumia PMMR, kwa kweli wananchi wanashukuru sana. Nina maswali mawili:-

(i) Mheshimiwa Rais alipopita kuomba kura mwaka 2005 akitokea Magu alisema Barabara ya kutoka Magu kuja Ngudu itaimarishwa kwa kiwango cha lami fedha ikipatikana, maneno ambayo bado yanatumiwa na Serikali. Je, tangu kipindi kile fedha haijapatikana?

(ii) Kama fedha kutoka Ngudu kwenda Hungumalwa ni nyingi sana kwa lengo tu la kuonesha nia ya kutekeleza Ahadi ya Mheshimiwa Rais; kwa nini sehemu ya ujenzi isigawanywe sehemu mbili, kwanza kutoka Hungumalwa mpaka Ngudu kwa kiwango cha lami (km 20) halafu fedha iendelee kutafutwa kwa ajili ya kumalizia sehemu inayobakia; kwa nini hatua hiyo haijatekelezwa?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ahadi ya Mheshimiwa Rais ya uimarishaji wa Barabara ya Magu hadi Ngudu kama nilivyojibu katika swali la msingi ni kwamba, tutaendelea kuifanyia kazi ifike kipindi ambacho tutaitekeleza kikamilifu. Kwa sasa tumeiweka barabara hiyo kwenye Mpango wa PMMR ili iweze kupitika kwa mwaka mzima bila matatizo kwa kiwango cha changarawe na fedha ya kutosha ikipatikana basi tutaipeleka kwenye hadhi ya lami.

Sasa kwa kipande hiki cha Ngudu mpaka Hungumalwa, nimeeleza kwenye jibu la msingi kwamba, tumetambua umuhimu huo, tumeipandisha hadhi mwaka jana na hivyo tuko katika taratibu za kuhakikisha kwamba tunaweza kuitengea pesa kwa ajili ya kuijenga barabara hii kwa kiwango ambacho kitawezesha kupitika kwa mwaka mzima bila matatizo yoyote.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa matatizo ya Barabara hiyo ya Ngudu yanafanana sana na matatizo ya Barabara ya Songea kwenda Nkenda mpakani mwa Msumbiji na Tanzania; na kwa kuwa katika barabara hiyo Mheshimiwa Rais alishawahi kuja kukagua ujenzi wa daraja lililokamilika na akaahidi kwamba barabara hiyo mara moja ianze kujengwa kwa lami na Mheshimiwa Waziri alipojibu swali langu katika Mkutano wa Kumi na Saba alithibitisha hilo; je, Mheshimiwa Waziri ataniambia sasa bajeti ya mwaka 2010 fedha za ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami zitaonekana katika bajeti hiyo ili kutekeleza Agizo la Mheshimiwa Rais?

**NAIBU SPIKA:** Naona unaharakisha mambo, Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatana na matatizo ambayo tunayatambua, tunapenda kuzijenga barabara hizi zote kwa kiwango cha lami lakini hali ya pesa haituruhusu. Kwa barabara hizi zinazoingia Msumbiji, sasa hivi tumemaliza ujenzi wa Daraja la Umoja na tuna-*focus* katika kulizindua hili daraja pamoja na barabara ambayo inapita kwenye hili daraja. Barabara hizi nyingine tutajitahidi kwa kadiri fedha zinavyopatikana kuzitengea kwa ajili ya ujenzi wake kwa kiwango cha lami.

Na. 22

**Uboreshaji Miundombinu ya Maji Jijini Dar es Salaam**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilichukua jukumu la kutafuta Kampuni ya kuzibua na kuboresha miundombinu ya utoaji maji katikati ya Jiji la Dar es Salaam ambayo ni kampuni kutoka China:-

(a) Je, ni sababu gani zilizofanya zoezi hilo likwame?

(b) Je, kiasi gani cha f edha kimetumika katika zoezi hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Musa, Mbunge wa Jimbo la Mfenesini, naomba niseme kwamba, nimewasiliana na Mheshimiwa Mbunge kama kutakuwa na tofauti kidogo katika majibu basi majibu haya ndiyo yanayokidhi maswali aliyouliza yeye. Baada ya kusema hayo na kwa ajili ya kuweka Hansard vizuri, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia DAWASA imekuwa ikitekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisaji na majitaka kwa kukarabati na kupanua miundombinu yake katika Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Bagamoyo na Kibaha kuanzia mwaka 2003 hadi Desemba, 2009 na kazi hizo zimefanyika kama ifuatavyo: Ukarabati wa mitambo ya majisafi, ukarabati wa matanki na kuzibua na kukarabati mabomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mifereji ya kuondoa maji ya mvua, kwa mujibu wa mgawanyo wa kazi suala hili linashughulikiwa moja kwa moja na Halmashauri za Manispaa za Temeke, Ilala, Kinondoni na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Nimewasiliana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ambaye ameniarifu kwamba, kwa mwaka huu wa 2010/2011, imeandaa Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Miji unaoitwa Strategic Cities. Mradi huu unajumuisha miji minane likiwemo Jiji la Dar es Salaam, Miji mingine ni Mwanza, Tanga, Mtwara, Kigoma, Mbeya, Dodoma na Arusha. Mradi huo umetengewa jumla ya dola za kimarekani milioni 150 ambao ni mkopo kutoka Benki ya Dunia. Katika Mradi huu, Jiji la Dar es Salaam limepewa kipaumbele cha kipekee kabisa kwa kutengewa dola za kimarekani milioni 11.9

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri na naipongeza Serikali kwa mipango mizuri tu ambayo imejiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa mifereji uliofanywa na Kampuni ya Kichina katika Mkoa wa Dar es Salaam, umetumia gharama kubwa sana, lakini ufanisi na *impact* ya kazi yenyewe haionekani mpaka hii leo; je, Serikali inachukua hatua zipi za kudhibiti au kuwachukulia hatua wale wote waliohusika na uzorotaji wa huduma hii

ambayo Wananchi wa Dar es Salaam wanaitegemea na mafuriko bado yanaendelea Dar es Salaam licha ya ukarabati kufanywa kwa kiwango na kwa gharama kubwa sana?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la swali la msingi, mgawanyo wa kazi unaonesha kwamba, Wizara ya Maji inashughulikia masuala ya maji safi na maji taka. Suala la kuzibua mifereji kwa ajili ya maji taka ni suala linaloshughulikiwa moja kwa moja na TAMISEMI kupitia katika Mamlaka nilizozitaja za Manispaa zile tatu.

Pamoja na hayo basi, mimi najua kabisa kwamba, miradi ambayo tumeitekeleza kwa ajili ya maji safi na maji taka, imetekelezwa vizuri na inaendelea vizuri. Sasa kama kuna tatizo lingine, naomba tuwasiliane kwanza, tujue TAMISEMI na Mamlaka hizi kwamba kuna kazi nyingine imefanyika ambayo haikukidhi. Kwa maelezo ambayo Waziri amenipa, inaonesha kabisa kwamba, tayari Serikali imeandaa mradi mahususi kwa ajili ya kazi hizo ambazo Mheshimiwa Zungu amezitaja.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea jamani, muda umekwisha. Nadhani bado inatakiwa kuwasiliana Wizara ya Maji na Umwagiliaji na TAMISEMI. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Dkt. Luka J. Siyame kwa swali linalofuata. Mheshimiwa Zambi anauliza kwa niaba yake.

Na. 23

**Mradi wa Umwagiliaji wa Naming'ongo**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI (K.n.y. MHE. DKT. LUKA J. SIYAME)** aliuliza:-

Kwa kuwa tarehe 24 Desemba 2006 Mradi wa Umwagiliaji wa Naming'ongo Jimboni Mbozi Magharibi ulibomolewa na mafuriko ya Mto Nkana; na katika bajeti ya mwaka 2008/2009 Serikali ilitenga kiasi cha shilingi 750,000,000 kwa ajili ya ukarabati wa mradi huo:-

Je, Serikali kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji inaweza kuwaeleza wananchi hatua iliyofikiwa katika matayarisho ya ukarabati huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Luka J. Siyame, Mbunge wa Jimbo la Mbozi Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 24 Desemba, 2006, mafuriko ya Mto Nkana yalibomoa na kuharibu kabisa banio la Daraja la Skimu ya Umwagiliaji ya Naming'ongo. Ni kweli kwamba, katika mwaka 2008/2009 Serikali ilitenga shilingi milioni 750 kwa ajili ya kufanya ukarabati wa miundombinu iliyoharibika. Hata hivyo, kutokana na upungufu wa fedha, katika mwaka 2008/2009 kiasi cha shilingi bilioni 5.4 zilizokuwa

zimepangwa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji hazikupatikana. Upungufu huu wa fedha uliathiri uendelezaji wa skimu nyingi ikiwemo skimu ya Naming'ongo, ambayo ilipata shilingi milioni 43.5 tu. Fedha hizo zilitumika kufanya uchunguzi wa eneo jipya la kujenga banio, usanifu, makadirio ya gharama mpya za ujenzi na kuandaa makabrasha ya zabuni. Kazi ya uchuguzi *(geotechnical investigations)*, ilifanywa kwa karibu na kwa ushirikiano mkubwa wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Mbeya Institute of Science and Technology. Kutokana na uchunguzi na usanifu huo, Mradi wa Umwagiliaji wa Naming'ongo sasa unakadiriwa kugharimu takriban shilingi bilioni 4.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi wa mradi kwa awamu na tayari mkandarasi anayejulikana kwa jina la GS Construction wa Iringa amekwishaanza kazi. Hata hivyo, kwa sasa mkandarasi huyo amelazimika kusitisha ujenzi kutokana na mvua nyingi inayoendelea kunyesha ambayo inatishia kuharibu miundombinu inayoendelea kujengwa mpaka hapo mvua itakapopungua. Kutokana na tatizo hilo la mvua nyingi, mkandarasi anaendelea na ukusanyaji wa vifaa vya ujenzi visivyoharibika kama vile mchanga, chuma, kokoto na vinginevyo. Kazi ya ujenzi itaendelea tena mara tu mvua itakapopungua. Matarajio yangu ni kwamba, Mradi wa Naming'ongo utatengewa fedha za kuukamilisha katika mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda hapa kukiri kwamba, mafuriko ya mara kwa mara yanasababisha gharama kubwa kwa Serikali pale yanapoharibu miundombinu mbalimbali zikiwemo barabara, madaraja na miundombinu ya umwagiliaji, kwa sababu tunalazimika kutenga fedha nyingi kwa ajili ya kukarabati miundombinu iliyoharibika na kuathiri miradi mipya ya maendeleo. Kwa mfano, shilingi bilioni 4.2 zinazotarajiwa kujenga upya Mradi wa Naming'ongo zingeweza kujenga miradi mingine mipya. Namwomba Mheshimiwa Mbunge na Wakulima wa Naming'ombe, kuwa na subira wakati Serikali inafanya jitihada kukarabati mradi wao.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Miradi mingi ya Serikali imekuwa inajengwa chini ya ubora na kwa hiyo kuharibika au kubomoka mara kwa mara hasa ile ambayo ni ya umwagiliaji. Je, sasa Serikali itakuwa tayari kumsimamia kwa karibu sana huyu mkandarasi (GS Construction) wa Iringa anayejenga ili kuhakikisha kwamba Mradi ule wa Naming'ongo sasa unajengwa kwa viwango vinavyostahili ili kuepuka ubomokaji kama ulivyotokea na kwa maana hiyo kusababisha Serikali kupata hasara kubwa sana?

(ii) Gharama zote zinazokadiriwa kukamilisha mradi huu ni shilingi bilioni 4.2 kama Mheshimiwa Waziri alivyotueleza lakini mwaka 2009/2010 kiasi kilichotengwa ni shilingi bilioni 1.2; sasa namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri alihakikishie Bunge hili na Wananchi wa Mbozi na hususan wale wa Naming'ongo kwamba hizi shilingi bilioni tatu zilizobaki

zitapatikana katika kipindi cha mwaka 2010/2011 ili kukamilisha mradi huo kama yeye mwenyewe alivyolieleza Bunge lako Tukufu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba miradi inajengwa chini ya ubora au haisimamiwi isipokuwa mafuriko ni suala ambalo linatokea nje ya uwezo wetu, maana mafuriko haya hayaharibu miradi ya umwagiliaji tu, hata barabara, reli na miundombinu mingine huharibiwa.

Linapotokea jambo kama hili, hili ni suala ambalo kiutaalam nataka nimwambie Mheshimiwa Zambi kwamba, liko nje ya uwezo na hata kimkataba linajulikana kama *force majoure*. Hili ni tatizo ambalo liko nje, likitokea ndio maana Serikali inalazimika kuingilia tena kurudisha miundombinu hiyo.

Napenda nimhakikishie kwamba, mradi huu sasa katika ukarabati unasimamiwa moja kwa moja kiutaalam na Wizara yangu chini ya Ofisi ya Kanda na hata Makao Makuu na tutahakikisha kwamba, tutasimamia kwa ubora unaotakiwa kimkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu gharama za kukamilisha mradi kwa bilioni tatu zilizobaki, naomba Mheshimiwa awe na subira kwa sababu tutakuja tena hapa na maombi ya fedha kwa ajili ya awamu ya pili ya kukamilisha mradi huu. Matarajio yangu ni kwamba, tutakapoleta bajeti hiyo, basi itajadiliwa na hatimaye itapitishwa kulingana na fedha zitakavyopatikana.

Na. 24

**Kampuni za Simu za Mkononi**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa kampuni nyingi za simu za mkononi zinafanya shughuli zake hapa nchini:-

(a) Je, ni kampuni ngapi za aina hiyo zimesajiliwa hapa nchini mpaka kufikia mwezi Februari, 2009?

(b) Je, ni watumiaji wangapi wamesajiliwa hadi kufikia Februari, 2009?

(c) Je, Serikali inafaidika kwa kiasi gani kimapato kutokana na kampuni hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Hadi kufikia Februari, 2009 kampuni 12 zimepewa leseni ya kutoa huduma za mawasilino ya simu. Kampuni hizo ni pamoja na Benson Informatics Limited (BOL), Celtel Tanzania Limited (Zain), Dovetel Tanzania Limited (SASATEL), Epocha & Golden Ocean Tanzania Limited (EGOTEL), ExellentCom Tanzania Limited (HITTS), My Cell Company Limited (My Cell), MIC Tanzania Limited (TIGO), Tanzania Telecommunication Company Limited (TTCL), Vodacom Tanzania Limited (VODACOM), Zanzibar Telecom Limited (ZANTEL), Six Telecom Company Limited na Smile Tanzania.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2009 jumla ya kadi za simu (simcard) zipatazo 13,006,793 zimetolewa kwa Watanzania. Idadi ya matumizi ya simu nchini kwa ujumla hadi kufikia mwezi Februari, 2009 ni zaidi ya 13,130,602 zikiwemo simu za mezani zipatazo 123,800.

(c) Serikali inapata mapato kutokana na tozo za kodi mbalimbali kutokana na huduma za mawasiliano ya simu za mkononi. Kuanzia mwaka wa fedha wa 2001/2002 hadi mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali imepata jumla ya shilingi 660,869,024,295. Aidha, kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008 pekee, Serikali ilipata shilingi 209,300,805,396. Uchangiaji wa Sekta ya Mawasiliano kwa pato ghafi la taifa kwa mwaka 2007/2008 ilikuwa zaidi ya asilimia 20.1.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru na namshukuru Naibu Waziri kwa majibu ya kina. Hata hivyo nina maswali mawili madogo ya kumuuliza:-

(i) Pamoja na maelezo ya fedha inayokusanywa bado kuna wasi wasi kuwa kuna baadhi ya kampuni hazilipi kodi ipasavyo; Serikali inasemaje juu ya hilo?

(ii) Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuweka mkongo wa mawasiliano na haya makampuni kusema wanatoa ofa ama za shilingi 500 kwa kutwa au vinginevyo lakini bado inaonekana kuna tatizo kubwa la mawasiliano katika makampuni mbalimbali na kiasi kwamba sisi watumiaji tunapata shida kubwa sana katika kutumia hizi simu. Je, Serikali inasemaje, hii *Regulatory Authority* ya mambo haya inafanya nini katika kuzuia hizi *jam* ambazo zinaonekana labda ni za makusudi ili kupunguza ule muda wa matumizi na kwa hiyo makampuni kujitengenezea faida? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Khalifa na kumtoa wasiwasi kwamba, makampuni yote yanayohusika yanalipa kodi zake kupitia Wizara ya Fedha; na kwa sababu Wizara ya Fedha ipo, italichukulia hilo kwa uzito wake kuona ni makampuni gani labda hayalipi.

Pili, napenda nimhakikishire kwamba, TCRA inafanya shughuli zake vizuri sana, lakini ni kweli nikubaliana naye baadhi ya wakati mawasiliano yanakuwa magumu na ukipiga simu unaweza ukaambiwa simu hiyo haipo au haipatikani. Sometime ni kwamba,

huwa wanabadilisha mitambo yao, lakini wakati mwingine kunakuwa na maingiliano, kitu ambacho TCRA inakishughulikia ipasavyo. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mawasiliano yatazidi kuboreshwa na tutaiomba TCRA isimamie ipasavyo masuala haya ili kusiwe na mwingiliano wa mawasiliano.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Waziri alipofanya ziara katika Wilaya ya Liwale aliona kwamba kuna matatizo ya usikivu katika baadhi ya maeneo kwa simu za mkononi. Na siyo hivyo tu, palikuwa na vijiji kadhaa kama vile Melui, Ntapata, Kikulyungu na maeneo mengine ambayo bado mawasiliano hayajaenea. Aliahidi kwamba atafanya mkakati wa kuweza kueneza katika vijiji hivyo katika Wilaya hiyo ambayo ni kubwa mno. Sasa nataka kujua ni lini utaratibu huo utaanza au mikakati yake imefikia hatua ipi ili wananchi hao waweze kujiandaa na kununua simu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, nilipata nafasi ya kutembelea katika Jimbo lake na tulijionea sisi wenyewe. Nikiri tu kwamba, eneo kubwa la Jimbo la Mheshimiwa Kigwalilo linapita kwenye Mbuga za Wanyama, kwa hiyo ni lazima wenye makampuni ya simu watafute teknolojia ambayo inafaa zaidi katika maeneo hayo.

Nilipofika pale kulikuwa na tatizo la pale pale mjini ambalo kwa siku ya pili tu tuliweza kulitatua. Nafikiri Mheshimiwa Mbunge atakuwa shahidi kwamba, kulikuwa na matatizo ya mawasiliano katika magereza na wataalam wakaenda siku ya pili yake kurekebisha hilo. Zaidi ni kwamba, makampuni ya simu haya yote tulikwenda nayo katika maeneo yale na tukawapelekea barua baada ya ziara yetu ile washughulikie, nina hakika wako njiani kutatua matatizo ya Liwale.

Na. 25

**Serikali Kuhamasisha Mawasiliano ya Simu za Mkononi Wilayani Nanyumbu**

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kata za Lumesule, Chipuputa, Napacho na maeneo yanayozunguka Kijiji cha Nangomba Wilayani Nanyumbu hakuna mawasiliano ya simu za mkononi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha kampuni za simu za mkononi kuanzisha huduma hiyo kwenye maeneo yaliyotajwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa mawasiliano katika maeneo mengi ya Mikoa ya Mtwara na Lindi, kampuni ya mtandao wa simu za mkononi ya VODACOM ipo katika hatua za mwisho za kuwasha mitambo ya mawasiliano katika maeneo ya Lukuledi, Mchinga, Nanyanga na Mahuta. Pia, kampuni hiyo tayari imewasha mitambo ya mawasiliano katika maeneo ya Nanyumbu, Mangaka na Mkarangati. Mchakato wa kuyawezesha maeneo ya Mikangaula, Lumesule, Chipukuta, Napacho na Nangomba kwa kuongeza mtambo mwingine katika Kijiji cha Mikangaula unaendelea. Usimikaji wa mitambo mipya katika maeneo hayo unaendelea ili kuwawezesha wananchi wengi waweze kunufaika na huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni za simu za ZAIN, ZANTEL na TIGO zinaangalia uwezekano wa kuboresha huduma ya mawasiliano ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya kibiashara ili kuyaingiza maeneo husika ya Kata za Lumesule, Chipukuta, Napacho na maeneo yanayozunguka Kijiji cha Nang'omba katika mipango yake ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Dunstan Mkapa na Uongozi wa Nanyumbu kwa ushirikiano walionipa wakati nilipofanya ziara katika Jimbo lake.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ya kutia matumaini. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Mheshimiwa Naibu Waziri alipofanya ziara Wilayani kwangu aliongozana na Wataalam wa TTCL na aliwaagiza waone uwezekano wa kuweka mitambo ya baraua pepe, fax na vinginevyo; kitu ambacho mpaka sasa…

**NAIBU SPIKA:** Nenda kwenye swali!

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Kitu ambacho mpaka sasa sijakiona. Je, unasemaje kuhusu hili?

(ii) Hizi kampuni za simu zinapaswa kulipa mrabaha Halmashauri za Wilaya au hapana?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokwenda katika ziara ile kulikuwa na mambo mengi tu ya kuangalia ya mawasiliano ya simu kwa makampuni yote. Na ni kweli niliwaomba Kampuni ya Simu ya TTCL waone uwezekano wa kupeleka huduma si ya fax tu bali ni pamoja na huduma zao ambazo zitawasaidia Wananchi wa Nanyumbu. TTCL nao wanalifanyia kazi suala hilo, hali yao ikiwa nzuri mawasiliano ya simu katika maeneo aliyoyazungumza Mheshimiwa Dunstan Mkapa yatapatiwa ufumbuzi.

Zain tunawashukuru kwamba wame-cover katika Kata kama 12 katika maeneo yale. Inakosekana katika Kata ya Masuguli tu, lakini najua kuna Kata nyingine ambazo zina udhaifu ambazo hivi sasa tumeomba wazishughulikie, usikivu kwao ni mdogo. TIGO nao wana Kata mbili tu, tumewaomba waongeze sehemu nyingine ili watu wawe na choice ya kuchagua mtandao ambao wanaupenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii niyashukuru makampuni ya simu yote kwa juhudi zao wanazofanya kufikisha mawasiliano ya simu katika maeneo yote mijini na vijijini.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Swali langu ni dogo tu; kwa kuwa tatizo ambalo liko Nanyumbu linafanana na tatizo lililopo katika Kata ya Kibati, Tarafa ya Mvomero; Kampuni ya ZAIN ilipokuwa inafahamika kwa jina la CELTEL walikubali kujenga mnara katika eneo la Salawe na Masimba na tayari walishapeleka vifaa lakini sasa ni karibu miaka miwili mkandarasi hajafika na ule mnara haujajengwa. Naomba Wizara itusaidie kuwasiliana na Kampuni ya ZAIN kwa sababu tatizo lililopo sasa hivi Wananchi wa Kata za Kibati, Masimba, Salawe, Hoza na Pemba hawana mawasiliano na tayari wanakijiji walishaandaa maeneo ya kujenga mnara na mkandarasi alishapeleka vifaa lakini leo miaka miwili mnara ule haujajengwa; je, ni lini Serikali itatusaidia mnara ule ujengwe?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimfahamishe Mheshimiwa Saddiq kwamba, tayari nimeshapokea malalamiko ya mawasiliano ya simu Kata ya Kibati na tayari tumewaandikia wahusika wote hasa ZAIN kwa sababu hata saruji iliyopo pale imeharibika na wao nina hakika watachukua shughuli hizi kwa uzito unaofaa.

Naelewa fika kwamba, mawasiliano Kibati ni magumu na wengi wanapata mawasiliano kupitia mnara wa Songwe ambao ni mpakani na Kilindi. Tungependa mawasiliano hayo yaboreke na tayari sisi kama Wizara tumeshachukua hatua kwa kuwaandikia wahusika.

Na. 26

**Idara ya Polisi Ngara Kupatiwa Magari ya Kutosha**

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Ngara inakabiliwa na wimbi kubwa la ujambazi hasa katika Kata za Mugoma, Kirushya, Kabanga, Mabawe, Murusagamba na Baragama ambapo juhudi za Polisi zinakumbana na tatizo la nyenzo hasa magari; na kwa kuwa Wilaya hiyo iko mpakani mwa nchi za Rwanda na Burundi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuipatia Idara ya Polisi Wilayani Ngara magari ya kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Feetham Filipo Banyikwa, Mbunge wa Ngara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Jeshi la Polisi Wilayani Ngara linakabiliwa na uhaba wa vitendea kazi hasa magari. Kwa sasa Wilaya hiyo ina magari mawili na pikipiki tatu. Vifaa hivi ni vichache ukilinganisha na ukubwa wa eneo kijiografia pamoja na tishio la usalama, ikizingatiwa kuwa Wilaya inapakana na nchi za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nia ya Serikali kuzipatia Wilaya zote hapa nchini vitendea kazi vya kutosha ili kukabiliana na uhalifu; hata hivyo, nia hiyo inakwamishwa na uhaba wa fedha kwa ajili ya kununua magari na pikipiki. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi kadiri bajeti ya Wizara yangu itakavyoendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matatizo yatokanayo na uhaba wa nyenzo za usafiri katika Wilaya ya Ngara, Jeshi la Polisi litaendelea kudhibiti hali ya uhalifu na ujambazi katika mipaka ya nchi yetu ikiwemo Wilaya ya Ngara. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, itakapofika mwezi Aprili mwaka huu, Wilaya yake itapatiwa gari moja aina ya Pick-Up, Toyota Landcruser katika jitihada za kupambana na uhalifu na ujambazi.

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nishukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri na ahadi ya kupatikana gari kabla ya mwezi wa Aprili. Pamoja na hayo, ningelipenda kuuliza swali moja la nyongeza:-

Kwa kuwa Vituo vya Mlusagamba, Kabanga na Mugoma havina kabisa usafiri kwa ajili ya doria na kupambana na wahalifu; je, Serikali inatoa ahadi gani kutoa gari la ziada kwa ajili ya hivi vituo vitatu ambavyo viko mpakani kabisa na uhalifu umeongezeka?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, tunazingatia matatizo ambayo yanaikabili Wilaya yake, ukizingatia kwamba imepakana na nchi jirani na upo uhalifu ambao tunautambua. Kwa kuwa nimemuahidi kwamba tutampatia gari jipya, ningeomba aridhike kwa sasa hivi kwamba hilo gari litaweza kufanya doria katika maeneo hayo kwa sababu bado ni jipya na ndivyo tutakavyokuwa tunaiboresha bajeti yetu. Haya maombi si Wilaya ya Ngara tu, yapo katika Wilaya zote katika Nchi ya Tanzania.

Na. 27

**Kuunganisha Umeme Mji wa Kagunga Kutoka Burundi**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA (K.n.y. MHE. KABWE Z. ZITTO)** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa kumekuwa na juhudi za kuleta maendeleo ya kiuchumi katika Mkoa wa Kigoma kama vile miradi mingi ya barabara na bandari ambapo Mamlaka ya Bandari Tanzania inajenga gati kwenye Bandari Ndogo ya Kagunga, ujenzi wa soko kubwa katika mpaka wa Kagunga unaofanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma; na ili kuboresha juhudi hizo za maendeleo ya kiuchumi katika Mji Mdogo wa Kagunga upatikanaji umeme ni muhimu sana:-

Je, Shirika la Umeme (TANESCO) lipo tayari kuanza mazungumzo na Shirika la Umeme la Burundi ili waweze kuunganisha umeme katika Mji Mdogo wa Kagunga hasa ikizingatiwa kuwa Mji wa Nyanza Lac wenye umeme upo jirani na Kagunga?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano wa Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Gisenyi Rwanda mwishoni mwa mwezi Oktoba, 2009, Mawaziri wa Nchi za Burundi, Rwanda na Tanzania walikubaliana kuitisha kikao cha wataalam ambacho kitafuatiwa na Kikao cha Mawaziri ili kuzungumzia masuala ya ushirikiano katika kuzalisha na kusafirisha umeme baina ya nchi zetu, yaani hususan Mradi wa Umeme wa Rusumo. Namna hii ya ushirikiano wa Tanzania na nchi jirani katika kufanikisha upatikanaji wa umeme kwa wananchi ni utaratibu ambao unatumika na Nchi za Uganda, Zambia na Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji Mdogo wa Kagunga upo kama kilomita 30 kutoka Mji wa Burundi wa Nyanza Lac wenye umeme. Serikali itaielekeza TANESCO kufanya mazungumzo na Shirika la Umeme la Burundi ili kuona kama kuna uwezekano wa kuunganisha njia ya umeme kutoka Mji wa Nyanza Lac nchini Burundi ambako kuna umeme hadi Mji Mdogo wa Kagunga.

Ni vyema pia kuzingatia kwamba, uzalishaji umeme Burundi ni mdogo na kwa hivi sasa Burundi inazalisha jumla ya MW 35 na mahitaji ya nchi hiyo yote yanakadiriwa kuwa kama MW40.

Aidha, hivi karibuni Serikali ya Burundi ilikuwa inafanya uboreshaji wa njia ya usafirishaji wa umeme kwenda Nyanza Lac. Pia tutawaelekeza TANESCO wafanye tathmini ya njia mbadala ya Kigoma kupitia Manyovu nchini Tanzania kama ni muafaka

kiufundi na yenye maslahi kwa Taifa ili kuhakikisha Mji Mdogo wa Kagunga unapatiwa umeme.

Mheshimiwa naibu Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaongeza agenda ya kutafakari uwezo wa kupata umeme Kagunga kutokea Nyanza Lac ili ijadiliwe kwenye vikao vya Mawaziri wa Nishati wa Nchi hizi. Kutegemeana na tathimini za wataalam zitakavyobaini na kulingana na hoja husika za kiuchumi, kijamii na kisiasa, Serikali itafanya maamuzi stahili.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake amesema kwamba Burundi wana umeme kidogo, kwa hiyo itakuwa ni ngumu kwa wao kupitisha umeme Nyanza Lac kwenda Kagunga. Sasa kwa nini amesema watafanya mazungumzo kuhusiana na suala hilo wakati anajua kwamba ule umeme wa Burundi ni mdogo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba majibu kwa kifupi sana, maana maswali ya nyongeza watu wanajibu kirefu. Kwa nini mnafanya mazungumzo wakati umesema umeme hautoshi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema Burundi wana umeme mdogo na sisi kama Tanzania tuna mikataba ya namna hii na nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe mfano wa Zambia, Zambia walikuwa na umeme mdogo sana, lakini pamoja na kuwa na umeme mdogo, kwa sababu ya maslahi ya kisiasa na ya kijamii baina ya nchi zetu hizi mbili, sisi tulikuwa tunachukua umeme Zambia kutoka Kituo cha Mbala hadi Sumbawanga, umbali wa kilomita 120.

Umeme ulikuwa unakuja kwa matatizo kwa sababu matatizo yenyewe kule Zambia yalikuwa ni makubwa, lakini bado kwa sababu ya makubaliano na ujirani mwema, tulikuwa tunapata umeme wa MW 3 na kiasi kidogo kuja Mji wa Sumbawanga.

Kwa hiyo, katika mazingira hayo, kulingana na mahitaji ya Kagunga, Kagunga ni mji mdogo lakini una *potential* za kuwa na *activities* za kiuchumi, tutazungumza na wenzetu Burundi tuangalie kama katika huo umeme wao mdogo ambao wanaupata wanaweza kutupa na sisi kidogo ukaenda Kagunga.

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini ningependa kuomba nafasi hii niitumie kwenye swali linalofuata la Busega. Ahsante.

Na. 28

**Utekelezaji wa Mradi wa Umeme – Busega**

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Kwa kuwa umeme wa Lamadi, Kalemera, Nyamikoma, Nyakaboja hadi Nyashimo na ule wa Lamadi, Mkula Hospitali, Igalukilo, Malili hadi Ngasamo Ginnery na Nyashimo, Nyamatembe, Shighala na Mwanangi, Badugu umekuwa uko ndani ya mpango wa Serikali kwa muda mrefu:-

(a) Je, mradi huu utaanza lini na kampuni gani imeteuliwa kutekeleza mradi huo?

(b) Je, ni fedha kiasi gani imetengwa kwa ajili hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Chegeni, Mbunge wa Busega, lenye sehemu A na B kwa pamoja kama ifuatavyo.

Serikili imekuwa na mpango wa kusambaza umeme katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Mpango huo umechukua muda mrefu kutokana na ukosefu wa fedha za kugharamia mradi huo kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Mradi huo umeshaanza kutekelezwa ambapo vijiji vya Kalemela, Nyamikoma, nyakaboja hadi Nyashimo vitapatiwa umeme kwa ufadhili wa wakala wa Nishati na vijijini *REA*. Mwaka wa fedha wa 2008/2009 wakala wa Nishati vijijini (REA) Walitenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa kupeleka umeme katika vijiji vya Nyamikoma na Kalemela mradi huo unakadiriwa kugharamia shilingi kama milioni 835.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi hicho cha fedha kitatumika kwa ujenzi wa kilomita 12 za njia ya umeme ya msongo wa *KV 33* kutoka Magu ufungaji wa transfoma ya ukubwa wa *KV 200* na ujenzi wa kilomita mbili za njia za umeme wa msongo *KV 04* katika kijiji cha Nyamikoma.

Vilevile fedha hizo zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa kilomita 16 za njia ya umeme wa Msongo wa *KV 33* kutoka Bunda Ufungaji wa *transfoma* ya *KVA 100* pamoja NA ujenzi wa kilomita moja ya njia ya umeme ya msongo wa *KV 0.4* katika Kijiji cha Kalemela.

Mheshimiwa Naibu Spika, uteuzi wa Kampuni ya kutekeleza Mradi huo utafanyika mara baada ya kukamilika kwa mchakato wa *tender* ya kumpata Mkandarasi. *Tender* ilifunguliwa Mwezi Novemba, 2009 na hivi sasa iko kwenye tathimini ya kuatiwa no *objection* kupitia Bodi ya REA inatarajiwa kukutana kutoa ridhaa hiyo tarehe 29 Januari 2010. Bank ya Maendeleo ya Africa *(African Development Bank (ADB)* inafadhili mradi ujulikanao kama *Electricity Five*, Mradi ambao unahusu kupeleka umeme katika Miji na baadhi ya Vijiji vya Mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Arusha.Na kuboresha huduma za umeme katika maeneo mbalimbali. Vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vilivyobaki vya Ramadi, Mkula Hospital, Kalukilo, Malili,

Ngasamo *Ginnery*, Nyamatembe, Shigala, Mwanangi, Nabadugu vitapatiwa umeme kupitia mradi huo wa *Electricity Five* na utekelezaji wake unafanywa na *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, zabuni kwa ajili ya kumtafuta mshauri muelekezwa wa mradi huu ni ilitangazwa mwezi julai 2009 na ripoti imepelekwa Benki ya Maendeleo ya Afrika ili watoe maoni yao.

Benki ya Maendeleo ya Afrika wametaka Mkataba kati ya TANESCO na Wizara ya fedha na Uchumi usainiwe, Wizara ya Fedha na Uchumi iliwasilisha TANESCO mkataba huu tarehe 11 januari 2010 kwa ajili ya kusainiwa na jana tarehe 26 Januari 2010 TANESCO wameusaini mkataba huo na kuuwasilisha Wizara ya Fedha na Uchumi. Punde Mkandarasi wa Ujenzi atakapopatikana fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi huu fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi huu zitatolewa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Chegeni swali la nyongeza.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika na nimeridhika na majibu mazuri sana ya Serikali walau kwa mara ya kwanza kwa suala hili. Suala hili limechukua muda mrefu sana lakini nimeona commitiment za Serikali na kama unavyosikia wanasema kwamba jana wamesigni mkataba, mwezi huu wamekamilisha hiki ni kitendo kizuri sana ninachosisitiza ni kwamba Serikali kupitia Wizara hii ya Nishati na Madini kuhakikisha kwamba mikataba hii inatekelezeka katika muda ambao umepangwa asante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mollel swali la nyongeza.

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ukosefu ulioko katika Jimbo la Busega ni sawa kabisa na tatizo la umeme lililoko katika Jimbo la Arumeru Magharibi ambapo Serikalia mara kwa mara imetoa ahadi ya kupeleka umeme katika vijiji vya Oljoro. Oldonyo Sambu, Sambasha na Ikidena je Serikali itatimiza lini ahadi yake hii ya kupeleka umeme katika vijiji hivyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini naomba ujibu kwa kifupi kabisa kwani wewe unajua mambo mengi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya maeneo ya Oljoro, Oldonyosambu na maeneo mengine ya Arumeru yana ufadhili wa *Sources* mbili. Moja ni *African Development Bank* kama nilivyosema wakati najibu swali la msingi katika Mikoa ya Arusha pia kuna ufadhili ambao utakwenda Arumeru kwako na kwa Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari na ufadhili wa upande wa pili wa miradi utatokana na pesa zinazo tokana na uwakala wa nishati vijijini *REA*. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba lile moja la *African Develpment* kama tulivyosema lilikuwa linasubiri kusainiwa kwa mkataba baina ya Wizara ya Fedha na *TANESCO* ambao tayari limeoita na hili jingine linatokana na Serikali ku-release fedha kwenda *REA* na *REA* kwa kadri hiyo wanatekeleza miradi hiyo kulingana na

upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo, nina mhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba litapata utekelezaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mungai nyongeza ya mwisho.

**MHE. JOSEPH J. MUNGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa vijiji kadhaa vya Wilaya ya Mufindi vinafanana kabisa na vile alivyovitaja Mheshimiwa Dr. Chegeni. Kwa kuwemo katika mpango kwa muda mrefu na hata kuwemo katika Bajeti ya mwaka huu lakini utelezaji bado haujaanza. Mheshimiwa Waziri anawapa matumaini gani Wananchi wa kijiji cha Ifwagi ambao katika Bajeti waliahidiwa kutekelezewa Mradi wa umeme na *REA?* Pia wananchi wa vijiji vya Rungemba,Kiterewasi pamoja na Chuo Cha Maendeleo ya Wanawake cha Rungemba ambao wameahidiwa na kuwemo mpango wa MCC *Melenium Challenge Corporation* lakini utekelezaji haujaanza na ni miradi iliyomo katika Ilani. Je, Waziri anawapa matumaini gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:**Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Ifwagi ni kweli umepata ahadi ya muda mrefu lakini kuna baadhi ya miradi pale lakini kuna mwingine unakwenda ndani kwenye mashamba ya chai. Tayari *REA* wamekwishaweka *commitment* ya kuanza kupeleka umeme kwenye maeneo hayo na nilipenda kusema kwamba vyanzo vya Iringa vinatofautiana kidogo na Mwanza kwasababu uhakika wa upatikanaji wa umeme Iringa ni mkubwa zaidi kwasababu ya matatizo madogo ya *transmission*, kwasababu vyanzo vya umeme vikubwa viko palepale. Kwa hiyo *REA* Wameahidi kwamba wataanza kupatia utekelezaji miradi hii ya Ufwagi na ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mungai, Mjomba wangu kwamba tutafuatilia kwa karibu hii miradi ya Ifwagi kwa ajili ya utekelezaji hii ya Rungemba na Kitarawasi ambayo inashughulikiwa na *MCC. MCC* ilipata kama tunavyofahamu kulikuwa na matatizo kidogo ya ucheleweshaji wa *MCC* lakini *consultant* ameshachaguliwa na yuko kwenye uteuzi wa Wakandarasi na ni imani kwamba miradi yote ya *MCC* Mkoa wa Mwanza, Dodoma, Tanga, Morogoro, Iringa yote itaanza kuonekana utekelezaji *on the ground* baada ya Wakandarasi kupata *instruction* za *consultant* tunakadiria kwenye mwezi wa 3 mwishoni au mwezi wa nne tutaanza kuona harakati za ukandarasi kwenye miradi ya *MCC* kwenye maeneo mbalimbali.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda umepita na maswali yamemalizika. Nina matangazo kwanza ya wageni. Bado ninasisitiza wageni wanaotakiwa watangazwe waandikwe na kupelekwa kwenye Idara husika. Ukileta vi – *sheet* vidogodogo hapa itakuwa tatizo kuvisoma. Kwa hiyo, ninao wageni hapa tunaowatambulisha. Wageni hao ni wa Mheshimiwa Lubeleje ambao ni wanafunzi 35 kutoka Chuo cha Mifugo Mpwampwa popote walipo wasimame. Karibuni sana nadhani mnaendeleza mifugo pamoja na matatizo ya mafuriko.

Halafu tuna wanafunzi 28 na walimu wanne kutoka shule ya *Independent* ilitoko Dar es salaam wamekuja kwa ajili ya kutembelea Bunge na kujifunza maswali ya Demokrasia. Wanafunzi wote wa shule hiyo wasimame pamoja na walimu ahsante sana na wengine wadogo sana tumefurahi sana kuwapokeeni nadhani wahudumu wa Bunge

watawafundisha yaliyopo hapa, hawa ni wale walioandikwa rasmi hawa wenye vikaratasi watanipa shida.

Kuna Katibu wa Wazazi nafikiri hawa ni wa CCM Wilaya ya Ilala Ndugu Fadhili Mlami yuko wapi? Karibu sana Ndugu Fadhil Mlami ni mgeni wa Bunge wa Wilaya ya Ilala akiwepo Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Sophia Simba, karibu sana Bwana Katibu.

Tangazo la kazi na wengine mlioko mnakaribishwa siyo hao waliotangazwa ndiyo wageni ni pamoja na ninyi mlioko kwenye *Public Gallery* mnaruhusiwa kuja kuliangalia Bunge lenu kwa wakati wenu. Sasa shughuli za kazi Mheshimiwa Anna Kilango Malecela yeye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundo Mbinu anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kuwa kutakuwa na kikao leo tarehe 27 Januari, 2010 saa saba mchana katika ukumbi namba 227 ghorofa ya pili. Hii ni kujadili Muswada wa Sheria ya mawasiliano na *Elektronic* na Posta ambao wameanza kujadili.

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Katiba Sheria na Utawala, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati leo saa saba mchana katika ukumbi namba 219. Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hiyo waende bila kukosa. Halafu Mheshimiwa Ali Mohamed Armeir, Katibu wa Kamati ya Wabunge wote wa CCM anatangaza kwamba amewagawia wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya CCM mwaliko wa kikao cha tarehe 27 Januari, 2010 yaani leo saa saba na nusu mchana. Lakini kikao hicho kimeahirishwa kitafanyika muda huohuo kesho tarehe 28 Januari, 2010. Kwa hiyo, waliopewa hizo barua wajue kuna mabadiliko ya agenda. Baada ya kusema hayo tunaendelea na shughuli za leo. Katibu endelea.

## MUSWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*(Kusomwa mara ya Kwanza)*

Muswada wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga wa Mwaka 2009 *(The Nursing and Midwifery Bill, 2009).*

Muswada wa Sheria ya Mawsiliano ya *(Elecronic na Posta wa Mwaka 2009 (The Electronic and Postal Communication Bill, 2009).*

Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2009*( The written laws (Miscellaneous Amendments) (No 3) Bill, 2009].*

Muswada wa Sheria ya Usajili wa Ubunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi wa Mwaka 2009*[The Archtects and Quantity Surveyors (Regisration) Bill, 2009].*

Muswada wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi wa Mwaka 2009 *[The Election Expenses Bill, 2009].*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi wa Mwaka 2009 *[The Electoral Laws [Miscellaneous Amendments] Bills, 2009.*

*(Miswada iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwamba Miswada yote tuliyonayo haikuweza kusomwa kama inavyotakiwa katika kifungu cha (94) kwamba kila Muswada ukiletwa katika Bunge hili haipaswi ishughulikiwe katika Bunge hili na katika hatua zingine. Lakini Miswada hii kutokana na umuhimu wake na Kamati ya uongozi imekaa na kukubaliana na umuhimu wa Miswada hii imebidi tuipitishe katika hatua zote katika kikao hiki kimoja. Lakini hatuwezi kufanya hivyo mpaka tutoe hoja ya kutengua ile Kanuni ili iweze kuingia katika hatua zote zinazostahili kwa hiyo tuendelee na hatua inayofuata.

*We are sorry Mr Ambassador from Sweeden we did not recognize your presence here. We are very sorry for that we couldn't introduce you from the beginning. But we have the great pressure to introduce you to the House that he is the Ambassador of Sweden. He is accompanied with other people including* Ndugu Tumsifu Mmari *and Iam sure the other is an assistance. You are most welcomed to our places and I hope you will have a good time here in Dodoma thank you.* Waziri wa nchi.

**Kutengua Kanuni ya Masharti Kuhusu Muswada Kupitishwa Katika Hatua zake Zote**

**WAZIRI WANCHI OFISI YA WAZIRI MKUU BUNGE, SERA URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 80 Kanuni ndogo ya (2) Kanuni ya 83 na Kanuni ya 93 (1) ya Kanuni za Bunge toleo la mwaka 2007. Zote zimeweka masharti kwamba Muswada wa Sheria mara baada ya kutangazwa kwenye gazeti la Serikali utasomwa kwa mara ya kwanza Bungeni na kwamba Bunge halitashughulika hatua zaidi ya moja kwa Muswada wowote wa Sheria katika Mkutano moja nina nukuu ile Kanuni ya 80 (2)

" Tangazo la kwanza la Muswada wa Sheria litatolewa na Kumfikia Katibu wa Bunge katika muda usiopungua siku 21 kabla ya Muswada huo kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza na litaonyesha Muswada mzima ikiwa ni pamoja kuhusu madhumuni ya Muswada husika yaliyotiwa *sign* na Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kanuni ya 83 (1) Muswada wowote wa Sheria ambao umetangazwa kwenye gazeti unaruhusa kuwasilishwa Bungeni kufuatana na Orodha za Shughuli ili kusoma mara ya kwanza na katika hatua hiyo Katibu atasoma jina refu la Muswada wa Sheria unaohusika bila hoja yoyote kutolewa kwa ajili hiyo kama ilivyofanyika sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika Kanuni ya 83 (2) hakutokuwa na mjadala wowote wakati Muswada wa Sheria kusomwa mara ya kwanza. Kanuni 93 (1) Bunge halitashughulikia hatua zaidi ya moja kwa Muswada wowote wa Sheria katika Mkutano mmoja wa Bunge sasa Kanuni ya 93 (2) ya kanuni ya Bunge toleo la 2007 imetoa

utaratibu wa namna ya kupeleka Miswada Bungeni na kushughulikiwa katika hatua zake zote na ninaomba kunukuu kanuni hiyo ya 93 (2)" Bila kuathiri masharti ya fasili ya kwanza ya kanuni hii Bunge linaweza kushughulikia Muswada wa Sheria katika hatua zaidi ya moja endapo kwanza hoja mahususi itatolewa kwamba Muswada huo ushughulikiwe katika hatua zaidi ya moja.

Pili Spika ataridhika na hoja hiyo na tatu Bunge litaafiki hoja hiyo kwa kuipigia kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano Wabunge wa Kumi na saba uliokamilisha shughuli zake tarehe sita November mwaka 2009. Hakukuwa na Muswada wowote uliowasilishwa kwa ajili ya kusoma mara ya kwanza kama yalivyo matakwa ya Kanuni za Bunge hata hivyo zilikuweko ahadi za Serikali kuleta miswada ambayo inakusudiwa kusomwa hatua zake zote katiaka Mkutanio huu wa kumi na nane wa Bunge ambao umeanza jana na unaendelea.

Kutokana na hali ahadi hiyo basi na baada ya kumaliza michakato ya waandishi wa Miswada hii nakupitishwa kwenye Baraza la Mawaziri na kutangazwa kwenye gazeti la Serikali, Serikali sasa inaomba kutoa hoja chini ya kanuni ya 93 ( 2) kuliomba Bunge lako likubali kujadili na kuipitisha Miswada ya Sheria iliyosomwa kwa mara ya kwanza leo katika hatua zake zote katika Mkutano huu wa kumi na nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miswada inayohusika ni kama ifuatavyo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2009( *The written laws (Miscellaneous Amendments) (No 3) Bill, 2009.*

(ii) Muswada wa Sheria ya usajili wa Ubunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi wa Mwaka 2009*[The Archtects and Quantity Surveyors (Regisration) Bill, 2009]*.

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi wa Mwaka 2009*[The Electoral Laws [Miscellaneous Amendments] Bills, 2009.*

(iv) Muswada wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi wa Mwaka 2009*[ The Election Expenses Bill, 2009]*.

(v) Muswada wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga wa Mwaka 2009 *[The Nursing and Midfery Bill, 2009]*.

(vi) Muswada wa Sheria ya Mawasiliano ya *(Elecronic na Posta wa Mwaka 2009( The Electronic and Postal Communication Bill, 2009)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu zinazoifanya Serikali kutoa hoja hii ni kutokana na umuhimu wa Miswada yenyewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ikumbukwe kwamba Bunge hili la tisa sasa linafikia ukomo wake kama inavyojulikana ni mwezi Julai mwaka huu wa 2010.

Muda uliobakia ili Serikali ya awamu hii iweze kukamilisha ratiba yake ya utunzi wa Sheria ni mfupi na hivyo Miswada hii isipopitishwa kupitia Mkutano huu kuna uwezekano mkubwa wa kushindwa kukamilisha agenda ambazo zimepangwa katika Mkutano mmoja uliobakia, Mkutao wa pili kwa kuwa mkutano mwingine unaofuatia ni kwa ajili ya kupitisha Bajeti tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pili Miswada inayowasilishwa katika Mkutano huu ina umuhimu wa kipekee sana kwa wakati huu kwani ni Miswada ambayo ina uhusiano mkubwa sana na Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu 2010.

Hivyo kulazimika ipitishwe katika Mkutano huu ili Kanuni zinazo ambatana na utekelezaji wa Sheria hizi ziweze kuandaliwa kabla ya Uchaguzi Mkuu na mwisho ziko shughuli ambazo zimeshaanza kutekelezwa na Serikali na zinahitaji ulazima kwa sheria zake maalumu badala ya kutumia vifungu mbalimbali katika sheria tofauti kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imetolewa na kuungwa mkono kikamilifu sasa nitawahoji. Naamini waliosema ndiyo wameshinda kwa maana hiyo Waheshimiwa Wabunge Mara ya Pili katiaka kipindi hiki hiki cha Bunge.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga wa Mwaka 2009
***[The Nursing and Midfery Bill, 2009]***

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kusimama hapa mbele leo. Nimshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kuniwezesha kuwa na Afya njema. Niruhusu nikutakie Heri ya Mwaka mpya wa 2010 na nimtakie pia Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Wabunge wenzangu wote kwa kuingia salama katika mwaka huu wa 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuchukua nafasi kumpa pole Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa niaba ya Watanzania kwa msiba wa Mzee wetu mpendwa Waziri Mkuu Mstaafu Marehemu Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa. Aliyefariki tarehe 31/12/ 2009. Aidha nampa pole sana Mheshimiwa Vita Rashid Mfaume Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kwa msiba huu mkubwa wa kupotelewa na mzazi wake, Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, aidha niwape pole waheshimiwa Wabunge wote waliopoteza ndugu na jamaa zao wapenzi katika kipindi hiki cha hivi karibuni. Sasa kwa Niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga 2009 *(The Nursing and Midfery Bill*, 2009) kama ulivyopangwa katika Shughuli za leo pamoja na jedwali la marekebisho kama lilivyoambatishwa sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuwasilisha hoja yangu naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati wa Huduma za Jamii chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Omar Shaaban Kwaang', Mbunge wa Babati Mjini.

Kkwanza niwashukuru kwa kuuchambua kwa kina Muswada ulioko mbele yenu na kutoa michango na maelekezo ambayo ameniwezesha kuwasilisha Muswada huu pamoja na jedwali la mabadiliko hapa Bungeni siku ya leo.

Aidha naishukuru ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, idara ya Mwandishi Mkuu wa Serikali kwa hatua zote kwa hatua zote walizotekeleza hadi kukamilisha muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile shukrani za dhati ziwaendee wadau wote ambao kwa namna moja au nyingine waliochangia maoni yao katika hatua za awali za maandali na hatimaye katika kukamilisha Muswada huu.

Mchakato wa kuandaa Muswada huu umechukua muda mrefu na ulishirikisha wadau wengi maoni na michango yao imechangua Muswada huu kuwa jinsi ulivyo.

Naomba pia niwatambue wadau walioshiriki katika kutoa maoni yao katika *Public Hearing* wakati Muswada huu ulipowasilishwa katika kikao cha Kamati ya Huduma za Jamii tarehe 13 Mwezi wa kwanza 2010 Jijini Dar es Salaam, wadau hao ni kama wafuatao:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni SIKIKA ambao hapo awali walijulikana kama *Youth Action Volunteers, National Organization for Legal Assistance (NOLA), National Councial for Techno Education* (*NACTE*), Ifakara *Health Institute*, Hubert Kairuki *Memorial University*, Chuo cha Uuguzi Massana na *Legal and Human Right*

*Center* ambao waliwasilisha maoni yao kwa maandishi tarehe 21 Januari, 2010. Michango yao ilisaidia kuboresha Muswada uliombele yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa shukrani hizo sasa ninayo heshima kubwa mbele yenu ili niweze kuwasilisha hoja ya Muswada wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga 2009 *The Nursing and Midwifery Act* 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Muswada, Muswada uliopo mbele yenu unakusudia kutungwa kwa sheria ambayo itashughulikia masuala yanayohusu huduma za Uuguzi na Ukunga ambao itarahisisha pamoja na kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wauguzi na Wakunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Usajili Wauguzi na Wakunga sura Na. 324 *The Nurses and Midwifery Registration Act Cap 2 (3) 2 (25) Revised Edition of 2002* ilitungwa upya mwaka 1992 baada ya kuifuta sheria iliyotungwa mwaka 1952 kutokana na mabadiliko katika sera ya afya. sheria hii imekuwa na upungufu ambao umeathiri utendaji kazi wa Wauguzi na Wakunga na hivyo kutoa mwanya kwa udhibiti na usimamizi wake kuwa mgumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria iliyopo sasa inatoa madaraka kwa Baraza lililoundwa chini ya sheria hii kusimamia maadili ya wanataaluma na usajili tu na siyo mwenendo mzima wa taaluma yenyewe. Kwa kuwa suala la taaluma lina umuhimu sana katika mchakato mzima wa utoaji wa huduma za Uuguzi na Ukunga, haja ya kuwa na Sheria itakayojumuisha kusimamia utoaji wa huduma pamoja na usajili wa Wauguzi na Wakunga ni muhimu sana katika kipindi hiki cha sasa ambapo tumeshuhudia ukiukaji wa maadili kwa baadhi ya wataalamu wa afya hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hayo upo umuhimu wa kufuta sheria iliyopo na kutungwa sheria nyingine itakayowezesha baraza la uuguzi na ukunga Tanzania kutekeleza majukumu yale kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kuwasilisha mapendekezo ya kutunga Sheria ya kusimamia huduma za Uuguzi na Ukunga nchini, hii ni kufuatilia mabadiliko yaliyotokea mwanzoni mwa miaka ya tisini na kuanza kutekelezwa mwaka 1996 mara baada ya kupitishwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha mabadiliko ya kiuchumi pamoja na yake ya sekta ya afya hapa nchini yamesababisha Serikali kutoa msukumo zaidi kwa sekta binafsi kushiriki katika kutoa huduma za afya zikiwemo zile za Uuguzi na Ukunga, Mabadiliko haya yanatoa changamoto katika kusimamia na kudhibiti utoaji wa huduma hii. Kutokana na mabadiliko haya vituo vingi vya kutoa huduma za afya vimeanzishwa ikiwa ni pamoja na Vyuo vya kutoa mafunzo ya Uuguzi na Ukunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya utoaji huduma ya Uuguzi na Ukunga imeongezeka, hii imesababisha ufuatiliaji wa maadili taaluma na huduma zinayotolewa

kutokuwa za kuridhisha. Kwa hiyo, inatakiwa sheria ambayo itawezesha kusimamia utoaji wa huduma ya Uuguzi na Ukunga pamoja na kuweka taratibu za nidhamu ndani ya sekta ya umma na binafsi ili kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa zinakidhi viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inayopendekezwa inazingatia pia mabadiliko yaliyotokea kufuatia mageuzi yanayofanywa na Serikali ambapo zimeanzishwa mamlaka nyingine zinazojihusisha na usimamizi wa taaluma mbalimbali, taaluma ya Uuguzi na Ukunga ikiwa mojawapo. Mamlaka hizo ni pamoja na *National Council for Techno Education* (*NACTE*) na Tanzania *Commision for Commision University (TCU)* na mamlaka nyingine zinazohusiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria zilizozianzisha mamlaka hizi zimepewa kibali cha kuanzisha mafunzo kama Uuguzi na Ukunga bila kuarifu mamlaka iliyokabidhiwa jukumu la usimamizi wa taaluma husika. Sheria inayopendekezwa itazitaka mamlaka hizi kushauriana na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili taaluma ya Uuguzi na Ukunga iweze kusimamiwa vizuri inahitajika sheria ambayo itazingatia maeneo mengi zaidi na yanayojitosheleza kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo muhimu katika Muswada. Mambo muhimu yaliyozingatiwa katika kuandaa Muswada wa sheria ya Usimamizi wa Taaluma ya Uuguzi na Ukunga ni haya yafuatayo:-

1. Jina la Muswada kwa sheria ya Uuguzi na Ukunga *The Nursing and Midwifery Act* badala ya sheria ya usajili wa Uuguzi na Ukunga, *The Nurses and Midwifery Registration Act.*

2. Itaweka madaraka ya Baraza katika kuzimamia elimu ya Uuguzi na Ukunga pamoja na kusimamia mafunzo kwa vitendo.

3. Kuweka utaratibu wa kusajili Wauguzi na Wakunga waliohitimu ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa daftari katika ofisi ya msajili.

4. Kuweka utaratibu wa kusimamia maadili ya Uuguzi na Ukunga bila kusubiri mpaka kuwe na malalamiko.

5. kutoa madaraka kwa wasimamiaji wa huduma za Uuguzi na Ukunga *Supervisory Authority* katika ngazi ya Wilaya, Mikoa na Hospitali za Rufaa.

6. Baraza kupewa uwezo wa kushtaki na kushitakiwa.

7. Baraza kupewa mamlaka ya kusimamia taaluma ya Uuguzi na Ukunga.

8. Kuzuia waajiri kuendelea kuajiri Wauguzi na Wakunga wasiokuwa na leseni.

9. Waajiri kutoendelea kuwaweka kazini Wauguzi na Wakunga waliosimamishwa usajili wao kutokana na kukiuka maadili ya taaluma ili kuruhusu uchunguzi wa ukiukwaji wa maadili kuendelea.
10. Kila Muuguzi au Mkunga kutakiwa awe na leseni yake ambayo atawajibika kuihuisha kila baada ya muda uliopangwa.

11. Kuweka vyanzo vya mapato kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za baraza na utekelezaji wa sheria inayopendekezwa.

12. Sheria imeainisha makosa na adhabu mbalimbali na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uimarishaji wa maadili na taaluma ya Wauguzi na Wakunga Muswada umeweka vifungu ambavyo vitaainisha utendaji kazi ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua za kinidhamu bila kuingiliwa na Waajiri Wauguzi au Wakunga. Aidha muswada umetoa nafasi kwa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania kuratibu huduma binafsi za Ukuguzi na Ukunga zitolewazo na sekta binafsi na hasa vyuo vya kitaaluma na ngazi zote. Lengo ni kuhakikisha kuwa vyuo hivyo vinatoa wahitimu ambao wamefikia viwango vinavyohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpangilio wa Muswada. Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu tisa. Sehemu ya kwanza inatoa masharti ya utangulizi ikiwa ni pamoja na jina la Muswada na ufafanuzi wa maeneo yaliyotumika katika Muswada huu. Sehemu ya pili inaanzisha Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania na mapendekezo kuhusu kazi na majukumu ya Baraza. Pia inapendekeza Wajumbe wa Baraza jinsi watakavyoteuliwa. Sehemu ya tatu inaainisha masuala ya utawala na watumishi wa Baraza vilevile inapendekezwa namna ambavyo Msajili wa Baraza na Naibu wake watakavyopatikana kutoka miongoni mwa watumishi wa umma. Msajili pia atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa Baraza pamoja na kuwa Katibu wa Baraza. Aidha sehemu hii inapendekeza majukumu ya Msajili na jinsi ya kuteua wakaguzi kwenye ngazi ya hospitali za rufaa, Mikoa, Wilaya na taasisi za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne inaweka utaratibu wa usajili na uorodheshwaji wa wauguzi na wakunga ikiwa ni pamoja na mapendekezo ya nani anastahili kupatiwa usajili au kuorodheshwa. Pia sehemu hii inaweka masharti ya jinsi wageni wanaotaka kufanya kazi ya uuguzi au ukunga watapatiwa usajili wa muda, katika sehemu hii vilevile utaratibu wa kumwondoa katika daftari Muuguzi au Mkunga aliyesajiliwa au kuorodheshwa umeainishwa.

Sehemu ya tano inaweka utaratibu wa kusajili na kutoa leseni za uendeshaji wa shughuli binafsi za Uuguzi na Ukunga na jinsi ya kufanya ukaguzi katika sehemu husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya sita inaweka utaratibu wa kupokea malalamiko yanayohusu ukiukwaji wa maadili ya Uuguzi na Ukunga pamoja na utaratibu wa kusikiliza malalamiko na kulipa uwezo baraza kwa kutoa adhabu na kuita mashahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya saba inapendekeza masharti yanayohusu masuala ya fedha za Baraza kama vile utaratibu wa kupata fedha na jinsi ya kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi kwa mujibu wa taratibu za Serikali. Sehemu ya nane inapendekeza adhabu na makosa mbalimbali ambayo yatatendwa chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni sehemu ya tisa inayojumuisha mambo mbalimbali ya kiutendaji na taratibu zake kama vile namna ya utoaji wa taarifa za Baraza, namna ya utoaji wa ada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kumpa uwezo Waziri kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Baraza na utekelezaji wa sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo makosa madogo madogo ya kiuandishi au kiuchapaji katika Muswada huu ambao utaona Waheshimiwa tutakapokuwa tunaupitia ambayo yatafanyiwa kazi na ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wa kukamilisha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho. Baada ya kutoa maelezo haya kwa heshima kubwa naomba Waheshimiwa Wabunge wajadili Muswada huu ulio mbele yao na kuridhia na hatimaye kupitisha na kuwa sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 yaani *The Nursing and Midwifery Act*, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kutoa hoja. Ahsante sana.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika Naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Bunge toleo la 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii yanayohusu Muswada wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga, 2009 *(The Nursing and Midwifery Act, 2009).*

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati yamegawanyika katika sehemu kuu mbili, kwanza maoni ya jumla na pili ni uchambuzi wa Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Muswada huu wa Uuguzi na Ukunga una umuhimu wa kipekee kwa jamii ya Watanzania kutokana na kazi na majukumu ya Wauguzi na Wakunga katika utoaji wa huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wauguzi ni Wataalam pekee ambao hukaa na kutoa huduma kwa wagonjwa muda wote kuliko kada zingine za wataalam hospitalini, na Wauguzi hufanya kazi za:-

- Kutoa huduma za ki-Uuguzi kwa wagonjwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na maadili ya taaluma hiyo;
- Kutoa elimu ya Afya kwa wagonjwa na jamii;
- Kufuatilia matatizo ya kiafya ya wagonjwa katika mazingira yao;
- Kutoa huduma za chanjo kwa mama na watoto na uzazi salama; na
- Kufanya kazi zingine kama inavyoelekezwa na Wakuu wao wa kazi;

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kutokana na kazi nyeti na muhimu wanazofanya Wauguzi na Wakunga kuna umuhimu wa kutunga Sheria ambayo itainua, kukuza na kudhibiti taaluma na huduma za Uuguzi na Ukunga. Hivyo Kamati yangu inakubaliana na Serikali katika kuifanya taaluma ya Uuguzi na Ukunga itambulike kama taaluma muhimu katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kuangalia umuhimu wa Kada hii ni muhimu kuzingatia maeneo yote ambayo huduma hii ya Uuguzi na Ukunga inahitajika.

Kulingana na taarifa ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hali ya huduma za afya nchini ni kama ifuatavyo:-

**JEDWALI Na. 1**

**HOSPITALI NA VITUO VYA AFYA NCHINI**

| **AINA YA HUDUMA** | **SERIKALI** | **TAASISI ZA UMMA NA BINAFSI** | **JUMLA** |
|---|---|---|---|
| HOSPITALI ZOTE | 87 | 132 | 219 |
| VITUO VYA AFYA | 331 | 150 | 418 |
| ZAHANATI | 3038 | 1641 | 4679 |

*Chanzo: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Januari 2010*

*Mheshimiwa Naibu Spika, kote huku Wauguzi na Wakunga wanahitajika, umuhimu wa taaluma hii pia unahusu upungufu wa watalaamu katika sekta ya afya, katika sekta ya afya upungufu wa watalaamu ni kama ifuatavyo:-*

**JEDWALI Na. 2**

**RASLIMALI WATU**

| | **AINA YA HUDUMA** | **UPUNGUFU WA WATAALAM** | |
|---|---|---|---|
| | | SERIKALI (2006) | TAASISI BINAFSI |
| 1 | HOSPITALI ZA RUFAA NA ZENYE HUDUMA MAALUM | 48% | Hospitali zote 87% |
| 2 | HOSPITALI ZA MIKOA | 66% | |
| 3 | HOSPITALI YA WILAYA | 67% | |
| 4 | VITUO VYA AFYA | 59% | 86% |
| 5 | ZAHANATI | 69% | 84% |

*Chanzo: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Januari, 2010*

Mheshimiwa Naibu Spika, Takwimu hizi zinaonyesha kuwa upungufu wa Wataalam wa afya kwa Vituo vya Serikali ni 62%. Kwa maneno mengine ni sawa na 38% tu ya Wataalam wanaohitajika ndio waliopo. Hili ni tatizo kubwa linalohitaji mikakati maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ya Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania *(TNMC)* kuna jumla ya Wauguzi (*Registered)* ni 8,850 na walioandikishwa *(enrolled 14,454* ) Jumla yao wote ni 23,304. Hii ni idadi ndogo sana kulingana na ukubwa wa nchi yetu na idadi ya watu karibu milioni 40

**JEDWALI Na. 3**

**JUHUDI ZA SERIKALI KUKABILIANA NA TATIZO LA RASILIMALI WATU**

| **2005/2006** | **2006/2007** | | **2007/2008** | **2008/2009** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| NURSES | 520 | 611(91) | | 745(134) | 2311(1566) | |
| ALLIEDHEALTH SCIENCESTUDENTS | | | | 493 | 497(3) | - |
| 575(78) | 1520(945) | | | | | |
| | | | | **JUMLA** | **3831** | |

*Chanzo: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Januari, 2010.*

*Post graduate studies* 2008/09 ni wahitimu 170 tu.

**JEDWALI Na. 4**

**VYUO VYA UUGUZI**

**VYUO VYA NGAZI YA CHETI** **VYUO NGAZI YA**

| | | DIPLOMA |
|---|---|---|
| SERIKALI | 15 | 15 |
| TAASISI ZA UMMA NA BINAFSI | 12 | 22 |
| **JUMLA** | **27** | **37** |

*Chanzo: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, 2010.*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zinazopaswa kuzingatiwa pamoja na kutungwa kwa Sheria hii ni pamoja na:-

- Baadhi ya Wahitimu kuajiriwa kwenye Taasisi zingine na hata wengine kufanya kazi tofauti.
- Vyuo vichache vilivyopo havipati maombi ya kutosha – bila shaka kutokana na sifa zinazohitajika.
- Wahitimu wengine baada ya kupangiwa vituo vya pembezoni mwa nchi hawaendi kuripoti vituoni. Bila shaka wanaona ni mazingira magumu.
- Maslahi ya Wauguzi na Wakunga ambao ndio wanaokaa na Wagonjwa saa 24 kuliko kada nyingine bado ni madogo. Serikali inapaswa kuongeza maslahi yao ikiwa ni pamoja na posho ya mazingira magumu ya kazi. Si sawa hata kidogo kuwalipa Wauguzi mishahara midogo kuliko Watumishi wa Idara zingine ambazo hulipwa zaidi
- Wauguzi na Wakunga wanaofanya kazi kwenye taasisi binafsi na zingine za Umma walipwe na kupandishwa Madaraja kama wenzao waliopo Serikalini. Hivi sasa taasisi zingine zinawalipa mishahara chini ya viwango vinavyotakiwa. Tunashauri Serikali ichunguze jambo hili na Taasisi zinazokiuka taratibu za kuwalipa na kuwapandisha Madaraja zichukuliwe hatua. Taasisi hizo ziache visingizio vya kuwa na vipato vidogo vinginevyo wasingepaswa kuanzisha vituo hivyo na kuwaajiri kwa viwango vidogo.
- Wauguzi na Wakunga wanaodai posho zao mbalimbali za likizo, uhamisho na malimbikizo ya madai yalipwe haraka ili kuondoa manung’uniko wakati wakifanya kazi hii nyeti ya kuwawananchi.
- Wauguzi na Wakunga wawe wakipata Elimu mara kwa mara kupitia mafunzo kazini ili kuinua taaluma yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utungaji wa Sheria kama hii unahitaji fedha zaidi kwenye Bajeti. Hivyo tunashauri kuwa Bajeti ya Wizara kwa 2010/2011 iongezwe na zaidi tufikie 15% ya Azimio la Wakuu wa nchi za Afrika – *Abuja Declaration.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata nafasi ya kujadili Muswada huu katika vikao viwili ambavyo vilifanyika katika ukumbi mdogo wa Bunge Dar es Salaam. Katika kikao cha kwanza kilichofanyika tarehe 13 Januari, 2010, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii alitoa maelezo ya jumla juu ya madhumuni ya Muswada. Kikao hiki kiliwashirikisha baadhi ya wadau wa Sekta ya Afya wakiwemo:-

*Legal and Human Right Centre;nola (National Organization for Legal Assistance);Youth Action Volunteer (SIKIKA);Ifakara Health Institute;*Chuo Kikuu cha Herbert Kairuki; Chuo cha Uuguzi Aga Khan; Chuo cha Uuguzi (Chuo Kikuu Muhimbili); Chuo cha Uuguzi Massana; na *National Counsel for Technical Education (NACTE)*

Mhesimiwa Naibu Spika, Kamati inawashukuru sana wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao ambayo yamezingatiwa na Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, katika kuishauri Serikali ili iyazingatie katika Jedwali la marekebisho ya Muswada wa Sheria hii ya Uuguzi na Ukunga 2009. Katika kikao cha pili kilifanyika tarehe 21 Januari, 2010, Kamati ilizingatia maoni ya wadau, Mwanasheria toka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na ufafanuzi uliotolewa na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipitia sehemu, ibara na vifungu vya Muswada na kuishauri Serikali kupitia Mwanasheria Mkuu kurekebisha ibara, maneno na sentensi ili yaendane na lugha ya kisheria na jedwali la marekebisho liletwe mbele ya Bunge lako Tukufu.

Baadhi ya vifungu vya Miswada vilivyoanishwa na kufanyiwa marekebisho wakati wa kujadiliana na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii katika sehemu mbalimbali ni kama vifuatavyo:-

Kifungu cha 25(2)(e);
Kifungu cha 15(1) ;
Kifungu cha 15(1)(a)-(d);
Kifungu cha 28(1)(a);
Kifungu cha 28(1)(b); na
Kifungu cha 32(2) **.**

Marekebisho haya yanapaswa kuonekana kwenye Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Kamati inashauri kuongeza maneno katika baadhi ya vifungu ili viweze kuleta maana itakayojitosheleza, vifungu hivyo ni:-

1. Kifungu cha 6(c) cha Muswada, neno *'update'* liongezwe katika majukumu ya Baraza na isomeke ifuatavyo, *"ensure that Register and Roll of nurses and midwives are kept, maintained and updated in the prescribed manner;*

2. Sehemu ya IV ya Muswada, katika kichwa cha habari, liongezwe neno *licensing* na kisomeke *'Registration, enrolment and licensing of nurses and midwives;*

3. Kifungu cha 25(2)(a) kiongezwe neno *professional* ili kulifanya neno *misconduct* kueleweka zaidi; na

4. Kifungu cha 25(3) kiongezwe neno *professional* kabla ya neno *misconduct*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kifungu cha 3 cha Muswada, Kamati ilishauri maneno yafuatayo yapewe tafsiri zaidi ili kuleta maana sahihi. Maneno hayo ni; *Nursing Home; Private Midwifery Services;Maternity Home;* na *Nursing Practice;*

Mheshimiwa Naibu Spika, Vilevile, Katika vifungu vifuatavyo Kamati inashauri kuongezwa kwa vifungu vipya ili kuboresha zaidi Muswada. Vifungu hivyo ni; Kifungu cha 6 cha Muswada, kiongezwe kifungu kipya cha 6(p) ambapo Baraza litakuwa na jukumu la kuendesha mitihani kwa Wauguzi kabla ya kusajiliwa; Kifungu cha 7(2) cha Muswada kinachozungumzia Kamati mbalimbali za Baraza, kiongezwe kifungu kipya cha 7(2)(e) cha Kamati itakayoitwa "*Registration and Enrolment Committee*"; Kwa kuwa kifungu cha 8(4) hakijabainisha masuala ambayo Baraza haliruhusiwi kuyakasimisha kama vile kubadili mitaala ya mafunzo na viwango vinavyohusiana na taaluma ya uuguzi na ukunga Tanzania. Kamati inapendekeza kuongezwa kifungu cha 8(4)(c) ambacho kitaainisha masuala ambayo Baraza halitakiwi kuyakasimisha. Ili kumtambulisha mtu mwenye usajili wa muda, Kamati inapendekeza kifungu cha 17 kiongezwe kifungu kipya cha 17(3) kitakachoonyesha uthibitisho wa usajili wa mpito;

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa kuwa kifungu cha 28 hakitoi ulazima wa kumtaarifu muhusika kuhusu uamuzi uliofikiwa na Baraza kuhusu kesi yake, Kamati inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 28(4) kitakachozingatia suala la muda wa kumtaarifu mhusika wa uamuzi wa Baraza *(notification of the decision)*; Ili kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato halali ya Baraza, Kamati inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 33(1)(e) kitakacholipa Baraza uwezo wa kuchangisha fedha *(fund raising*) badala ya kutegemea bajeti ya Serikali pekee; Kamati inashauri kuongezwe kifungu kipya cha 3(3) katika jedwali, kinachofafanua jinsi mjumbe wa Baraza atakavyopoteza sifa za kuwa mjumbe kwa sababu mbalimbali;

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutokana na mabadiliko yanayoweza kutokea mara kwa mara, Kamati inapendekeza katika kifungu cha 6(e) cha Muswada yasitajwe majina ya mamlaka husika; Katika kifungu cha 6 (m) na (n) viwango vilivyotakiwa kuzingatiwa na vituo vya kutolea huduma za uuguzi, na vyuo vya uuguzi, vilingane na kusiwe na tofauti kati ya vile vya binafsi na vya umma kwa lengo la kumlinda mteja; Kamati inashauri cha 17(1) cha Muswada kifanyiwe maboresho ili kukifanya kisomeke vizuri

pasipo kuleta tafsiri tata na kukifanya kiwe cha kueleweka zaidi kisheria; Kamati inapendekeza katika jedwali, kifungu cha 2(1), kuanishwe muda wa kikomo cha kuchaguliwa tena *(re-appointment)* wajumbe wa Baraza ili kila wakati kuleta mawazo mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Sehemu ya Nane ya Muswada imeainisha adhabu kwa makosa mbalimbali. Kamati inapendekeza adhabu hizo ziwekewe kikomo kama ifuatavyo:-

Kifungu cha 38(c) kisomeke, *not less than one million shillings and not more than three million shillings*. Kifungu cha 39(c) kisomeke, *not less than five hundred thousand shillings and not more than two million shillings.* Kifungu cha 40 isomeke, *not less than five hundred thousand shillings and not more than two million shillings.* Kifungu cha 41 kisomeke, *not less than three million shillings and not more than five million shillings*. Kifungu cha 42 kisomeke, *not less than five hundred thousand shillings and not more than two million shillings*. Kifungu cha 43 kisomeke, *not less than three hundred thousand shilling and not more than one million shilling.* Kifungu cha 44 kisomeke, *not less than one million shilling and not more than three million shillings;* na Kifungu cha 45 kisomeke, *not less than three hundred shillings and not more than one million shillings.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inawapongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii katika kwa kukubali kuleta jedwali la marekebisho wakati akiwasilisha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa (Mb), Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda (Mb) na Wataalamu wote wa Wizara hii kwa kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika; Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kwa kutoa maoni yao katika kuboresha Muswada huu. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati waliochambua Muswada kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mb. - Mjumbe, Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili, Mb. - Mjumbe, Mheshimiwa Prof. Feetham F. Banyikwa, Mb. - Mjumbe, Mheshimiwa Meryce Emmannuel, Mb. -Mjumbe, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mb. - Mjumbe, Mheshimiwa Hemed M. Hemed, Mb. - Mjumbe, Mheshimiwa Janeth B. Kahama, Mb. – Mjumbe, Mheshimiwa Dr. Christine G. Ishengoma, Mb.-Mjumbe, Mheshimiwa Susan A.J.Lymo, Mb-Mjumbe, Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman, Mb. - Mjumbe, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mb. - Mjumbe, Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, Mb. - Mjumbe, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mb. - Mjumbe, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mb. - Mjumbe, Mheshimiwa Ussi Amme Pandu, Mb. -Mjumbe, Mheshimiwa Luka Jelas Siyame, Mb. - Mjumbe, Mheshimiwa Fatma Abdulla Tamim, Mb. - Mjumbe,

Mheshimiwa Oscar R.Mukasa, Mb. - Mjumbe; na mimi mwenyewe Omar S. Kwaangw, Mb. - Mwenyekiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalize kwa kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashililah, pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake.

Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Kamati hii Ndugu Hosiana John na Ndugu Asia Minja, kwa kuratibu vikao vya Kamati hadi maoni haya kutoka katika muda muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba pia nitumie nafasi hii ndogo kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Babati Mjini, kwa kuendelea kunipa ushirikiano na imani yao kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naunga mkono Muswada na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. DR. ALI TARAB ALI - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote naomba kutoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kusimama hapa nikiwa mzima na kutoa maoni haya kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge Kanuni ya 53 (6) (c) toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa salamu zangu za mwaka mpya kwa Watanzania wote na hasa wapiga kura wa Jimbo la Konde kwa kuingia mwaka mpya wa 1431 Hijiria na mwaka 2010 wakiwa na afya njema kabisa. Aidha natoa pole kwa wale wote waliofikwa na majanga mbalimbali kwa kipindi kilichopita cha mwaka 2009 na mwanzoni mwa mwaka huu wa 2010, Mwenyezi Mungu awape moyo wa matumaini na ujasiri kuweza kukabiliana na mitihani hiyo. Maoni ya jumla kuhusiana na Muswada. Fani au taaluma ya Uuguzi na Ukunga ndiyo iliyotakiwa kuwa nguzo kuu ya kupigana na adui namba mbili wa nchi hii yaani maradhi kama ilivyoainishwa na kufafanuliwa katika maandiko mbalimbali ya historia ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kuwa katika historia ya nchi yetu ni taaluma ya Uuguzi pekee ambayo Serikali imekuwa ikipata maombi rasmi kutoka nchi za ulaya kuhitaji watumishi kwenda kufanya kazi kwenye nchi hizo, pamoja na hivyo hali halisi ni kwamba Serikali haijapata msukumo unaohitajika wa kuongeza motisha kwa wale wanaojiunga na taaluma hii ili kukidhi mahitaji ya ndani na kuendelea kupeleka watumishi wengine katika nchi zenye uhitaji wa watu wa fani hii kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kuwa Tanzania ina upungufu mkubwa wa Wauguzi na pia Tanzania ina Wauguzi wengi sana ambao wako nje ya Nchi na wanafanya kazi lakini nchi haina takwimu ya watalaam hao. Swali ambalo Kambi ya Upinzani inauliza. Je, Tanzania inafaidika vipi na Wauguzi hao wanaofanya kazi nje ya Tanzania wakati wamesomeshwa na kodi za Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali halisi ya tasnia ya afya au *Health Industry* inaendeshwa na fani ya Uuguzi na Ukunga lakini jambo ambalo hadi sasa Serikali bado haijaligundua au imeligundua lakini imeshindwa kulitekeleza ni mazingira ya kazi na maslahi duni kwa watalaam wa fani hii. Jambo hili limekuwa kikwazo kikubwa cha kuhakikisha adui namba mbili wa nchi hii, maradhi, toka enzi hizo kama alivyobainisha muasisi wa Taifa hili anashindwa kuondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu hauonyeshi kifungu chochote ambacho kinatoa motisha kwa wauuguzi na wakunga badala yake umesheheni vifungu vya kuwadhibiti wauguzi na wakunga katika utendaji kazi wao. Kambi ya Upinzani inaona kuwa pamoja na nia nzuri ya Serikali tunayo ambiwa lakini jambo hili litazidisha uhaba na upungufu wa wataalam katika fani hii, jambo ambalo ni hatari katika mustakabali mzima wa nchi yetu, kumbuka hata kama tutakuwa na madaktari wengi kiasi gani lakini bila ya wauguzi bado hatujafanya kitu. Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya Muswada. Baada ya kutoa maoni ya jumla kuhusiana na umuhimu wa wauguzi na wakunga, sasa tuangalie baadhi ya vifungu ambavyo tunaona viangaliwe vyema kwa maslahi ya nchi kwa upana wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 5(1) (a) kinachosema kuwa Waziri atamteua Mwenyekiti wa Baraza kutoka miongoni mwa wauguzi maveterani waliosajiliwa (*senior registered nurses).* Kambi ya Upinzani inaona ili kuleta kuaminiana miongoni mwa wajumbe wa Baraza itakuwa ni bora kama Mwenyekiti atachaguliwa na wajumbe wenyewe wa baraza badala ya kuteuliwa na Waziri. Aidha kifungu hicho kinasema kuwa Mwenyekiti mteule atakuwa miongoni mwa *senior registered nurses*. Kambi ya Upinzani inaona kuwa veterani aliyesajiliwa kisiwe kigezo cha kuwa Mwenyekiti bali pamoja na kigezo hicho kiwango cha weledi katika fani hiyo ni kigezo muhimu sana, kwani taaluma hiyo inabadilika kulingana na mazingira ya dunia yanavyobadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 6 kinachoainisha kazi za Baraza kuwa pamoja na kazi zingine, ni (a) kusajili na kuandikisha waombaji wa waliohitimu mitihani na kuidhinisha wale wote waliokidhi vigezo. Kambi ya Upinzani inaona kazi hii inastahili kufanywa na msajili na si Baraza. Tujaribu kuangalia katika sheria zingine ambazo kuna msajili na majukumu yake ya msingi ni yapi. Msajili ndiye mtendaji na msimamizi Mkuu wa yale yote yanayoamuliwa na Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 9(1) kinachohusu uteuzi wa msajili, kuwa atatoka miongoni mwa maveterani wa Wauguzi na Wakunga *(Senior Registered Nurse or Midwife)* waliosajiliwa. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, kwa kuwa kifungu hakikuwekewa sifa za kitaaluma hivyo itakuwa ni bora nafasi hiyo iombwe na kushindaniwa kwani tunaamini kabisa kuwa kuna wale watakaokuwa na sifa za ziada ambazo wengine watazikosa na hivyo kuondoa dhana ya kupendeleana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha 13 (1) kinachohusu mamlaka ya usimamizi *(Supervisory Authority).* Kambi ya Upinzani inaona ingelikuwa ni bora sheria

ikaweka vigezo (*criteria*) vya *Senior Registered Nurse or Midwife* kupewa mamlaka ya usimamizi *(Supervisory Authority).* Vinginevyo sheria hii inaweza kusababisha Bunge, chombo chenye heshima kwa jamii kuonekana kuwa sio makini kwani kuwa *Senior Registered Nurse or Midwife* sio kigezo cha mtu kuwa msimamizi wa Mkoa au Wilaya. Sambamba na hilo kifungu cha 13(2) (C ) Kinampa nguvu msimamizi huyo kutoa adhabu ya kumsimamisha Muuguzi au Mkunga yeyote aliyesajiliwa kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu. Kambi ya Upinzani inaelewa na ndivyo ukweli ulivyo kuwa kazi kubwa ya msimamizi ni kutoa taarifa kwa mamlaka anayoiwakilisha na sio kutoa adhabu. Hivyo basi, kifungu hiki kinaweza kutumiwa vibaya na wasimamizi hao kwa watumishi. Swali la kujiuliza. Je, pale ikibainika mtu hakutendewa haki na msimamizi huyo inakuwaje? Anaweza kudai fidia kwa tendo alilotendewa na msimamizi huyo?

Kambi ya Upinzani inashauri kuwa jukumu la kutoa adhabu libaki kuwa chini ya Baraza na pale tu mhusika atakapokuwa amekwishapatiwa nafasi ya kujieleza na si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 18(2) kinachohusu mtu aliyeondolewa au kufutiwa usajili, kuwa hatoweza kutumikia fani yake hiyo tena. Kambi ya Upinzani inaona hapa kuna tatizo kwani usajili huu ni sawa na fani zingine ambazo wanafani wanasajiliwa kama vile wafamasia, madaktari, walimu, wahandisi na kadhalika. Lakini mwanachama akishindwa kuhimili matakwa ya chama haina maana kuwa asitumike fani yake hiyo tena. Fani ya Uuguzi na Ukunga ina maadili na miiko yake na hivyo maadili hayo si lazima yawe ndiyo hayo ya Baraza. Tunamtaka Mheshimiwa Waziri kukiangalia vizuri kifungu hiki kitakuwa hakijatenda haki kwa wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 27 (2) kinachosema kuwa muuguzi au mkunga anayetuhumiwa kupewa nafasi na kuwakilishwa na wakili mbele ya baraza. Kambi ya Upinzani inaona kuwa maneno *may be represented by an advocate* yanaweza kuwasilishwa na wakili yafutwe kwani baraza sio mahakama na kazi ya baraza sio kutoa hukumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jedwali kifungu cha 2(1) kinasema kuwa nanukuu: *A member of the council shall hold office for such period of the appointing authority may specify in his appointment or if no period is so specified shall hold office for a term not exceeding three years from the date of his appointment and may be eligible for reappointment,* mwisho wa kunukuu.

Kambi ya Upinzani inaona kuwa mamlaka ya uteuzi kutamka muda wa mjumbe wa bodi kutumikia inaweza kuleta utata na kusababisha utendaji mbovu kwani mamlaka ya uteuzi ni binadamu na kwa hilo mapungufu ni kitu cha kawaida, na kuondokana na mambo kama hayo kutokea ndio maana tunatunga sheria zilizo wazi kuondoa uwezekano wa mtu kutumia mamlaka yake kwa upendeleo. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inashauri kufutwa kwa maneno *such period of the "Appointing Authority may specify in his appointment or if no period is so specified shall hold office."* Kifungu hicho kisomeke kama ifuatavyo: *A member of the council shall hold office for term not exceeding three years from the date of his appointment and may be eligible for reappointment.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nashukuru kwa maoni yote. Naomba twende kwenye kifungu cha kanuni zetu kifungu cha 84. Nimejifunza mambo mawili kutokana na uwasilishaji wa Mwenyekiti wa Kamati na Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Wametoa maelekezo ya *amendment* nyingi sana katika hotuba zao. Sasa sina uhakika yule wa Kamati walimshirikisha Waziri na yeye akafanya *amendments* zilizoletwa au sivyo.

Huyu wa Maoni ya Upinzani hayo maelekezo aliyosema ataleta nyaraka zingine za *amendment* au vipi kwa sababu kwa mujibu wa kanuni ya 84 inawata wale wa Kamati kama wana mabadiliko yoyote wamshauri Waziri akishamshauri Waziri anaweza kuyakubali kuyaweka kwenye amendment ama anaweza asiyakubali. Kama Kamati iko *serious* inaweza kuleta *amendment* yenyewe humu ndani. Hivyo hivyo kama maoni ya Kamati ya Upinzani kama wako *serious* na waliyosema hapa basi walete *amendment* tuzione kwa wakati. Sasa sijui haya mawili yamefanyika. Ama siyo basi tunaendelea kujadili na watu wengine.

Mpaka sasa hivi ninao wachangiaji ni saba wa kwanza kabisa ni Profesa Mtulia, atafuatiwa na Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa Job Ndugai.

**MHE. PROF. IDRISA A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu naomba niseme kwamba na mimi mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii nimeupitia Muswada huu lakini hata hivyo yako mambo mawili matatu naomba niyaeleze.

Naomba sana nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Afya na Naibu wake hususani kwa leo kutoa maelezo ya Muswada huu kwa umahiri mkubwa hongera sana Dk. Aisha Kigoda. Aidha ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Mwenyekiti wa Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Kwaag'w, kwa ripoti yake nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Wizara ya Afya hususani kwa Taasisi yake ya *ICUP* kwa kujenga *theatre* mpya katika hospitali ya mji wa utete na kituo cha UKIMWI vilevile wamejenga *theatre* pale Kibiti na kituo cha UKIMWI, tunawashukuru sana kwa ujenzi huo. Aidha Wizara ya Afya yenyewe napenda nitoe shukrani za wananchi kwa kituo cha afya cha Nyaminywili kimepatiwa *ambulance* mpya na hiki kituo hakikupendelewa tu kiko kilomita mia moja kutoka hospitali kubwa ya Utete. Watu wa Nanyimwili wanaishukuru sana Wizara ya Afya ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama afya inavita kubwa afya sasa hivi lazima ipigane na kupunguza vifo vya akina mama wajawazito mpaka sasa tunazungumzia akina mama 578 hufa kila Wazazi mia moja elfu na wao wamepania wanataka warudishe namba hiyo ifikapo 2017 wa mama wakijifungua wafe warudishwe kutoka 578 mpaka 175 hii ni hatua kubwa na inahitaji kazi kubwa. Vilevile imejipanga kupunguza vifo vya

watoto chini ya umri wa miaka mitano kutoka miaka kumi na mbili 2017 mpaka sitini na tano kufika 2017. Vilevile imejipanga kupunguza vifo vya watoto wachanga chini ya umri wa mwezi mmoja watoto wachanga kutoka 68 2007 mpaka wapungue wafike 35 kwa watoto 1000 watakaozaliwa katika hospitali hiyo.

Sasa utakuta huu mzigo hii kazi iliyoko mbele inategemea raslimali watu na Muswada huu umefika kwa wakati muafaka kwa sababu unagusa *point* kubwa kabisa katika huduma yote ya afya. Serikali tunafahamu imepanua training imepanua mafunzo madaktari matabibu wauguzi, wakunga maafisa afya, mafundi maabara, mafundi *X-rays* na wauguzi wa vijijini. Sasa kazi hii ni kubwa inahitaji watu waliojitolea inahitaji watu waliosomesha vizuri na inahitaji watu wanaothaminiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niwakumbushe ndugu zangu tu kazi wanazofanya hawa wauguzi mama akiwa mjamzito ni muuguzi au mkunga ndio wanaotabiri wanampina wanampa chanjo ya kwanza wanatabiri kama uzazi huu utakuwa salama au la anaweza kuzalia katika *dispensary* za kawaida au aende hospitali kubwa ni hawa na siku ya kuzaa hawa wapo pale. Mtoto akiumwa akishazaliwa na mtu mzima akiumwa wanaenda hospitali wanaonana na hawa manesi. Ukiwa unaenda kufanyiwa *operation* basi huna habari manesi ndio wako pale saa yote na ukitoka hapo unaenda *ICU* daktari anatoa maagizo lakini manesi wako *ICU*. Manesi wanakutazama muda wote mpaka karibu unakata roho manesi wako pale na kuna kitu kinaitwa *last respect* yaani kukuosha mara ya mwisho ili ufungwe katika ile nguo nyeupe ndugu zako wako kukuchukua ni manesi.

Kwa hiyo, kazi wanayofanya hawa ni kubwa ni kubwa mno Muswada huu ulihitaji uwe na *categorization* yaani mpangilio unaowaweka katika madaraja mbalimbali. Sasa hivi manesi wako wenye *Ph.D.*, wako manesi wana *degree* za kwanza na *Masters Degree*, wako manesi wa *Certificate* na *Diplomas* wako manesi *Assistant*, wako wale wa vijijini wale *First Aid Attendant*, hawa wote wanatakiwa wapangwe vizuri.

Vilevile namna yao ya kwenda katika kazi hizo ni *career parties* inataka ipangwe vizuri. Muswada huu kwa bahati mbaya haukujionyesha vizuri. Vilevile wanahitaji *continue education* iwe nje ya nchi au hapo hapo kazini kama ilivyo desturi tunajifuza lakini vilevile tunahitaji kuwe na mkazo maalum wa *continuing education*.

Mambo makubwa ya kufikiria ile kazi ngumu wanayofanya, *work load*. Kwa kweli manesi wanafanya kazi nzito na kwa muda mrefu nakumbuka nilivyokuwa nafanya kazi ya udaktari manesi wanafanya kazi mpaka wanasinzia. Unajua huyu ndiye anayeshika roho ya watu. Kwa hiyo ni muhimu sana kupanua na kuharakisha mafunzo yao. Upungufu wa manesi nchi nzima ni jambo linalofahamika kama tulivyoelezwa hapa kwamba Serikali ina watumishi inafanya kazi na watumishi asilimia 30 mpaka 38 kuna upungufu wa asilimia 62 au zaidi ya watumishi wanaohitajika. Kwa hiyo, hawa wachache kazi wanayofanya ni nzito sana. Ninakumbuka nilipokuwa daktari kijana, basi naona nisikumbuke ila niendelee tu kwamba kuna hoja kubwa sana kuweka *incentive levels* za hawa manesi kiwazi wazi mno. Kwa mfano mimi ningependa kama tunavyowapa maziwa manesi wanaoshughulika na wagonjwa wa *TB* wale wakunga kila mkunga

akizalisha mtoto angeratibiwa yule mtoto halafu baada ya pale mwezi akazalisha wangapi angepewa namna fulani ya *incentive* inaweza kuwa pesa kidogo au kitu chochote lakini ili kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa mpaka amezalisha basi ilikuwa inatosha kumfikiria *incentive*.

Sasa naomba nirudi katika Muswada wetu. Muswada huu katika *sections* Na. 6(a) unazungumzia juu ya mafunzo. Lakini nilitaka kukumbusha Serikali kwamba sasa hivi kuna vyuo vingi sana vya manesi vya wauguzi na wakunga vyuo hivi sina hakika kama vinaratibiwa vizuri na kama vinaratibiwa vinaweza vikawa vingapi, maana Dar es Salaam pale karibu sasa kila uchochoro ina chuo cha manesi. Lakini kubwa kuliko yote ni kwamba hawa wanaofundishwa hapa wanafundishwa wanapata tuzo yaani *certificate* zinazotambuliwa na mahospitali ya Serikali au ni watu binafsi kwa sababu mimi ninao ndugu wengi sana vijana wamekuja na vyeti hivi lakini vyeti hivi havina kibali cha Baraza la Wakunga linalowatambua kama ni kweli wamejifunza. Ili tusiwapotezee muda vijana hawa wale wanaoanzisha shule za manesi nilikuwa naomba sana Serikali ingehakikisha kama *training* hiyo imefikia kiwango kizuri basi na *certificate* zake ziwe *endorsed* na Baraza la Wauguzi ili vijana hawa wasipoteze muda bure katika shule hizi. Wakitoka pale waweze kupata ajira na waweze kuhudumia wananchi.

Pili naomba niisifu Serikali katika *section* Na. 7(c) kwamba kuweko kwa *ethical and disciplinary committee.* Hili ni jambo nzuri kuhimiza na kuhakikisha kwamba huduma hizi za Unesi, huduma za Ukunga na huduma za Uuguzi zinafanywa kwa uangalifu mkubwa na kufuata maadili yake. Ndugu zangu msisahau kabisa daktari huandika dawa halafu anaondoka, dawa zile ni sumu, zinataka mtu aliyesomeshwa vizuri na kufuata maadili ya utoaji ile dawa kwa wakati wake, akitoa zaidi hapo hapo inageuka dawa inakuwa sumu mtu anapoteza maisha.

Kwa hiyo, hiki kipengele cha *disciplinary* na *ethics* ni muhimu sana katika Muswada huu. Vilevile liko suala la *Nursing Administration* ambayo haikutokea vizuri katika Muswada kwamba *the Nursing*, manesi hawa ni Jeshi kubwa sana kamanda wao mkubwa the *Chief Nursing Officer* taifa lazima awe na manesi wanaomsikiliza na kuchukua maamuzi haraka katika ngazi za Mkoa na ngazi za Wilaya.

Kwa hiyo, utakuta sasa hivi kabla *Nursing Chief Nursing Officer* hajamgusa *Nursing Officer* wa Wilaya hapa katikati kuna ngazi ya TAMISEMI na utawala wote hauendi moja kwa moja kwanza kulikuwa na *nurse* huyu lazima awe chini ya TAMISEMI halafu tena awe chini ya afya halafu vilevile awe chini ya Baraza la wauguzi. Kwa hiyo, utaona kwamba pamoja na kwamba *section* inasema.........

**NAIBU SPIKA:** Ahsante naona ni kengele ya pili.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Ahsante naunga mkono hoja nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Kwa kweli tunafahamu wewe ulikuwa daktari na hayo maneno unayasema kwa uhakika kwa sababu umefanya nayo kazi. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu hoja ya kutunga sheria kwa ajili ya kuwatambua Wauguzi na wakunga. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Naibu Waziri, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii wanafanya kazi nzuri sana, kwa mazingira magumu. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kada hii ya Uuguzi na Ukunga ni muhimu sana hasa katika kipindi hiki ambapo sera yetu ya maendeleo ni kuhakikisha kwamba kila Kijiji wanajenga zahanati, kila Kata wanajenga kituo cha afya. Zahanati ni jengo ambalo linatakiwa liwe na watumishi, tuwe na *Clinical Officer*, Wauguzi pamoja na watumishi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuna tatizo kubwa sana la upungufu wa watumishi Wauguzi na Wakunga. Upungufu huu unasababishwa kwa sababu inawezekana aidha vyuo vya kufundisha hawa Wauguzi na Wakunga ni vichache na ndiyo maana tunakuwa na upungufu mkubwa sana wa watumishi hawa. Haina ubishi kwamba kada hii ni muhimu sana hapa nchini.

Kama alivyozungumza Mheshimiwa Profesa Mtulia pale kwamba manesi wanafanya kazi nzuri sana katika hospitali zetu kuanzia hospitali za rufaa, hospitali za mikoa, Wilaya, kwenye vituo vya afya pamoja na zahanati na wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Muswada huu utasaidia sana kuboresha hata utendaji tu wa hawa Wauguzi pamoja na Wakunga.

Sasa kuna suala hili kama alivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii kwamba kuhusu maslahi, uchache wa watumishi hawa, ni kweli kama nilivyosema wanafanyakazi katika mazingira magumu sana, kwanza hawa ndiyo wanawatunza wagonjwa katika wodi, usiku kucha, ndio wanaogawa dawa, ndio wanapiga sindano. Mganga kazi yake ni ku-*prescribe* dawa lakini anayegawa dawa ni Muuguzi, ukienda chumba cha sindano, chumba cha kufunga vidonda utakuta hawa ndiyo wanashughulika sana.

Kuna kazi nyingine ambayo wanashughulikia Wauguzi ni suala zima la *outbreak* ya magonjwa kama vile kipindupindu. Lazima hawa Wauguzi ndio wanakuwa mstari wa mbele. Zamani walikuwa wanalipwa posho ya mazingira magumu.

Lakini siku hizi hawalipwi na wengi wanadai mpaka ikiwepo hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa watumishi wengi wanadai walipwe madai yao, walikwenda kufanyakazi yao kazi kwenye milipuko ya magonjwa ya kuambukiza lakini mpaka sasa bado hawajalipwa madai yao wanayodai tena ya muda mrefu.

Kwa hiyo, mimi naishauri Serikali kwa kweli kada hii ni muhimu sana ni lazima tuongeze tuwe na wauguzi wa kutosha tuongeze vyuo vya kufundisha Wauguzi na Wakunga ili kila zahanati iwe na Muuguzi pamoja na vituo vya afya viwe na Wauguzi wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza litasaidia sana kwa sababu kama kulikuwa hakuna Baraza basi Baraza hili litawasaidia kwa sababu matatizo mbalimbali ya Wauguzi na Wakunga watapeleka malalamiko pale badala ya kushughulikiwa katika eneo moja tu, lakini Baraza hili linaweza likawasaidia sana kutatua matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kama nilivyosema kada hii ni muhimu sana kwa Serikali lazima ihakikishe kwamba wanaboresha maslahi yao na vile vile wanawapa vitendea kazi vya kutosha hasa wale ambao wako vijijini.

Sasa hivi katika zahanati zetu vijijini na mimi ninapenda niwapongeza sana hawa *Nursing Auxiliary* wanafanyakazi nzuri sana. Kuna mwaka fulani nadhani kwenye miaka ya 1995/1996 walifanyiwa *retrenchment Nursing Auxiliary* wengi sana. Lakini baadhi yao walibaki na wanafanyakazi nzuri. Kwa hiyo, ni kuwaendeleza ili wapate vyetu vya Uuguzi pamoja Ukunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ambalo nilitaka kuchangia kuhusu hii Uuguzi kama nilivyosema ni suala zima la kuwapatia vitendea kazi Wanafanyakazi katika mazingira magumu hasa katika hospitali zetu na vituo vya afya. Kwa hiyo, wapate vitendea kazi husika ili waweze kufanya kazi kwa .

Namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii wamechambua Muswada vizuri na maoni haya mimi naungana nao kabisa kwamba kama Serikali itatekeleza haya mimi nina hakika kabisa tunaweza tukaboresha hali ya utendaji ya wauguzi wetu hapa nchini.

Sasa kuna suala la maadili, Uuguzi na Ukunga ni taaluma. Kwa hiyo, lazima kuwe na maadili ambayo lazima yazingatiwe, *ethics*. Kwa upande wa afya kuna *Medical Ethics* ambazo lazima watumishi kuzifuata kwanza lazima wawe wapole kwa wagonjwa na lugha inayotumika kwa wagonjwa lazima iwe lugha ambayo inakubalika. *(Makofi)*

Wagonjwa wengi wanakata tamaa kwa sababu ya lugha, hivi karibuni tumesoma kwenye magazeti, siwezi kukumbuka ni eneo gani akina mama wajawazito wanakataa kwenda kujifungulia hospitali kwa sababu ya lugha za baadhi ya wauguzi wetu. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba, wauguzi wanafanya kazi nzuri sana nawapongeza, lakini wale wachache ambao wana lugha mbaya kwa kweli haipendezi, inawakatisha tamaa wagonjwa. Naomba wauguzi kama hao wachukuliwe hatua ili waweze kujirekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, uuguzi na ukunga *it is a professional* ambayo ni lazima maadili yawe ya hali ya juu sana, kwa sababu eneo wanaloshughulikia la kutibu

wagonjwa ni nyeti sana. Yangu machache yalikuwa ni kuungana na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwamba, Muswada ambao umeletwa ni mzuri na naomba tuupitishe ili uweze kufanya kazi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, sasa nitamwita Mheshimiwa Job Ndugai, kama nilivyosema Mheshimiwa Jenista Mhagama ajiandae, naona Mheshimiwa Anna Lupembe atafikiwa na Mheshimiwa Mohamed Mnyaa pia atafikiwa asubuhi hii.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Muswada ulio mbele yetu. Kwanza, nianze kwa kuunga mkono hoja lakini nitumie fursa hii vile vile kabla sijaingia kwenye Muswada, kutoa pole kwa wananchi wa vijiji mbalimbali vya Wilaya ya Kongwa, ambao walikumbwa na mafuriko kule Mtanana, Igwaga na sehemu nyingine na wiki iliyopita kuna kimbunga kimepita eneo la Mlali Bondeni ambapo familia sitini na nane nyumba zao zimeezuliwa na wako nje hadi hivi sasa. Nawapa pole sana, niwahakikishie kwamba, tuko pamoja katika matatizo haya na Serikali inawashughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya na Naibu wake, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo na Wakurugenzi na Watumishi wote hasa walioshiriki katika mchakato mzima wa kutuletea Sheria hii ya Manesi na Wakunga *(The Nursing and Midwifery Act).*

Umoja wa Mataifa umeweka malengo hasa kwa nchi zetu maskini kuhakikisha kwamba inapofika 2015 au karibu na hapo, kunakuwa na kupungua kukubwa sana kwa vifo vya akinamama wajawazito na vifo vya watoto na yako malengo ambayo yamewekwa pale kuhakikisha kwamba kupungua huku kunakuwa kukubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, matarajio makubwa na mategemeo yetu katika kupunguza vifo hivyo, tunawategemea sana manesi na wakunga kuwa sehemu kubwa sana ya watu watakaotusaidia kupunguza vifo vya akina mama, wajawazito na watoto. Manesi na wakunga ni muhimu sana katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni malengo ambayo tumejiwekea kidunia kwa hiyo lazima eneo hili tulitazame ipasavyo, ndio maana tunasema tunaipongeza Serikali kwa kutazama jambo hili na kutuleta sheria hii mpya. Nikikumbuka, Profesa alishindwa kukumbuka kwa sababu ya muda, nilipokuwa sekondari Kibaha enzi hizo Headmaster wetu akiitwa Michael Msaki, alikuwa akipenda kutuhutubia wanafunzi na moja ya hotuba zake alikuwa anapenda kuirudiarudia alikuwa anasema, vijana wangu kazi tatu hapa duniani ni nzuri sana, ukifanya moja ya kazi hizo unakwenda mbinguni moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kwanza ukiwa mwalimu wa dini kwa nafasi yoyote ile; kazi ya pili ukiwa mwalimu wa shule; na kazi ya tatu ukiwa nesi, mkunga au mganga. Akasema kwamba, ukifanya moja ya kazi hizo kwa kweli unakuwa umewatumikia wanadamu katika nafasi ya kipekee. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu ataangalia makosa yako na kukupunguzia mzigo wako kwa sababu umefanya moja ya

kazi takatifu. Kwa hiyo, tunaongea habari ya manesi na wakunga, watu ambao wanafanya kazi muhimu sana katika jamii yetu, nafasi ya kipekee kabisa. Sasa sheria inakuja mbele yetu kwa dhumuni la kuinua taaluma hii ya unesi na ukunga, lakini vile vile kudhibiti huduma hii ya unesi na ukunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzisha Baraza la Wauguzi na Wakunga ndani ya Baraza atakuwepo Msajili atakayeshughulikia mambo yaliyowekwa ndani ya sheria na kuweka utaratibu wa usajili mzima; nani anasajiliwa; kwa utaratibu gani; atakayekwenda kinyume atafutwa vipi na utaratibu mzima wa kushughulikia malalamiko endapo yapo kuhusiana na manesi na wakunga.

Kabla sijakwenda mbali niende kwenye sheria yenyewe, nikianza na ukurasa wa kumi na moja pale, fungu la saba, Kamati wamezungumzia na mimi nimeliona hili ni muhimu; nimeona nilirudie kwa msisitizo kwamba katika Kamati zinazoundwa pale chini ya (7)(2) basi iwepo Kamati inayohusika na *registration* na *Enrollment Committee*. Naona ni muhimu sana kuwa moja ya Kamati zile nne zilizoko hii iwe ya tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa kumi na nne, fungu la kumi na tatu, nimemsikia Msemaji wa Kambi ya Upinzani akipitia kwa mbali, ningependa kusisitiza na kwamba, hapa Baraza linapewa mamlaka ya ku-*appoint a senior registered nurse* au *midwife* awe ndiyo *supervisory authority* kwenye Wilaya, kwenye Mkoa na kwenye *Insitutions* mbalimbali. Anapewa nguvu huyo mtu mmoja ku-*investigate any charges, complaints* na kadhalika, anapewa nguvu za ku-*suspend temporarily nurse* yeyote au muuguzi yeyote kwa miezi mitatu; huyu mtu anapewa nguvu hizi hana kikao, hana nini yeye tu peke yake anapewa nguvu kubwa namna hii!

Mhehsimiwa Naibu Spika, nilidhani jambo hili lingeangaliwa vizuri, madaraka yakiwa makubwa sana hata kama yametolewa kwa nia njema, mwisho wa siku inakuwa tabu. Awekewe kikao fulani katika ngazi yake kuweza kujadili angalau na watu watatu, wanne ili kuweza kum-*suspend* mtu. Haya ni madaraka ambayo yamezidi kiasi kabisa, kwa hiyo litazamwe hilo. Matarajio yangu Mheshimiwa Waziri jioni atakuwa amerekebisha hapo, vinginevyo itabidi nisimame tena hapa ili nipate ufafanuzi zaidi kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa kumi na sita, ambapo tuna ile 15(e)(ii) anasema; *has successfully completed a course of training as a nurse of not less than three years* na *midwife for a duration of not less than one year*. Sina matatizo, lakini ukurasa huo huo pale chini 3(a); *A person shall be entitled to be enrolled as a midwife if he has successfully completed a course of nursing for a duration of not less than two years*. Sasa inajichanganya yenyewe, pale juu miaka mitatu, hapa chini miaka miwili! Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba, 3(a) ipandishwe iwe *not less than three years* ili pawe na mtiririko unaokwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa ishirini na mbili, lile fungu la 27 na mimi naunga mkono hoja ya kwamba, habari ya mtu mwenye matatizo aliyeitwa katika Baraza kwamba anaweza akawakilishwa na Wakili nadhani hii si mahali pake, tuache Baraza

lifanye kazi yake, kama mtu hakuridhika aende mahakamani, apeleke mawakili na mambo yanoyofanana na hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko makubwa ambayo yamekuwa yakitolewa na wananchi na kuletwa kwetu sisi Wabunge kama Wawakilishi wao kuhusiana na kada hii ya unesi na ukunga ni masuala ya *ethics*; kuporomoka sana kwa maadili ambako kunatokana na kashfa kwa wagonjwa kutowahudumia ipasavyo, malalamiko yanayohusiana na kutelekeza wagonjwa na malalamiko yanayohusiana na kutoa siri za wagonjwa. Bahati nzuri Baraza hili limepewa mamlaka ya kushughulikia malalamiko haya na sisi tunasisitiza kabisa kwamba, jambo hili liangaliwe sana, lipewe msisitizo wa kipekee, lisimamiwe ipasavyo ili kada hii iweze kujisafisha na malalamiko makubwa sana ambayo yanatokea kwenye kada hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nijiulize na nimuulize Mheshimiwa Waziri; hivi wakunga wa jadi wao wanaingia wapi maana hapa hawakutajwa popote kabisa; je, hatuwezi kuwaorodhesha tukawatambua kwamba sehemu fulani kuna mkunga wa jadi au *practice* yao tunaitazamaje? Nafasi yake iko wapi?

Kama walivyosema wenzangu kazi hii ni ngumu na mimi narudia ni ngumu sana, ni kazi ya kujitoa, wanafanya kazi katika mazingira magumu; kusafisha wodi, kuogesha baadhi ya wagonjwa waliozidiwa sana, kuwapa dawa, kuhangaika nao kwa namna ambayo inatia huruma. Tunaiomba sana Serikali katika uchache wa watu hawa waangaliwe mapato yao, mishahara yao itazamwe vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo ambalo linaenda na haya ambalo nimekuwa nalalamikiwa na wananchi; mama akishahudumiwa na wakunga hawa amejifungua salama, kuna chandarua anapewa, ni vizuri nipenyeze hapa hapa kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya, chandarua kile anachopewa mama aliyejifungua ni kidogo sana, kinamtosha mama na mtoto. Sasa wapiga kura wangu huwa wananiuliza Mheshimiwa sasa baba hapa nafasi yake iko wapi kwenye chandarua kile? Kwa hiyo, wamenituma nifikishe ujumbe huu kwamba kiangaliwe kiwe kikubwa kidogo, angalau na baba naye atoshe pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nizungumzie habari ya Manesi wa Kitanzania ambao wanafanya kazi nje ya nchi yetu. Niliwahi kusimama Bunge lililopita nikazungumzia habari ya manesi wetu waliokuwa wakifanya kazi Bostwana, walikuwa wakinyanyasika, wakidhalilika kwamba wao si mahiri ni manesi wasiokuwa na ujuzi unaostahili kulinganisha na Wakenya na Waganda wanaofanya kazi kule Bostwana. Kwa hiyo, ikawa inatoa picha kama vile Manesi wa Tanzania ni *inferior*. Matumaini yangu ni kwamba, sasa *registration* itakayofanyika hapa, itakuwa ya uhakika, itawafanya manesi wetu waweze kufanya kazi hapa nchini kwa kutambulika na katika Commonwealth, ikiwa ni pamoja na nchi nyingine hizo ili picha ya kwamba Manesi wa Kitanzania wako chini ya kiwango isijitokeze mahali popote pale. Jambo hili litawatia moyo sana manesi wetu ambao wanafanya kazi nje ya nchi yetu kwa sababu mwisho wa siku wanaleta chochote kile katika nchi yetu kusaidia katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ni matumaini yangu kwamba, Baraza hili jipya litakuwa jipya kweli, wasije wakachukua maofisa wale wale wakahamisha wote katika Baraza jipya, tutahamisha ugonjwa ule ule katika sheria mpya lakini mabadiliko hayatakuwepo. Yawepo mabadiliko ya uhakika ili tuwe na chombo ambacho kitasaidia kusukuma mbele mambo yanayohusu manesi na wakunga katika nchi yetu. Naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumzia hoja iliyoko mbele yetu. Nianze kwa kuwapongeza manesi na wakunga wote wa Tanzania. Mimi kama mama, sina budi kulisema hilo, ninatambua mchango mkubwa sana wa kada hii ya unesi na ukunga hasa katika suala zima la kutetea haki ya kuishi kwa mwanadamu akiwemo Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama manesi na wakunga, wangefanya njama yoyote ile nadhani hata sisi Wabunge tusingeweza kupata haki yetu ya kuishi hasa katika tendo la kuzaliwa ambalo wao wamekuwa ni wasimamizi wakubwa. Kwa hali hiyo, naomba niwapongeze sana na niwashukuru kwa sababu wanatekeleza wajibu wa Kikatiba wa nchi yetu wa kutoa haki kwa Wananchi wa Tanzania na tukianza na haki ya msingi ya kuishi. Muswada huu umefika katika wakati muafaka, ni wakati ambao tunahitaji kabisa kada hii iweze kusimamiwa kwa kufuata taratibu na kanuni zitakazotuwezesha kuhakikisha kwamba yale ambayo yamekuwa ni matarajio kwanza kwa kada yenyewe ya manesi na wakunga, lakini vile vile kwa matarajio ya kujenga maendeleo ya nchi yetu kupitia Sekta ya Afya yanaweza kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unajibu maswali mengi sana kama walivyosema wenzangu, lakini na mimi nitarudia; ukiangalia kwa sasa nchi yetu inakaribia kuwa na takriban idadi ya watu wasiopungua milioni arobaini kwa mwaka huu, sasa ni idadi kubwa sana hiyo na idadi hiyo inaonesha hawa watu wote watahitaji matibabu, lakini ili kufikia *population* ya watu hao ni kwamba, hawa watu wanaendelea kuzaliwa siku hadi siku. kwa hiyo, kada hii ina maana kwamba ni kada muhimu sana ya kuzingatiwa na inajitokeza kabisa. Yako Makubaliano ya Accra yanayodai tuone namna gani tunaongeza bajeti kwenye Sekta ya Afya ambayo hawa manesi na wakunga wamo ndani yake. Nchi yetu haijatekeleza lakini kwa Muswada huu nadhani tutafikia huko. Zipo Itifaki za SADC zinazungumzia sana haya yote.

Mheshimiwa Profesa Mwakyusa amezungumzia sana suala la malengo ya kimilenia, kuhakikisha tunaokoa vifo vya akinamama na watoto na tumeona kabisa kwamba, vifo vya akinamama na watoto lazima vipungue kutoka mia tano kwa elfu moja angalau tufike kwenye mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwamba, hili suala watu wengi wanaweza kuwa hawalioni, lakini kama ingekuwa kwa siku moja gari lenye abiria mia tano linapinduka na watu wote wanakufa, nadhani hiyo ingekuwa sasa ni kelele ya kutosha ya kuonesha ukubwa wa tatizo uko kwa kiasi gani. Kwa hiyo, nasema kwamba, Muswada huu hakika unajibu mambo mengi sana; tuna malengo yetu sisi ya ndani ya nchi, tuna MKUKUTA, tuna mambo kadha wa kadha, lakini ukiangalia wachangiaji wakubwa wa

kufikia haya yote ni Sekta hii ya Wauguzi ambayo ni muhimu sana katika afya ya Watanzania kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakubaliana na maeneo mengi ya Muswada, sioni kama yana matatizo, nadhani matatizo makubwa yatakuwa katika suala zima la utekelezaji. Mara nyingi tunaweza kuwa na sheria nzuri lakini isiposimamiwa vizuri ndio inaweza ikaleta matatizo. Labda niseme katika kifungu cha (5)(1)(f) ni uundwaji wa Baraza la Wauguzi na Wakunga, lakini tumeona kwamba kifungu cha (f) kinashauri Wawakilishi wa Baraza hilo watoke katika ngazi ya Mkoa ama ngazi ya Wilaya; mimi nauliza kwa nini kwa sababu lile Baraza tumeambiwa litakuwa na watu wasiopungua kumi na tano?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nadhani pale tusiseme ama wauguzi na wakunga, wengi wako katika ngazi ya Mkoa na wengi wako katika ngazi ya Wilaya na kule ndio tunakoona kuna mahitaji mazito ya wauguzi hawa kupatiwa haki zao, lakini na wao kutekeleza wajibu wao wa kimsingi katika maeneo yao ya kazi. Kwa nini hapa tusiseme *Regional Nursing Officers and District Nursing Officers na siyo All District Officers* kuhusu ile *component* iwe vizuri tuwe na Uwakilishi wa Mkoa na tuwe na Uwakilishi wa Wilaya, kuliko kusema *all* kwamba, lile Baraza litakapokuwa linaundwa, mtu anaweza akajisikia akawaweka wawakilishi kutoka kwenye ngazi ya Mkoa tu na wale wa Wilayani wasiwe na uwakilishi wao.

Naomba hilo neno dogo libadilishwe, badala ya *all* tuweke *and* kusudi tuweze kuhakikisha tuna uwakilishi wa Mkoa na Wilaya kwa maana yangu halisi kwamba, wauguzi hawa wengi wako katika ngazi ya Mkoa na wengi wako katika ngazi ya Wilaya ambao wanashuka mpaka kwenye vijiji, kwenye Kata na kule mnaona tuna zahanati, tuna kila kitu na ndiyo kwenye matatizo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 5(3) inaonesha masharti ya mtu atakayekuwa *appointed* kuingia kama Mjumbe wa Baraza na ile sehemu ya tatu inasema kwamba, *no person shall be appointed a member of the Council who is declared bankrupt.* Nafikiri hapa labda tungepewa maelezo vizuri zaidi; kwa nini kigezo hicho kiwekwe kama ni kigezo kimojawapo?

Sehemu ya 11(1) ni *appointment* na *duties* za *supervisory authority*. Mimi nakubali kwamba, mwenzangu wa Upinzani amelizungumza vizuri, yeye amemzungumzia *supervisor* mwenyewe na majukumu yake na jinsi ambavyo itaonekana amepewa nguvu za ziada kama atakuwa pale ndiyo muamuzi wa kesi bila kusaidiwa na chombo kingine chochote; na Mheshimiwa Job Ndugai namshukuru ameeleza kwa kirefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kwamba hii *authority* ipelekwe chini kwenye *level* ya Mkoa na kwenye *level* ya Wilaya. Nadhani ni kitu cha msingi sana, tumepata uzoefu mamlaka nyingi zinazoundwa zinaishia kwenye ngazi ya Taifa, lakini utekelezaji unakuwa kwenye ngazi ya Mkoa na ngazi ya Wilaya na hivyo tumeona

kwamba zinapoishia kwenye ngazi ya Taifa, utekelezaji ule makini kwenye ngazi ya Mkoa na ngazi ya Wilaya unalegalega. Ninachoshauri, nakubaliana na wenzangu, tuone mamlaka haya tunayompa huyu *superviser* ni kweli yanaweza kuendana na hali halisi ya wauguzi na wakunga wetu kule waliko. Tumeona hapa watumishi wengi wako kule chini; hivi ni kweli mtu huyu anaweza kuwa na busara ya kutosha ya kufanya maamuzi sahihi kwa wakati sahihi yenye kutoa haki kwa watu ambao ni sekta muhimu sana kwenye jamii yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani hilo ni la kuangalia, labda kama ni la kikanuni, nadhani sheria ingekuwa na nafasi kubwa zaidi kuliko kanuni ingawa najua uadilifu wa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri katika kusimamia masuala ya Wizara hii. Hatuna mashaka nao; ni watu waadilifu, wachapa kazi, wanaoweza kuelewa na wana upeo mkubwa sana wa kuelewa mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiofichika hali halisi ya hawa wauguzi na wakunga katika nchi yetu wanakabiliwa na matatizo makubwa yafutayo:-

Sisi wote Waheshimiwa Wabunge hata mimi kwenye Jimbo langu la Peramiho nimekuwa nikizunguka kwenye maeneo yangu ya kazi na ninakutana nao hawa watu, unaona jinsi walivyo, wanakabiliwa na matatizo makubwa. Naomba niyaseme machache: Kwanza kabisa, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ametuambia kada hii ya manesi na wakunga, watu hawa ni wachache sana katika nchi yetu ya Tanzania, hawatoshi kabisa na kwa kuwa ni wachache basi mzigo wao wa utendaji wa kazi ni mkubwa kuliko hata umri walionao. Kazi inayofanywa na mkunga mmoja inaweza kuwa ilitakiwa ifanywe na wakunga watano, sita, kwa hiyo, unaona kwamba ni wachache na wana mzigo mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sikatai ni kweli wako baadhi yao wana tabia ya kuchukulia kigezo cha uchache wao kuidhalilisha kada hiyo ya unesi na ukunga kwa kuwadhalilisha wanawake hasa wakati wa kujifungua na wakati wa matatizo mengine. Nadhani sasa ni wakati muafaka kwa sheria hii tuone ili kuondoa tatizo hili la mzigo wao mkubwa wa utendaji, basi suala la kuongeza manesi kwa kadiri tunavyoweza na sera yetu sasa hivi tunasema tunaongeza zahanati, lakini watu hawa wasipoongezeka basi hatutaweza kuwaondoa katika suala la utendaji kazi ulio bora kwa sababu ya uchache wao.

Wanafanya kazi katika mazingira duni, wala siyo siri; vitendea kazi ni vichache na sasa hivi kuna magonjwa mengi ya milipuko, kuna magonjwa mengi ya kuambukiza. Kwa kupitia sheria hii, nadhani ipo haja ya kutekeleza Agizo la Accra la kuongeza bajeti kwenye Sekta ya Afya ili watu hawa wapatiwe vitendea kazi katika ngazi yao ya utumishi lakini katika ngazi ya zahanati zetu na hospitali zetu vitendea kazi vipatikane vya kutosha, lakini kwa kuongeza bajeti ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watumishi wa kada ya uuguzi na ukunga wanapofanya kazi maeneo mengine, tushukuru tu kwamba wanakubali kujitolea kufika mpaka huko kama walivyo walimu. Mimi nadhani sasa ifikie wakati hawa nao

waangaliwe wapewe posho za mazingira magumu ambazo zitawasaidia manesi wetu na wakunga wakubali kufanya kazi mahali popote katika Nchi ya Tanzania. Hawa watu wakati mwingine wanafanya *overtime*, unaweza kukuta wakati mwingine baadhi ya manesi ni wagonjwa anabaki mmoja au wawili wanafanya kazi mpaka muda wa kazi unapita wao wapo kazini tu. Hebu niambie kama mkunga ana wanawake sita wanasubiri kujifungua atafunga Kituo cha Afya; atafunga zahanati kwamba muda wake wa kazi umekwisha na hana mtu mwingine wa kumsaidia? Inampasa afanye kazi wakati mwingine mpaka usiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru sana Serikali yetu sasa hivi imeanza mkakati wa kuweka angalau hata *solar power* kwenye zahanati zetu. Anafanya kazi na kibatari ili kuwasaidia wanawake wajifungue, kuwachoma sindano watoto na wagonjwa. Hebu niambie kitanda cha kuzalishia yule mama, hali ya hicho kitanda ni ngumu; tunapimaje ubora wa kazi wa mkunga huyo katika mazingira ninayoyasema?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu nchi yetu inafanya mambo mazuri sana, ninaomba Bajeti ya Afya iongezwe ili iweze kuendana na suala zima la sheria tunayoipitisha leo ili iweze kuwasaidia manesi wanapotoa huduma. Kwanza, wao wenyewe wawe katika mazingira ambayo yatawaondoa katika hatari, lakini vile vile waweze kuwahudumia Wananchi wa Tanzania kwa kiwango cha kada yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho katika Sekta hii ya Afya; tumeona kabisa kwamba manesi na wauguzi wana soko kubwa hata nje ya nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Haya taarifa imefika, ina soko kubwa hapa nchini na nje. Sasa namwita Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Mnyaa ajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa mchana huu. Naomba nimpongeze Waziri pamoja na Naibu Waziri, kwa kutuletea Muswada mzuri ambao utawaletea mafanikio makubwa sana wauguzi wetu pamoja na manesi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kuwa, wauguzi na wakunga katika nchi yetu ya Tanzania ni wachache sana kama wenzangu walivyosema na vile vile wanaishi katika mazingira magumu na wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Unaweza kukuta zahanati au hata hospitali tu ya kawaida, muuguzi akifika wagonjwa wanamsubiri na usafi unamsubiri na mara nyingi tunakwenda katika zahanati zetu na hospitali zetu tukilalamika kuwa ni safi au chafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unakuta muuguzi yuko mmoja katika zahanati na zahanati nyingi za vijijini utakuta muuguzi mmoja tu, huyo huyo apokee wagonjwa na huyo huyo saa nyingine anakuwa daktari. Muuguzi huyo huyo anasubiri mama mjamzito amekuja ajifungue na vile vile kuna mgojwa amekuja ana malaria yuko *serious* au mtoto amekuja yuko *serious*, *dispensary* chafu; ndiyo maana tunasema ukiwa *nurse* au muuguzi

ama mkunga unatakiwa upate rehema ya Mwenyezi Mungu maana bila huruma ambayo Mwenyezi Mungu amekupa, ndiyo unakuta wachache wanafanya kazi wanachoka, matokeo yake akija mgonjwa mwingine anamjibu pasipo kutegemea kwa kuwa amechoka maana atatoka kuzalisha, atatoka kumhudumia yule mtoto ambaye amekuja *serious* pale amuwekee *drip,* akitoka pale anakwenda kufanya usafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizingatia mazingira yetu vijijini mengine ni magumu, mgonjwa mwingine anakuja yule muuguzi hawezi kutibu, anatakiwa ampe vifaa aende labda kwenye Kituo cha Afya au Hospitali ya Wilaya na kawaida mara nyingi mgonjwa akiwa *serious* sana, muuguzi anatakiwa amsindikize mpaka kwenye Kituo cha Afya au kwenye Hospitali ya Wilaya. Kutokana na mazingira yetu magumu, wauguzi wetu ni wachache, unakuta anaambiwa labda mzazi naomba niku-*refer* Kituo cha Afya au Hospitali ya Wilaya.

Yule mama anakuwa hana kipato cha aina yoyote ni mama wa kijijini, kutokana na hali ngumu hakuna gari la Kituo au tuseme zahanati mara nyingi hazina magari ya afya, ataondoka na yule mtoto atampakiza kwenye baiskeli, akifika njiani yule mtoto hatimaye anafariki. Hayo ni matatizo magumu ambayo yanapatikana huko vijijini kutokana na hali halisi ya wauguzi wetu na wakunga wetu wakiwa wachache ndani ya Nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, nasemea Hospitali yetu ya Mpanda; Hospitali ya Wilaya ya Mpanda wauguzi wako wachache mno. Sasa hivi anaingia muuguzi kuanzia asubuhi anafanya kazi mpaka saa 12 jioni, anatoka kidogo anakwenda nyumbani kuoga anarudi tena anakaa *night* mpaka asubuhi. Mazingira hayo ni magumu mno kiasi ambacho wauguzi katika Hospitali ya Mpanda wanalalamika, hawana posho wala *over time* lakini kutokana na hali halisi ilivyo, wauguzi wachache, inabidi wafanye hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetuletea suala la Mabaraza. Baraza litakaa Taifani na matatizo mengi kama hayo niliyoyasema yako Mawilayani na Mikoani. Ninaomba niungane na mwenzangu aliyepita Mheshimiwa Jenista Mhagama, tunaomba haya Mabaraza yaje mawilayani na mikoani ili yaweze kuwasaidia kwa ukaribu zaidi hawa wauguzi pamoja na wakunga. Kama nilivyosema, huko vijijini kwenye Kata zetu kuna muuguzi unamkuta mmoja huyo huyo ndiyo mganga, ndiyo *nurse* na huyo huyo ndiye mfagiaji wa hiyo zahanati. Kwa hiyo, akiwa na shida au matatizo akitoka kule kwenye Kata akija mpaka Wilayani ina maana ile zahanati inafungwa na nyingi mara nyingi ndivyo zilivyo. Unakuta zahanati nyingi wanaitwa kwenye semina mawilayani, zahanati inafungwa anakuja wilayani anafanya semina siku mbili kutokana na hali ya usafiri mpaka akae kule siku tano, kule wananchi wanapata tabu, matatizo yanakuwa makubwa na wengi wanakufa kutokana na matatizo hayo. Tunaomba haya Mabaraza yashuke ndani ya mawilaya na mikoa ili yaweze kutusaidia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri zamani Mpanda tulikuwa na Chuo cha Wauguzi lakini sasa kilifungwa. Hivi vyuo vilikuwa vinasaidia sana, tunaiomba Serikali ivirudishe viweze kuibua wauguzi na wakunga wawe wengi katika hospitali na zahanati

zetu. Hivi sasa tunategemea kujenga zahanati nyingi, tunatoa hamasa kwa wananchi wajenge zahanati na vituo vya afya kwenye Kata na Vijiji vyao lakini Watendaji hatuna. Tunaomba Serikali ijipange vizuri, katika bajeti ya 2010/2011 vile vyuo ambavyo waliviwekea mpango vifunguliwe kama Chuo chetu cha Mpanda walisema watakifungua tangu 2008 mpaka sasa 2010 kipo tu hakijafanyika kitu chochote. Tunaomba Serikali ijipange waweze kufungua vyuo hivyo ili tuweze kupata manufaa na wananchi vile vile waweze kupata matibabu kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wauguzi wetu mishahara yao ni midogo sana na wanafanya kazi kama nilivyosema kwenye mazingira magumu. Tunaomba Serikali iwaone kwa jicho la huruma, hizi posho na malimbikizo yao, unakuta saa nyingine hawaendi likizo kutokana na kazi nyingi zilizokuwa mbele yao. Malimbikizo yao ya likizo wapewe, hawa ni watu wa kuwaona kwa uso wa huruma sana kwa kuwa wanafanya kazi ngumu ya kuokoa maisha ya mwanadamu. Tunaomba mishahara yao na malimbikizo yao wapewe kwa muda muafaka na mshahara uongezwe kwa wauguzi na wakunga kwa kuwa wanafanya vitu ambavyo vinaokoa maisha yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaomba niseme nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango wako. Sasa nimwite Mheshimiwa Mohamed Mnyaa na kama muda utapatikana Mheshimiwa Pindi Chana atapewa nafasi.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika na mimi kunipatia nafasi angalau niseme machache katika hoja iliyopo mbele yetu ya Muswada wa *The Nursing and Midwifery.*

Kwanza, nichukue nafasi hii nimpongeze Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dkt. Tarab Ali Tarab, kwa namna alivyouchambua Muswada huu. Vifungu vyote ambavyo kwa taaluma kwa vile na yeye ni Daktari, akaviona vina matatizo na bahati nzuri vifungu hivi pia vimeonekana na wachangiaji wengine kama Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Ndugai. Kwa hiyo, naamini Mheshimiwa Waziri utaviangalia kwa makini ili vifungu hivyo vifanyiwe marekebisho. Kwa ujumla katika Muswada huu vifungu ambavyo vinapaswa kuangaliwa vizuri ni cha sita, tisa, kumi na tatu, kumi na nane na ishirini na saba. Nafikiri Mheshimiwa Waziri na najua kwa uadilifu wako na usikivu wako, utaviangalia vizuri kwa manufaa ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ningependa nilizungumzie hapa ni mfumo au utaratibu wa Muswada huu na inawezekana si kosa la Muswada huu tu au si tatizo la Muswada huu, lakini Miswada yetu mingi ambayo mara nyingi sana tumeletewa hapa katika Bunge lako Tukufu; ukitazama utaratibu wa Muswada baada ya maelezo haya yote ya Bodi na nini basi zaidi ni kupanga namna ya adhabu na utaratibu wa usimamizi na mambo kama hayo. Waheshimiwa Wabunge waliochangia Muswada huu wote wamebainisha na kuthibitisha kwamba hawa wauguzi na wakunga kazi yao ni ngumu tena ngumu sana.

Muswada huu haujaangalia maumbile ya kazi zao za hatari na namna gani angalau ukapanga *privilege* za watu hawa au utaratibu na motisha ili kwa kuwathamini angalau kuwapa moyo, badala yake unapanga adhabu tu; akifanya hivi adhabu hivi, Baraza liwe hivi na msimamizi awe hivi. Sasa kidogo hii inatia wasiwasi na si taratibu nzuri, kama ni mfumo wa Miswada ya kizamani, ya kikoloni, sasa bwana tuko mbali sana, nafikiri tufike mahali na sisi tuwape moyo hawa watu.

**NAIBU SPIKA:** Kusudi letu mambo ya ushirikishaji wa jamii. *(Kicheko)*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Naam!

**NAIBU SPIKA:** Maana umesema Miswada mibaya siyo ya ushirikishwaji wa jamii na wauguzi.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Hapana ni kwamba, tufike mahali tuwe na mfumo ambao hawa watu nao wanajisikia, wanasema kuna Muswada leo wa *The Nursing and Midwifery* anajisikia yule anayesikiliza kule kwamba Muswada umemgusa katika kumpa sifa fulani au kumpa *privilege* fulani. Siyo Muswada unaomgusa kwa kumuwekea vikwazo tu, ukifanya hivi utafanywa hivi ni adhabu tu, hii kidogo haileti picha nzuri.

Hawa watu hawapati hata *risk allowance* au *hardship allowance.* Hivi ni vitu ambavyo wao wenyewe wangetamani wavisikie vinazungumzwa kwa manufaa yao na kwa manufaa ya Taifa kwa sababu sote tunakiri kazi zao ni kubwa na hata sisi tumefikishwa hapa tulipofika kwa msaada wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Mtulia alizungumzia kwamba, kuna *grade* tofauti kuanzia hawa wakunga wa vijijini mpaka *nursing* wenye *Bachelor of Science in Nursing,* wenye *Masters;* hakujazungumziwa hizi *grades* na kwa ugumu wa kazi zao hawa huwezi ukasema wakati mwingine huyu mkunga wa vijijini labda yeye ana kazi nyepesi kuliko mwingine.

Kwa mfano, Mheshimiwa Naibu Spika, nikupe mfano mmoja huko vijijini, hawa wakunga wa vijijini ni wakunga ambao saa nane usiku wanagongewa milango waende wakamhudumie mgonjwa labda kuna mzazi na masafa ni marefu labda sana sana wanasindikizwa na ndugu wawili au watatu wa wale wagonjwa. Muswada haujazungumzia lolote na hawa wameolewa wanaondoka wanawaacha waume zao peke yao. Haujazungumzia hata *incentive* gani wazipate hawa wanaoamshwa saa nane za usiku na siyo siku moja wala mbili au hata waume zao nao wapate *benefits* za namna gani. Haya ndiyo mambo ambayo yangefaa yafikiriwe pia; wanapata tabu sana hawa na wanaume kwa sababu wakati mwingine tunakuwa peke yetu muda mrefu vitandani wakati wao wanahudumia wagonjwa huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu; kuna tatizo kwa hawa ndugu zetu wenye *Bachelor of Science in Nursing* inaonekana hawalipwi mafao yao kwa mujibu wa taaluma zao. Kuna malalamiko makubwa mno, yaani *level* yao ya mishahara na taaluma

hawafikiwi na imeleta kitu kama dharau na sasa hivi idadi ya wanafunzi pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam imepungua sana na inapungua mwaka hadi mwaka, kwa sababu mtu anajitazama anamaliza *BSc Nursing* lakini kuthaminiwa kwake au *level* ya malipo yake hailingani na wenye *Bachelor of Science* wengine yeye anakuwa yuko *down* kabisa.

Ningependelea Waziri ambaye ni msikivu sana Mheshimiwa Profesa Mwakyusa na Dada yangu Mheshimiwa Aisha Kigoda, mlitazame kwa karibu na hivi ni vitu vya kuangaliwa kwa ukaribu sana. Sote tumekiri hapa, wasemaji wamekiri, Kamati imekiri na Msemaji wa Kambi ya Upinzani amekiri kwamba, kada hii ya *Nursing and Midwifery* ndiyo pekee ambayo kuna maombi nchi za nje wanahitajika lakini sisi wenyewe hapa ndani hatunao wa kutosha. Sasa ikiwa imeshafikia *stage* hiyo halafu wale tulionao tusiwathamini vizuri tukawachunga vizuri; nini tunafanya? Kwa hiyo, nafikiri hili ni suala ambalo inabidi liangaliwe vya kutosha na Muswada huu uwe ni faraja kidogo uwape *privilege* hawa watu nao wajisikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wa vijijini nikimalizia kusema na kushauri ni kwamba, kutokana na maumbile ya kule vijijini na kazi zao kuwa ngumu, imefikia *stage* nakumbuka wengine waliwahi kupewa baiskeli na wengi wao ni akinamama wanapewa baiskeli saa nane za usiku waende kutoa huduma. Hiki ni kitu kigumu kidogo, labda iwe motisha ya namna nyingine. Ufanywe utaratibu maalum kwa kusaidiana na wakunga wa kienyeji ambao wana mchango mkubwa kule vijijini.

**NAIBU SPIKA:** Wanaitwa wakunga wa jadi.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Wanaitwa?

**NAIBU SPIKA:** Wanaitwa wakunga wa jadi.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Wanaitwa wakunga wa jadi?

**NAIBU SPIKA:** Siyo wa kienyeji. *(Kicheko)*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Wanaitwa wakunga wa jadi, nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika. Hawa wakunga wa jadi pamoja na hawa wenye taaluma ya ukunga wawe na ushirikiano fulani, kuwe na makubaliano wasaidiane na wafanyiwe taratibu na Muswada huu utazame ni namna gani utawapa *privilege* watu hawa si kuwekewa vizingiti tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi yangu yalikuwa hayo machache tu, nategemea yatazingatiwa pamoja na vile vifungu tulivyovitaja au vilivyotajwa na upande wa Upinzani. Nafikiri tunaweza kuuboresha Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nianze kushukuru kwa kupata nafasi hii adimu ya kuchangia Muswada huu unaohusiana na

masuala ya wauguzi na wakunga. Nianze kwa kuwapongeza wauguzi na wakunga wote nchini kwa kazi nzuri ambazo wamekuwa wakizifanya.

Kwa maeneo ambayo yamepatwa na mafuriko, nichukue nafasi hii pia kuwapa pole hata katika Mkoa wangu wa Iringa eneo la Idodi na hivyo kuwashukuru sana wauguzi ambao wamesaidia wananchi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni muhimu sana kama ambavyo wengi wameelezea. Nianze kwa kusema kwamba, katika nchi yetu tumeahidi kwa mfano kupunguza vifo vya akina mama wajawazito. Tumeelezea katika waraka mbalimbali, kutoka vifo vya akinamama 229 hadi 265 ifikapo mwaka 210, ikiwa ni pamoja na maeneo mengine kama Millennium Development Goals, MKUKUTA na kadhalika.

Nilipokuwa natafakari nikasema kwa nini tuseme tunapunguza vifo na siyo kuondosha vifo maana tunabariki vifo viwepo lakini kwa kiwango kidogo. Hivyo, ningeomba kwa mchango wangu huu, Wizara izingatie kwamba hatutapunguza bali tutaondosha. Kwa Lugha ya Kiingereza tukubaliane kwamba, tuwe na Sera *"No mother should die when giving birth"* na hivyo itatusaidia sana. *(Makofi)*

Kila wakati tukisema tunapunguza basi lengo litabaki kwenye kupunguza na watu wakifikia 265 ifikapo mwaka 2010 tutasema tumefanya vizuri zile *vision* na *mission* tulizokuwa nazo zimekuwa *achieved* lakini kumbe tukiwa kama Viongozi na Wawakilishi wa Wananchi wa Tanzania na tukizingatia kwamba asilimia 50 ya idadi ya watu milioni 40 nchini ni wanawake, hivyo hatupaswi kabisa kubariki kwamba wawepo watu wanaokosa maisha kutokana na kutoa maisha kwa kiumbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba kushauri ibara ya 5 kifungu cha 9 ambacho kinaendelea kumteua huyu *Registrar* ninavyojua kazi za *Registrar* zinahitaji malengo ya muda mrefu na kadhalika. Sasa *section 5,* ibara ya 9, kifungu kidogo cha 2, sehemu ya 3 inaelezea kwamba, *Registrar* atateuliwa kwa muda wa miaka mitatu. Naomba kushauri kwamba, aongezewe muda iwe ni miaka mitano kwa sababu ndani ya miaka mitatu atafanya mambo machache na kunakuwa na *tension* kwamba baada ya miaka mitatu naondoka. *Of course*, kuna nafasi ya kuteuliwa mara ya pili, lakini miaka mitatu kwa kazi kama hii ni muda mchache.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine tumekubaliana katika sera kwamba, tupate huduma za wauguzi na wakunga kupitia taasisi mbalimbali kama taasisi za dini. Tunashukuru sana taasisi hizi zinafanya vizuri, lakini baadhi ya maeneo taasisi hizi za dini huwa zinawatoza wananchi maana hazipewi ruzuku, ruzuku huwa inakwenda kwenye Hospitali za Serikali. Nikichukulia mfano wa hospitali iliyoko jirani kabisa na Wilaya ya Ludewa inayoitwa Rugalawa, pale wanatoa huduma kwa wananchi. Sasa hospitali nyingine ni kama Tosamanga na maeneo mengine ambako kuna hospitali kama hizi. Sasa huduma kama hizi za akinamama wajawazito wanapokwenda kwenye hospitali za taasisi za muundo huu huwa wanakuwa *charged.* Kwa mfano, Hospitali ya Rugarawa wanatozwa 35,000, kwa mama wa kijijini kutoa 35,000 anapokwenda ku-

*deliver* au anapohitajika kufanya operesheni hakika ni nyingi sana hivyo kupelekea wanapohitaji huduma za ukunga wanabaki nyumbani hadi inapofikia *critical stage* na wanapofika hospitali aidha mama au mtoto anafariki.

Hivyo, ningeiomba Wizara itambue huduma za taasisi hizi na wawape vitendea kazi si lazima sana wawape ruzuku ya pesa lakini vitendea kazi ili akinamama wanapoenda kupata huduma za ukunga wakati wa kujifungua wapatiwe huduma hizo bure kama tulivyokwishakubaliana kwamba hakuna mtu anayepaswa kufariki anapotoa uhai wa mtu mwingine. Kwa hiyo, tupate takwimu nchi nzima ya taasisi zinazotoa huduma kwa Wanawake wa Tanzania maeneo mbalimbali na tupate *statistics* kwamba, ndani ya wiki, ndani ya siku ni akinamama wangapi wanajifungua. Baada ya kulitambua hilo, kupitia mashirika yetu ya MSD kwa sababu tunataka tuboreshe huduma hizi za wakunga na wauguzi, wapelekewe vitendea kazi ili akinamama wanapokwenda kutibiwa maeneo hayo watibiwe bure kama Hospitali za Serikali na hata kama wanatozwa basi kiwe ni kiwango kidogo sana ambacho ni *affordable* kwa akinamama wote wa Tanzania kama ni 2000 au 5000 na wala isizidi hapo; vinginevyo bado azma yetu ya kuhitaji kuondosha vifo na siyo kupunguza, inakuwa haijafikiwa malengo. Kwa hiyo, ningeomba kutoa ushauri; ili Muswada ufanye kazi vizuri lengo la kutoa huduma bora ya uuguzi basi maeneo hayo ni muhimu sana yakazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyokwisha kujifunza kutoka kwa wachangiaji wengine, kwa kweli huduma hii ya wauguzi na wakunga inahitaji moyo na wito. Vile vile nichukue nafasi hii kukishukuru sana Chuo Kikuu cha Muhimbili kwa kuzalisha wanataaluma wengi wa uuguzi na ukunga. Wanatoa Digrii na safari hii kuna mama mmoja amepata hadi *Ph.D* juu ya masuala ya *nursing.* Kwa hiyo, nawapongeza sana. Faculty kama hii ni muhimu ikawepo Chuo Kikuu cha Dodoma ili tupate wauguzi na wahudumu wa kutosha.

Taasisi hii ya Muhimbili, pamoja na pongezi hizi ningeomba tuzingatie kuwapa mahitaji yao, yaani ruzuku na wanalo eneo ambalo wanahitaji kuongeza ili kupata *products* za kutosha za wauguzi na wakunga, basi eneo hilo nalo lizingatiwe, linaitwa Mlonga Mzila kule Dar es Salaam. Tunaishukuru sana Serikali kwa kuzingatia hilo ili nchi iweze kuzalisha wauguzi na wakunga wengi hatimaye wengine wafike kwenye zile Wilaya zetu za Ludewa, Makete, Njombe na Mufindi, waweze kutoa huduma kwa ufasaha na kwa wakati unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningeomba Wizara ijaribu pia kulizingatia ni kuhusiana na maadili. Ibara ya 7(2)(c) inasema kutakuwepo na Kamati inaitwa *Ethical and Disciplinary Committee*. Sasa wengi wamezungumzia maadili ya wakunga, yako maadili mengine ni ile *appearance* ya mavazi; wauguzi na wakunga tunatarajia katika nchi yetu wanapoonekana unaona kabisa kwamba huyu ni muuguzi na mkunga. Wanaita *body expression,* unakuta wauguzi na wakunga wana kucha ndefu sana, nywele zimekaa hazieleweki, unaanza kusema hivi huyu ni *engineer* au ni *nurse!* Sasa zipo *ethics* huyu akisema mwanasheria hata anapo-*appear* unajua huyu ni *laywer,* akisema ni muuguzi unahitaji nguo nyeupe, usafi, ukarabati wa vitu mbalimbali. Kwa hiyo, tungetarajia hizi Kamati zisaidie sana, ikiwa ni pamoja na lugha. Wengi

wamelizungumza, tukienda kifungu cha 21 kinazungumzia kuhusu *licence to practice* kwamba, kutakuwa kunatolewa leseni za kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara hii inasema kwamba, leseni na *certificate* zitatolewa *in a prescribed form,* katika utaratibu utakaoelezwa. Sasa huu utaratibu pia umeelezwa kwamba, kutakuwepo na ku-*renew* hizo leseni za *midwife* katika kutoa huduma. Ningeomba sana, hizi leseni zitakapokuwa zinatolewa kusiwe na taratibu ambazo wanataaluma hawa watashindwa kukidhi vigezo. Kwa mfano, labda unatakiwa ulipe ada, hiyo ada ikiwa kubwa sana watashindwa na hatimaye wanaoumia zaidi watakuwa ni Watanzania walio wengi na siyo yule mwanataaluma. Vile vile hata hili suala la ku-*renew* hizo leseni nalo ni vema likazingatiwa ili uwepo utaratibu ambao ni *very friendly* ambapo wale wanataaluma wanaweza wakakidhi mahitaji na taratibu zikazingatiwa pande zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo, niungane na Wizara kwa kutuletea Muswada huu mzuri sana kwa manufaa ya nchi yetu na niwapongeze sana na nasema naunga mkono Muswada huu ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mtu ambaye jina lake hakuliweka anasema hivi: "Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ndani ya Ukumbi inasikitisha. Naona *UWT is better represented and do nurse! When we resume in the evening, they should be told that nurses and midwives are for the entire population regardless sex."* Sasa yeye amesema sex, angesema *gender* ingekuwa *better.* Huyu ndugu hakuandika jina, basi wanaohusika wajue hizo habari. *(Kicheko)*

Tutarudi saa 11.00 jioni, tutakaporudi tutakuwa na Mheshimiwa Juma Njwayo na Mheshimiwa Martha Mlata, nadhani watakuwa wametosha halafu tutampa Mheshimiwa Naibu Waziri saa moja ya kuweza kujibu hoja mbalimbali mlizotoa kisha tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mimi sina lingine. Napenda kusitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni. Ahsanteni sana.

*(Saa 6.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipoahirisha Shughuli za Bunge mchana nilikuwa nimewataja wafuatao kwamba ndio watakuwa wachangiaji wetu wa mwisho, tukianza na Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo akifuatiwa na Mheshimiwa Martha Mlata. Mheshimiwa Juma Njwayo.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii ili niungane na Wabunge wenzangu kuchangia Muswada ulioko mbele yetu. Kwanza, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza mwaka huu 2010 kuongea hapa Bungeni, naomba kuwatakia Watanzania wote heri ya mwaka mpya wa 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kutujengea jengo jipya la OPD pale kwenye Hospitali yetu ya Wilaya ya Tandahimba na kufunguliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu mpendwa, Mheshimiwa Pinda, tarehe 22 Novemba. Nawashukuru sana Wananchi wa Tandahimba. *(Makofi)*

Vile vile napenda kupongeza jitihada zinazofanywa na Serikali kutupunguzia matatizo ya afya pale Jimboni. Pamoja na kushukuru, nichukue nafasi hii kuwaomba kuwa ile *X-Ray* mashine iliyobaki pale iwekwe sasa tupunguze kwenda Newala na maeneo mengine. Pia napenda kuipongeza Serikali kwa zahanati zangu za Jimboni kule karibu tano kupatiwa umeme wa solar hivi karibuni. Naomba waendeleze jitihada hizo ili zile nyingine zilizobaki muda si mrefu nazo zipatiwe angalau kupunguza giza na nini, unajua tena usiku wauguzi wetu wanapokuwa na wagonjwa bila taa inaleta adha na usumbufu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza tena serikali kwa kuleta Muswada huu hapa Bungeni kwa sababu una lengo la kuratibu shughuli za uuguzi na wakunga na kwa maana hiyo, kuboresha huduma kwa wananchi. Ninapenda kutoa ushauri kwa Serikali kuwa, kwanza ninaiomba iongeze wigo wa mafunzo kwa wauguzi na wakunga kwa kuongeza wanafunzi wengi na udahili mkubwa na vyuo vingi ili uendane na mpango maalum wa afya ya msingi. Hali iliyoko sasa kule vijijini ni adha. Nasema adha, labda nitoe mfano; pale Wilayani kwangu Tandahimba nina zahanati 9 ambazo hivi leo ninavyoongea, sina *competent* wauguzi au wakunga. Sasa zahanati zipo na upo wakati Serikali ilisema kwamba, tuna mpango wa kuanzisha zahanati kila kijiji na kituo cha afya kila Kata. Sasa kwa upungufu huu tulionao tukienda hivi, ninaona kuna haja ya kuongeza jitihada tena za nguvu kabisa, bajeti pamoja na vyuo na kutoa nafasi kwa wanafunzi wengi na vyuo ili tuendane na hali iliyoko kule vijijini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, wananchi wengi wanaishi vijijini; ni lazima kuwe na mpango wa makusudi wa kuratibu wakunga na wauguzi waende vijijini. Kwa hivi sasa hawa wachache wanaohitimu kwenye vyuo vyao huwa hawaendi kule. Mimi ninadhani kuna haja ya serikali kuweka mpango mahususi kabisa kuhakikisha kuwa kila anayesomeshwa na hela ya mlipa kodi wa Tanzania anakwenda vijijini. Hilo lilikuwa ni ombi langu kwa Serikali. Ninaiomba Serikali pia iwaangalie watumishi kwa maana ya wauguzi na wakunga ambao wana upungufu kidogo, wameajiriwa siku nyingi lakini wana upungufu wa sifa kidogo; wawapunguzie masharti ili waweze kupata nafasi ya kwenda kusoma. Kwa kufanya hivyo, wanaweza wakajiendeleza vizuri na hivyo kuinua ufanisi na utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wauguzi na wakunga wana kazi ngumu na nzito na majukumu yao ni mengi. Wanaamka usiku, mishahara yao ni midogo, mazingira ya kazi ni hatarishi, uwezekano wa kukutana na maambukizi ni mkubwa; mimi nadhani ipo haja ya Serikali kuangalia mara mbili mbili watu hawa maana kwa kweli ndio wanaosaidia sana kupunguza matatizo ya afya kule vijijini tuliko. Naomba wajitahidi sana wawaongezee wafanyakazi, maana unaenda kijijini unamkuta nesi hana hata glovu!

Wiki nne zilizopita nilitembelea kijiji kimoja kwenye mikutano yangu ya hadhara ya nchi, nilipomaliza pale nikapita kwenye zahanati; nilipofika pale nikamkuta mtu ana kifafa cha uzazi, nesi akaniambia sina *magnesium sulphate* ambayo pengine ingeweza kumsaidia huyu. Pia akaniambia hata *MSD* tumeomba mara nyingi kupitia Halmashauri yetu, hakuna *oxytocin* ambayo inasaidia tatizo la damu, *bleeding* kubwa kwa wajawazito.

Sasa kwa hali hii ninadhani kuna haja ya kuwasaidia hawa tupeleke dawa za kutosha, tuhakikishe mazingira yanakuwa mazuri ili waweze kufanya kazi katika mazingira yanayofanana. Habari ya nyakati za nyuma kwamba kuna baadhi ya kazi ni wito, mimi nafikiri muda huo haupo tena; tuiangalie *scheme* ya kada hii ili mazingira mazuri yatengenezwe ikiwa ni pamoja na *promotion.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango uliopo sasa wa Maendeleo ya Afya ya Msingi, unataka tutakapofika mwaka 2017 tupunguze vifo vya watoto chini ya miaka mitano kutoka 112 mpaka 65. *Marternal mortality rate* ipungue kutoka 578 mpaka 175, *infant death* zitoke kwenye 68 mpaka 35, lakini watu wa kuchanja ndio hawa wauguzi, watu wa kuweka *drips* sijui na nini ndio hawa wauguzi; sasa tusipowatengenezea mazingira mazuri ndugu zangu, Watanzania wenzangu, hali inazidi kuwa mbaya. Ni ombi langu kwa Serikali kuongeza juhudi ili wauguzi wetu, wakunga wetu, wafanye kazi katika mazingira yaliyoboreka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo jambo lingine ningependa niliseme hapa, kwa kupita kule kwenye vituo vya afya na zahanati nimebaini jambo moja. Kuna matatizo ya wauguzi, unakuta aliyeajiriwa wiki iliyopita na aliyeajiriwa miaka 10 mshahara ni mmoja, vyeo vyao ni vile vile; kwa nini? Tunapunguza motisha, matokeo yake wanakimbia mazingira ya vijijini hayafanani na ya vijijini; wakikumbana na hali hiyo wengine wanatoka kule vijijini wanakimbilia mijini, tumewakosa.

Niombe pia wale ambao ni wazalendo wanaotoka kwenye zahanati au vituo vya afya vya binafsi wakija huku basi kama anajulikana alikuwa *competent* kwenye maeneo hayo na taasisi aliyokuwa anaifanyia ni *competent,* inajulikana ina sifa, basi tusimuanzishie mshahara ule wa mwanzo, tumuweke kutegemeana na sifa aliyotoka nayo kule. Kama amefanya miaka mitano kule basi sisi huku tumfikirie miaka mitano ile iwe motisha kwake kwa kufanya kazi lakini pia kuwafanya waweze kuishi kule vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Muswada wenyewe nina mchango mdogo kwa kifungu cha 9(2) na kifungu cha 2(1) cha Jedwali kuhusiana na kuchaguliwa tena kwa Registrar na Wajumbe wa Baraza. Mimi nina mapendekezo kwamba, kifungu hiki kiainishwe kiwe wazi, muda wa Registrar na Wajumbe kukaa kwenye Bodi ile uwekwe wazi na ukomo ujulikane. Hii itapunguza umimi umimi, umilele umilele na pia utatengeneza mawazo mapya, maana unajua ukikaa muda mrefu kwenye chombo kimoja inaleta matatizo sana; unaona wewe ndio una uzoefu wakutosha na nini; kwa hiyo nilikuwa nina mawazo kwamba eneo hili liangaliwe na uwazi uwe mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye kifungu cha 13(1) kuhusu *appointment and duties of supervisory authority,* kwa kweli sina tatizo lakini hapa ninapenda kuchangia

kwamba, mfumo wa utawala kwenye maeneo haya ufuate *hierarchy* ya *professional* ya wale wauguzi. Kwamba, kutoka kule juu kwa *Chief Nursing Officer, Regional Nursing Officer, District Nursing Officer*, tukifanya hivyo tutatengeneza komandi nzuri.

Ninachochelea tu ni kwamba, wakati tunaingiza mambo ya Wizara ya Afya kama ndio *Professional Ministry,* tukachukua TAMISEMI tukaiingiza hapo, unakuta panatokea migongano kidogo, unapeleka TAMISEMI mara unaridisha hapa. Mimi hoja yangu hapa tuendelee kufuata mawazo na komandi ya mfumo wa Wizara badala ya kuunganisha unganisha mara Wizara hii au Wizara ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua wakisema sana wenzako unakuwa huna hoja mpya sana. Mimi kwa leo nilikuwa ninataka nichangie katika maeneo haya na kuiomba Serikali ifanye jitihada za dhati kuboresha huduma ya afya nchini kwetu na hasa vijijini. Naunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona msemaji mwingine niliyemtaja hapa alikuwa mara aseme naomba mara ondoa jina langu, basi tena hayupo, kwa hiyo huyu ni msemaji wetu wa mwisho.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. OMARI ALI MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga ni muhimu sana katika Sekta ya Afya, kwani asilimia 60 ya Watumishi wa Afya ni Wauguzi na Wakunga. Hivyo, kuletwa Sheria hii itasaidia sana utekelezaji wa majukumu na ufanisi kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutambua umuhimu wa Kada ya Uuguzi na mchango wake mkubwa katika Afya, Wizara iunde Kurugenzi ya uuguzi ili kuhakikisha, kuharakisha na kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya kada hii muhimu, ambayo inahudumia wagonjwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa Kurugenzi ambayo itajihusisha na uuguzi itasaidia kutatua matatizo mengi ya wauguzi ambao wanafanya kazi zaidi kuliko kada nyingine za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wauguzi ndio wanaofanya kazi usiku na mchana lakini maslahi yao ni madogo sana na hayakidhi ukilinganisha na kazi yenyewe, hivyo ipo haja ya kurekebisha maslahi ya wauguzi kulingana na kazi ambayo wanaifanya ili wafanye kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitishwa kwa Sheria hii ya Kuanzishwa kwa Bodi ya Uuguzi, Mwenyekiti awe ni mtu ambaye ana taaluma ya uuguzi kwani atarahisisha kutatua matatizo ya Wauguzi kwa kuwa atakuwa muelewa na mambo hayo. Ahsante.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Kaibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji. Kwa kweli wanafanya kazi ya wito, iliyotukuka, ya huruma na kuwasaidia Wagonjwa wote na mahali popote walipo Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakunga na Wauguzi ni watu muhijmu sana kote duniani na hapa kwetu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, taaluma hii nyeti na muhimu sana, haikupewa umuhimu mkubwa huko nyuma ikizingatiwa kwamba Wauguzi ndio wanaokaa na Wagonjwa wakati wote; naomba sana wakumbukwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi wanayopata ni madogo sana sawa sawa na wakusanya ushuru au walinzi kwenye Mashirika ya Umma. Naomba Sheria hii itambue tatizo hili na maslahi yao yaongezwe, pia wawe wanapelekwa mafunzoni na kupandishwa vyeo kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Wauguzi na Wakunga wana madai mengi sana ya nyuma ambayo mpaka sasa hayajalipwa; naomba sana malimbikizo ya madai yao yalipwe na kusiwe na malimbikizo tena.

Mheshimwa Naibu Spika, naiomba Serikali iongeze Bajeti nzima ya Wizara ya Afya ili kutatua matatizo ya Wauguzi na Wakunga, yakiwepo mishahara midogo, fedha za uhamisho, fedha za mazingira magumu, sare za kazi, vitendea kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie pia uwezekano wa kuwasaidia Wauguzi na Wakunga walioko kwenye Hospitali za Mashirika yetu ya Dini na kadhalika kwani nao wana matatizo mengi kuliko hata hao walioko Serikalini. Naomba Serikali iwasaidie kwani kazi wanazofanya ni zile zile za kuokoa maisha ya Wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, naunga mkono hoja na kuipongeza Wizara ya Afya kwa usimamizi wa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri na kuwasilisha Muswada huu ili ipitishwe sheria iweze kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali isimamie vizuri Muswada huu ukipita utumike kwa maslahi ya Watanzania na itolewe elimu kwa Wataalam, Wauguzi na Wakunga ili kuwezesha kwa hali na mali na tupate faida ya kiafya Tanzania kama nchi ya kileo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Magogoni, naunga mkono Sheria hii itumike.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza wote waliohusika kututayarishia Muswada huu na kutufikishia hapa Bungeni.

Kipekee, ninaomba kuwapongeza rasmi Waziri wa Afya, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Chief Medical Officer Tanzania.

Baada ya pongezi hizo, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Pamoja na kuunga mkono hoja ninaomba ufafanuzi kwenye yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Muswada huu unakusudia kufuta Sheria ya Usajili ya Wauguzi na Wakunga, Sura ya 325 na hivyo kutimiza matakwa yaliyokusudiwa katika taaluma ya uuguzi na ukunga ni vyema kabisa vitendea kazi vikaboreshwa pamoja na kinga ikiwemo Life Insurance kwa watendaji hawa popote walipo.

Mheshimwa Naibu Spika, ninaomba ieleweke na ikubalike kuwa kazi hii ya Wauguzi na Wakunga ni hatarishi sana na pia ni *very demanding*.

Serikali inasemaje kuhusu afya ya Watendaji hawa? Mara nyingi sana Muuguzi/Mkunga huwa anatoa huduma bila *gloves*. Wakati mwingine hata wakiwa na *gloves* wanatobolewa na sindano au kukatwa na wembe, endapo yule anayehudumiwa ana ugonjwa wa kuambukiza, basi naye anaingia kwenye kuambukizwa maradhi. Katika hali kama hii, Mkunga huyo au Muuguzi huyu anasaidiwaje na Serikali? Ni kifungu kipi kati ya vifungu hivyo tisa vya Muswada huu kinamlinda?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba maelezo ya kina wakati wa majumuisho. Ninamalizia kwa kuwapongeza Wauguzi na Wakunga wote. Ninawaomba wafuate nyayo za Mwanzilishi Florance Nigtugel.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Nafurahi kupata nafasi hii ili nichangie kuboresha Sheria ya Ukunga na Uuguzi. Kabla ya yote, nitoe pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Timu yote kwa kuleta Muswada huu.

Muswada huu ni muhimu sana na ni wakati wa kuiangalia kwa umakini mkubwa Sekta ya Afya kwa idadi ndogo waliyonayo ukilinganisha na idadi ya wagonjwa. Pamoja na Sheria hii kupitishwa Serikali itenge bajeti mfululizo kwa miaka kadhaa kuhimili wimbi la Wagonjwa na hasa vitendea kazi havitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote hayo naomba Waziri anipe ufafanuzi kwa maswali haya:-

(i) Kwa nini Serikali imeshindwa kumtambua Muuguzi aliyesomea taaluma ya dawa za usingizi na ganzi? Tatizo hili lipo, naomba ufafanuzi.

(ii) Serikali ina mkakati gani wa kuboresha Chuo cha Bugando ili kitoe Diploma ya Dawa za Usingizi na Ganzi *(Nurse Anaesthethetist)?*

(iii) Je, Serikali huchukua hatua gani kwa hospital zake zinazofanya upasuaji bila wataalam hao wa dawa za usingizi na pia kuna mkakati gani wa kumaliza tatizo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iendelee kuboresha Hospital zote za Wilaya ambazo bado ziko nyuma kimajengo mfano Hospitali ya Wilaya ya Misungwi. Hospitali ya Wilaya ya Misungwi inahitaji msaada wa bajeti kubwa juu ya majengo yake hayatoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema nikakubaliana na wenzangu kuwa kazi ilifanyika kuandaa Muswada huu. Vile vile mishahara yao ni midogo ingawa wanafanya kazi saa 24.

Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na naomba ufafanuzi wa yale niliyouliza.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja na natoa maelezo kama ifuatavyo:-

Motisha ni kichocheo cha mtumishi kufanya kazi kwa ari zaidi kwa kuwa si sehemu ya pato lake. Hivyo, Wauguzi na Wakunga hawa wafikiriwe kwa yafuatayo: Motisha ya mkopo wa magari ya bei nafuu (yenye gharama za chini); fedha nje ya mshahara wake kama motisha, napendekeza asilimia tano mshahara wake; na posho za mazingira magumu asilimia tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo moja muhimu sana ni hili la wakunga wa jadi. Amini usiamini, kama yupo mkunga wa jadi aliye na sifa nzuri za uzalishaji huaminika zaidi kwa wananchi kuliko zahanati au kituo cha afya kisicho na sifa au vifaa vya kutosha na muuguzi mwenye sifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Baraza lishushwe mpaka kwenye ngazi za Wilaya, lisiishie katika ngazi ya Mkoa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Muswada huu. Section (9)(2), Part III, nashauri Registrar ateuliwe kwa miaka mitano badala ya mitatu.

Lengo la Sheria hii ni kuboresha huduma ya uuguzi na ukunga ikiwa ni pamoja na kuratibu na kadhalika. Katika Ilani tumeahidi kupunguza vifo vya watoto wachanga kutoka watoto 95 kwa kila watoto 1000 wanaozaliwa hai kwa utafiti wa mwaka 2002 hadi 50 mwaka 2010. Kupunguza vifo vya uzazi kutoka 529 kati ya wazazi laki moja kwa utafiti wa mwaka 2002 hadi 265 mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu 265 - 100,000 bodo ni wengi. Nashauri tuwe na Sera inayosema *no mother should die when giving birth.* Hivyo Section (6) - Function of the Council pamoja na kazi zilizoorodheshwa iwepo function ya kupunguza vifo vya akinamama. Ielezwe wazi wazi katika Muswada huu function ya Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na function (e) inayosema collaborate with National Council Technical Education, Tanzania Commission of Universities et cetera, ni muhimu sana Bodi ya Mikopo ikatoa mikopo kwa wauguzi na wakunga kwa vyeti vyote vinavyohusu taaluma hii mfano Diploma, Degree, Ph.D na kadhalika.

Aidha, nitumie fursa hii kukishukuru Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi ya Jamii Muhimbili (MUHAS), kwa jitihada zake za kufundisha wanataaluma wa Nursing na Midwife na hatimaye kutoa graduates wa Degree na hata Ph.D.

Vile vile nitumie nafasi hii kuiomba Serikali iwasaidie Chuo Kikuu cha Muhimbili kupata fedha kwa wakati na kuongeza eneo la Chuo cha Mlonganzila ili kiweze kutoa wanataaluma wa Nursing and Midwifery.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako maeneo vijijini ambayo hutoa huduma za ukunga kupitia Taasisi za Mission na kadhalika kwa kutoza gharama, mfano, Hospitali ya Lugarawa Wilaya ya Ludewa hutoza Sh. 35,000 kwa operation ya mzazi na hivyo hupelekea watu kujifungua nyumbani na kupoteza maisha.

Naishauri Wizara ipate takwimu *(statistics sensus)* ya wanawake na *estimates* ya wale wanaoweza kujifungua na kupanga Budget ili wajitolee vifaa katika hospitali husika ili huduma za kujifungua kote nchini ziwe bure kama katika Hospitali za Serikali. Hospitali hizi zipo nyingi nchini ambazo zinatusaidia kama Ikonda, Lugarawa, Tosamaganga na nyingine nyingi.

Mheshimwa Naibu Spika, aidha, suala la upungufu wa wauguzi na wakunga liangaliwe ili kupunguza shifti ndefu za kazi na haki zao “Entitlements” ziweze kuboreshwa. Part VI, Section 25 - Receipt of Complaint by the Registrar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Section 7(1)(c) - *Ethical and Disciplinary Committee.*

Mavazi – *White*
– Kufuga kucha
– Nywele
– *Jewelleries*

*Section 21 - Licence to Practice Nursing or Midwife;* hizo regulations za registration zisiwe na utaratibu mgumu sana, mfano, fees wakashindwa ku-practice na hatimaye wakashindwa kuwahudumia wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Nawashukuru sana kwa michango yenu. Sasa tumpe nafasi mtoa hoja aweze kuhitimisha hoja yake. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, unayo saa yako moja.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuhitimisha hoja yangu, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii tena niweze kuhitimisha hapa Bungeni.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi. Wote ninawashukuru sana kwa michango yao ambayo nina imani kubwa itatusaidia wakati wa kutekeleza sheria hii baada ya kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni; kwanza, Mheshimiwa Omar Kwaangw' - Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Dokta Tarab Ali Tarab - Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Profesa Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Juma Njwayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Vuai Abdallah Hamisi, Mheshimiwa Shally Joseph Raymond, Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir, Mheshimiwa Margret Sitta na Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao, naomba kutoa ufafanuzi wa maswali yaliyojitokeza wakati Waheshimiwa Wabunge wakichangia Muswada huu kama inavyojionesha kama nitakavyokuwa nimezungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia kwa uchungu mkubwa tatizo la uhaba wa watumishi. Kimsingi, baada ya kukaa na Kamati kule Dar-es-Salaam chini ya Mheshimiwa Omari Kwaangw', yale yote ambayo tumekubaliana tumeyaingiza katika jedwali la *amendment* iliyotolewa leo. Aidha, mambo mengi ya moja kwa moja yaliyojitokeza katika mchango wa Mwenyekiti wa Kamati na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani yote tumeyazingatia katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia kwa uchungu mkubwa tatizo la uhaba wa wauguzi na watumishi wa Sekta ya Afya kwa ujumla. Aidha, wameisihi Serikali iboreshe mazingira ya kazi kwa wauguzi ikiwa ni

pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa vitendea kazi na kuwapatia maslahi yanayoendana na umuhimu wa kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imechukua hatua kadhaa za kukabiliana na changamoto ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezizungumzia. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kutekeleza mkakati wa kuongeza idadi ya wadahili katika vyuo vya uuguzi na ukunga. Chuo cha Sayansi ya Afya Muhimbili kama ilivyokuwa imezungumzwa baada ya kupata kiwanja katika eneo la Mlonganzila kwa ujenzi wa Chuo Kikuu, imetenga bilioni nane kwa ajili ya kulipia fidia kwa waliokuwa wanamiliki eneo hilo. Pia chuo kikuu hicho kimepata mkopo nafuu wa shilingi bilioni 50 kutoka Benki ya Exim ya Korea kwa ajili ujenzi wa Hospitali ya Chuo itakayotumika kwa mafunzo. Upembuzi yakinifu umeshafanyika na inategemea kuwa ujenzi wa hospitali hiyo utaanza mwaka huu. Chuo Kikuu vile vile kinafanya mawasiliano na vyombo vingine vya fedha hapa nchini kuona uwezekano wa kupata fedha za kujenga mabweni na madarasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea na jitihada za kuvikarabati vyuo vyote vya uuguzi vilivyofungwa kama vile Chuo cha Nachingwea, Tunduru na Mpanda ili viweze kuchukua wanafunzi, ambapo hatua za manunuzi zinafuatwa ili tupate wakandarasi waweze kufanya ukarabati. Aidha, ukarabati wa Chuo cha Nzega na Kibondo umekamilika na vipo tayari kufunguliwa mwezi wa tatu. Serikali imeongeza nafasi za ajira mwaka hadi mwaka na pia kuitumia Wizara ya Afya moja kwa moja kupata wahitimu na kuwapangia kazi kulingana na vibali vya ajira kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Tatizo la muundo wa utumishi pia limeshughulikiwa na muundo mpya unategemea kuanza kutumika mwezi Julai mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine yaliyozungumzwa na yaliyochangiwa kwa maandishi ni ya jumla, ambayo ninakubali kabisa yanaweza kuathiri utendaji wa mtaalamu huyo, hivyo kusababisha akakiuka mambo yaliyomo katika sheria. Kama Wizara, tutajitahidi kuhakikisha tunaboresha yale yote yanayoathiri moja kwa moja utendaji wa mtumishi. Kwa mfano, kuongeza watumishi, vitendea kazi, mazingira mazuri ya kazi na maslahi kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamechangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia tatizo la mmomonyoko wa maadili ikiwa ni pamoja na lugha mbaya. Wizara yangu imeendelea na jitihada za kushughulikia tatizo hili ikiwa ni pamoja na kulishughulikia kwa uharaka tuhuma mbalimbali zinazotolewa na uvunjaji wa maadili. Aidha, Wizara imeandaa na kusambaza nchi nzima Vitabu vya Kanuni za Maadili ya Wauguzi na Wakunga, viwakumbushe wajibu wao. Vilevile Wizara yangu ikishirikiana na Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, imeendesha mafunzo kwa muuguzi mmoja na mwalimu muuguzi mmoja kutoka kila hospitali na chuo cha uuguzi nchi nzima, watakaoendelea kutoa elimu ya maadili sehemu za kazi. Wizara inachukua nafasi hii kutoa wito kwa jamii kutoa ushirikiano kwa wauguzi na viongozi wa sehemu ya kutolea huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la motisha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara nyingine inaendelea kufuatilia maslahi ya wafanyakazi na imeendelea kuboresha upatikanaji wa vitendea kazi kwa wauguzi na wakunga kulingana na bajeti inavyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitajaribu kujibu baadhi ya hoja ambazo zimejitokeza kutokana na wakati utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja za Kamati ya Huduma za Jamii; baadhi ya wahitimu kuajiriwa kwenye taasisi nyingine na hata wengine kufanya kazi tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inahitaji kuboresha mishahara na maslahi kwa watumishi wake ikiwa ni pamoja na wauguzi na wakunga ili kuwavutia kufanya kazi kwa moyo zaidi. Vyuo vichache vilivyopo havipati maombi ya kutosha, bila shaka kutokana na sifa. Vyuo vya Afya huhitaji wanafunzi waliofaulu masomo ya sayansi ambao bado ni wachache. Aidha, baadhi ya wanafunzi kutoka sekondari huomba nafasi katika vyuo mbalimbali vikiwemo vya afya na hatimaye baadhi ya wanafunzi hawa huchaguliwa sehemu zaidi ya moja na hivyo huchagua sehemu nyingine badala ya vyuo vyetu. Hali hii itatatuliwa baada ya Serikali na wananchi kuongeza shule za sekondari na hasa zenye mchepuo wa sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni wahitimu wengine baada ya kupangiwa vituo vya pembezoni huwa hawaendi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Wabunge kuhusu kutoa posho maalum na wale wanaopangiwa katika mazingira mazuri ni mazuri. Wizara itaendelea kuongea na utumishi kuona jinsi ya kutekeleza suala hili, hata hivyo baadhi ya Halmashauri zimeanza kutekeleza jambo hili kuvutia watumishi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wauguzi na wakunga wanaofanya kazi katika kwenye taasisi binafsi nyingine walipwe na kupandishwa vyeo kama wenzao.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yaliyotolewa na Kamati ni ya msingi lakini kimsingi Serikali inatoa miongozo kwa waajiri binafsi kutolipa chini ya kima cha ngazi cha mishahara. Vile vile wauguzi na wakunga wanaodai posho zao mbalimbali za likizo na uhamisho; Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, inawasiliana na TAMISEMI kuhakikisha kwamba wauguzi wenye malimbikizo yao wanalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa ujumla ambayo ameyazungumza hapa ni yale yale ambayo Mwenyekiti wa Kamati tulikubaliana kule Dar-es-Salaam, lakini kwa sababu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani alitaka na yeye tumsikie, basi nitajibu kama ifuatavyo:-

Alisema kwamba Tanzania inafaidika vipi na wauguzi wanaofanya kazi nje ya nchi wakati wamesomeshwa na kodi ya Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli na mimi nakubaliana naye kwamba, wamesomeshwa na kodi ya Watanzania. Serikali kupitia Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, iko katika mchakato wa kuandaa takwimu za wataalamu wa Tanzania walioko nje ya nchi na baadaye kuandaa Sera Maalum na kuona ni namna gani Serikali inaweza kufaidika na wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema Muswada hauoneshi kifungu chochote ambacho kinatoa motisha kwa wauguzi na wakunga, badala yake umesheheni vifungu vya kuwadhibiti katika utendaji kazi. Nafikiri hii pia Waheshimiwa Wabunge wengine walisema kwamba tumesema zaidi masuala ya kuwadhibiti lakini hatujaonesha vipengele vya motisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii lengo lake ni kusimamia suala la maadili na utendaji kazi kwa wauguzi na wakunga wa kitaalamu. Masuala ya maslahi pamoja na mazingira ya kazi yamewekwa bayana katika taratibu za uendeshaji wa utumishi wa afya, yaani *The Health Service Scheme General Notice 126* ya 2009 iliyotolewa chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura Namba 298.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti kuchaguliwa na Wajumbe wa Baraza badala ya kuteuliwa na Waziri; ni muhimu sana suala la uteuzi wa Mwenyekiti libaki katika mamlaka ya uteuzi kwa sababu Serikali inayo utaratibu wa kuhakiki, yaani *vetting*, kwa atakayeteuliwa kuwa Mwenyekiti. Hivyo, kusema kwamba wachaguliwe na Wajumbe inaweza ikawa shida kwa sababu hawatajua, pengine kuna taarifa nyingine ambazo Mheshimiwa Waziri amezipata kuhusu Mwenyekiti huyo na ndio zikasababisha amchague. Kwa hiyo, kipengele hiki ambacho kiko katika sheria nadhani kitaendelea kubaki kama kitakavyokuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kusajili wauguzi liwe la Msajili badala ya kuwa la Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema mamlaka ya kuamua kama muuguzi anazo sifa za kusajiliwa yabaki kwa Baraza na Msajili awe mtekelezaji wa maamuzi ya Baraza; hii itaondoa uwezekano wa mtu mmoja kuhodhi madaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sifa za kitaaluma za msajili hazikuwekwa wazi na hivyo napendekeza sifa hizo ziwekwe wazi na nafasi hiyo ishindaniwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana suala la uteuzi wa msajili libaki kwa mamlaka ya uteuzi kwa sababu Serikali kama nilivyosema hapo mwanzo, ina utaratibu wake wa kufanya *vetting.* Aidha, sheria nyingine za utumishi wa umma zitazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sifa za kitaaluma za msajili hazikuwekwa wazi na hivyo ninapendekeza sifa hizo ziwekwe wazi na nafasi hiyo ishindaniwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uteuzi wa msajili libaki na mamlaka ya uteuzi kama nilivyokuwa nimesema. Vigezo vya nani atakuwa *supervisory authority* na mamlaka ya *supervisory authority* kumsimamisha muuguzi yanaweza kutumika vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vya nani atakuwa *supervisory authority* na mwongozo atakaoutumia kumsimamisha muuguzi utatolewa kwenye kanuni chini ya ibara ya 49. Aidha, muuguzi anayesimamishwa chini ya kifungu hiki, hasimamishwi kama adhabu bali ni kumzuwia asiendelee kuhatarisha jamii wakati uchunguzi kamili ukiendelea kufanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya muuguzi kufutiwa usajili kabisa, kifungu cha 18(2); kifungu hiki ni muhimu kubaki kwa vile kinatoa nyakati ambazo muuguzi au mkunga atakuwa anakiuka maadili ambayo hawezi kufaa tena kuwa katika fani hiyo. Iko mifano ya taaluma mbalimbali kama vile madaktari, wanasheria, ambao wanafutiwa leseni moja kwa moja na kutoweza kufanya kazi hizo katika fani zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la muuguzi kuwakilishwa na wakili katika kifungu cha 27(2); kifungu hiki kimetoa hiyari kwa mhusika kuweza kujiwakilisha mwenyewe au na wakili anapokuwa na shauri mbele ya Baraza. Aidha, kuwakilishwa na wakili kutasaidia kuhakikisha kuwa haki inaendelea. Kama tunavyofahamu, kila mtu anayo haki na wajibu wa kutendewa haki, kwa hiyo kama mtu atakuwa anatakiwa aende kujieleza akiona kwamba yeye mwenyewe hatoshi, anayo haki kabisa na uhuru wa kuweka mtu ambaye atamsimamia na kujibu hizo hoja badala yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya uteuzi wa Wajumbe wa Baraza kufanyika na mamlaka ya uteuzi itakavyoona. Pendekezo hili limezingatiwa katika jedwali la marekebisho ya ziada, *further schedule of amendments,* ambalo litawasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mbunge wa Kiwani, alitoa hoja anasema Wizara iunde Kurugenzi ya Uuguzi ili kuhakikisha, kuharakisha na kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya kada hii muhimu ambayo inahudumia wagonjwa zaidi. Wizara itafanya tathmini na hatimaye kushauriana na mamlaka nyingine kama Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kuona uwezekano wa kuanzisha Kurugenzi ya Uuguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya wauguzi ni madogo sana, haya yamechangiwa pia na Waheshimiwa Wabunge wengine na hayakidhi kulingana na kazi yenyewe. Kwa hiyo, ipo haja ya kurekebisha maslahi ya uuguzi kulingana na kazi ambayo unaifanya. Vile vile Mwenyekiti wa Bodi ya Wauguzi awe ni mtu mwenye taaluma ya uuguzi na atarahisisha kutatua matatizo ya wauguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ushauri umezingatiwa na serikali imepitisha muundo mpya wa utumishi katika Sekta ya Afya ambao utaanza kutekelezwa terehe 1 Julai, 2010. Muundo huu unaboresha maslahi ya watumishi katika Sekta ya Afya katika ngazi zote.

Mheshimiwa Mgana Msindai amesema, taaluma ya uuguzi haikupewa umuhimu mkubwa huko nyuma; maslahi wanayoyapata ni madogo sana. Sheria hii itambue tatizo hili na maslahi yao yaongezwe, pia wawe wanapewa mafunzo na kupandishwa vyeo. Hili pia lilezungumzwa na Wabunge wengi ambao wamechangia hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo mpya wa utumishi kama nilivyosema unaanza mwezi wa Julai. Waajiri wote wamehimizwa na Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kuandaa mipango ya mafunzo ya watumishi, hii ni pamoja na wauguzi. Jitihada kubwa zimefanyika za kukabiliana na malimbikizo ya watumishi waliokaa muda mrefu bila kupandishwa cheo. Kwa hiyo, hili linashughulikiwa. Malimbikizo ya mishahara nayo yanalipwa, lakini kwa kuwa tatizo hili lilikuwa la muda mrefu, itachukua muda kulipa malimbikizo kutegemeana na bajeti itakayokuwepo.

Mheshimiwa Vuai Abdallah amesema anaunga mkono Muswada, anaiomba Serikali iweze kusimamia vizuri Muswada huu. Tunaahidi kuwaelimisha wote wanaohusika na utekelezaji wa Muswada huu na tutausimamia kuhakikisha kwamba unakwenda vizuri.

Bima ya Wauguzi na Wakunga; Mheshimiwa Shally Raymond alitaka wauguzi na wakunga pamoja na kuboreshewa vitendea kazi wawe na Bima ya Maisha kutokana na kufanya kazi katika mazingira hatarishi na Serikali inatakiwa kujali afya ya watendaji hawa.

Maoni ya Mheshimiwa Mbunge yamezingatiwa na kuwa swali hili ni la kisera, Wizara italifanyia kazi katika kuboresha kazi na Wafanyakazi wa Sekta ya Afya, ikiwa ni pamoja na kuwa na Bima ya Maisha kutokana na kufanya kazi katika mazingira hatarishi kutokana na itakavyokuwa imeonekana inafaa.

Mheshimiwa Pindi Chana, amesema pamoja na kazi za Baraza zilizoorodheshwa, kuwepo kazi ya wauguzi na wakunga ya kupunguza vifo vya akina mama ni muhimu chombo cha mikopo ya uuguzi na wakunga ikatoa mikopo ili kuwamotisha. Katika majukumu yao ya msingi, wauguzi na wakunga hutoa huduma kwa akinamama wajawazito na hivyo kuchangia sana katika kupunguza vifo vya akinamama na watoto. Aidha, watumishi hawa wamepewa fursa sawa kuweza kukopa katika vyombo vya mikopo, Serikali huwa inadhamini katika kupata mikopo ya aina mbalimbali kwa kadiri ambavyo wenyewe wanaruhusiwa kuweza kukopa.

Mheshimiwa Maria Hewa amesema motisha ni kichocheo cha mtumishi kufanya kazi kwa ari zaidi, wakunga wapewe mikopo kama alivyokuwa amezungumzia mwingine lakini vilevile anasema wapewe asilimia tano ya mshahara wao kama motisha na asilimia tano ya mazingira magumu. Muundo mpya wa utumishi utakaoanza Julai, 2010 umeboresha maslahi ya watumishi katika Sekta ya Afya. Wizara ya Afya itaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kuziingiza baadhi ya posho kama ile ya mazingira iwe motisha zaidi kwa watumishi wa Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkunga wa jadi aliye na sifa nzuri ya kuzalisha huaminika zaidi kwa wananchi kuliko zahanati au kituo cha afya kisicho na sifa au vifaa vya kutosha au muuguzi mwenyewe. Wizara inatambua sana kazi na mchango mkubwa ya wakunga wa jadi. Hivyo basi, wakunga wa jadi wanasimamiwa chini ya sheria ya tiba asili na tiba msafara. Baraza lishuke chini hadi ngazi ya wilaya, pendekezo hili tumelizingatia katika Muswada huu nafikiri itakuwa inajionesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mtulia alitushukuru kwa sababu tumempatia na majengo. Yeye pamoja na Mheshimiwa George Malima Lubeleje na Mheshimiwa Ndugai wote walizungumzia kwamba hakuna clear pass wala watumishi, kuna mkanganyiko katika ngazi zao kwa hiyo vitu vyote hivi vinatakiwa viwe vimerekebishwa. Pia walikuwa wanazungumzia kuhusu madaraka mengi ambayo wamepewa ile authority. Nataka kusema tu hapa kwamba, wale supervisor authority wenyewe kila watakachokuwa wanakifanya ni lazima baadaye wakiripoti katika Baraza. Kwa hiyo, maamuzi yote yanayotolewa na supervisor iwe authority lakini maamuzi anayopata yule Registrar yote haya atakuwa hawezi akamua yeye kama yeye lakini vilevile itabidi aendelee kutoa ripoti katika ile Council. Kwa hiyo, yote yale ambayo yameonekana kwamba wameongezewa majukumu makubwa, nadhani haitakuwa tatizo kwa sababu Council yenyewe ndio itakuwa inatoa jibu la mwisho.

Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa mdomo walizungumzia kuhusu bajeti ndogo ambayo nayo inachangia sana katika utoaji wa huduma. Mimi nakubaliana kabisa kwamba ili tuweze kuhakikisha kwamba watumishi wanatoa huduma inavyotakikana kutokana na ujuzi ambao wameupata ni lazima na sisi kama Serikali tuweze kuhakikisha kwamba tunawawezesha ili waweze kufanya kazi hii kwa uangalifu na umakini zaidi. Hivyo, sisi kama Serikali kama nilivyojibu kwa ujumla kwamba tutajitahidi sana na bahati nzuri bajeti yetu huwa inaongezeka mwaka hadi mwaka ingawa hatujaweza kufikia Abuja Declaration, kwa hivi sasa tuko katika asilimia 11, naamini kabisa jinsi tutakavyokuwa na bajeti ya kutosheleza, basi tutaweza vilevile na sisi kufikia ile asilimia 15 ambayo Abuja Declaration imeizungumzia.

Mheshimiwa Mohamed Mnyaa amezungumzia pia suala la motisha ambalo nimeshalijibu. Grades za nurses nafikiri nimeshajibu. Pia amezungumzia kuhusu suala la nurses ambao wana degree, *Bachelor of Science.* Nafikiri hii itajiweka wazi mpaka Julai tutakapotoa mwongozo wa utumishi.

Mheshimiwa Job Ndugai na yeye pia yote ambayo amezungumzia kuhusu ibara ya 7, 14(3) ya madaraka kwamba ni mengi lakini vilevile wakili kwamba siyo sehemu yake. Mimi nafikiri haya yote nilikuwa nimeshayajibu. Vilevile alizungumzia kuhusu malalamiko kwamba, manesi wana lugha chafu. Wakunga wa jadi anasema kwamba hatuwezi kuwatambua, sisi tumewatambua na nafasi yao kwa kweli ni kubwa na ndio maana tumesema tunawatambua chini ya Kurugenzi ya Tiba Asilia.

Pia alizungumzia kuhusu suala la mama ambaye anajifungua na kwamba anapewa chandarua kidogo; tumelichukua hili tuone ile size lakini mama anapojifungua leo, kwa ushauri wangu nadhani ni vizuri tukamuacha mama huyu kwa muda wa mwezi mmoja, aweze kulala na mtoto wake badala tena baba aanze kulala na mama, atakuwa anawasumbua. Mimi nafikiri kwa ushauri mzuri baba atumie kitanda kingine halafu amuache mama baada ya kazi ngumu ya kujifungua aweze kumnyonyesha mtoto na yeye apate muda wa kupumzika ili maziwa yawe mengi aweze kumnyonyesha mtoto wake. *(Makofi)*

Hata hivyo, hii size ya vyandarua tunavyotoa mimi nachukua kwamba kweli ni kitu kizuri. Kwa hiyo, tutaangalia size ya vyandarua vinavyotolewa ili mtoto akishachangamka mama na baba waweze kuwa na mtoto wao na kuweza kumwongezea joto. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Jenista Mhagama naye amezungumzia kuhusu bajeti ya Sekta ya Afya na jinsi ya kupunguza vifo vya akinamama, lakini pia alikuwa anazungumzia Wajumbe wa lile Baraza. Alipokuwa anasema kwamba pale kwenye *Regional Nursing Officer or District Nursing Officer* badala yake tuweke *DNO*; sisi tumeliangalia tukaona kwamba, pale anapokuwa ni Mwakilishi wa *Regional Nursing Officer* haina maana achukue mwakilishi huyu *nurse* anayetoka pale mkoani. Kwa hiyo, nafikiri hii sheria imesema wasiwe zaidi ya kumi na tatu, lakini tunaiangalia tuweze kuona kwamba hata kama akichukuliwa huyu ni *Representative* wa *Regional Nursing Officer* kama ni *Representative* wa *Regional Nursing Officer* anaweza akatoka pia katika wilaya yoyote ile lakini iwe ni ndani ya ule mkoa.

Kwa hiyo, nafikiri ikibaki hivyo hivyo *Representative and Regional Officer or DNO* haitaleta madhara yoyote. Halafu pia katika kifungu cha 5(3) ilikuwa imeuliza kwamba, yule mtu ambaye anakuwa *declared bankrupt* kwa nini asiwe na sifa. Kama mnavyojua mtu yeyote yule atakayekuwa *declared bankrupt* atakuwa ameshakuwa amekosa sifa kwa sababu huyu tena ameshakuwa ni mufilisi kwa maana kama ameshakuwa mufilisi hatuoni kama ana sifa tena kuweza kuwa katika Mabaraza makubwa kama haya. Kwa hiyo, ndio maana tukasema mtu yeyote katika hawa atakayechaguliwa moja ya sifa zake asije akaonekana kwamba ameshakuwa *declared* kuwa *bankrupt*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwamba katika baadhi ya dispensary zimekutwa hazina umeme; hili ni suala tunalitambua ndio maana tumeona Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya TAMISEMI sasa tuangalie utaratibu kama inawezekana pesa zikipatikana tuweze kuhakikisha kwamba walau basi tutumie umeme ambao unapatikana kwa nguvu za *solar*. Hii inaweza ikampunguzia makali ya kazi ambayo mtumishi anajikuta yuko kule peke yake, lakini masuala mazima ya vitendea kazi, mazingira ya posho na *overtime*, yote haya nafikiri nimeshayajibu katika eneo ambalo nilikuwa nimelizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo lilikuwa limeulizwa na Mheshimiwa Job Ndugai la muda wa mafunzo kuwa miaka mitatu na miwili; mitatu kwa

*registered nurses* na miwili kwa *nursing.* Nafikiri hapa nakubaliana naye, tutafanya marekebisho yote itakuwa ni miaka mitatu, hapa ilikuwa imekosewa kidogo itatakiwa kufanyiwa marekebisho.

Wakunga wa jadi kama nilivyojibu wanapata katika Sheria ya Tiba Mbadala, Sura ya 244.

Nataka kusema kwa vile masuala mengi ambayo yamezungumzwa na mengine unakuta yamejirudiarudia, labda niweze kusema tu kwamba, yote kwa pamoja tutayaandika na kuyatolea majibu na kuweza kuyatoa kwa Waheshimiwa Wabunge wote hapa Bungeni ili tuwe tunajibu kwa ufasaha. Kwa sababu unapokuwa unaongea hapa saa nyingine unaweza ukawa umekosea kidogo, lakini naahidi tutaandika kwa maandishi ili yaweze kujibiwa vizuri na tutayatoa kabla ya Bunge hili kuisha.

**NAIBU SPIKA:** Nategemea hayo utakayoyafanya ni yale ambayo hayahusiani na Muswada. Kwa mfano, vile vifungu alivyovisema Ndugai kwamba vimepinga, nategemea tutakapoingia kifungu kwa kifungu mtarekebisha, yale mengine uliyozungumzia ya kisiasa uwaandikie tu lakini ya sheria itabidi yawe hapa sasa.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniongezea mwongozo huo. Niseme tu kwamba, kwa kweli mchango ambao mmeutoa umetusaidia sana na bado tutaufanyia kazi ili tuweze kuhakikisha kwamba, yale ambayo yanaboresha Muswada yatatusaidia sana ili kuweza kutekeleza huu Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukushukuru, naomba sasa niseme kwamba naomba kutoa hoja. Ahsante sana. *(Makofi*)

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono, mtakubaliana na mimi kwamba, Mheshimiwa Naibu Waziri amebobea sana katika kujibu maswali yanayohusu Idara hii, kwa hiyo nampongeza sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaingia hatua nyingine.

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga wa Mwaka 2009
***(The Nursing and Midwifery Bill, 2009)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namba 5(1)*(a): A chairman of the Council who shall be appointed from amongst senior registered nurses;* kwa nini huyu *Chairman* asichaguliwe na Wajumbe wenyewe wa *Council* badala ya kuwa *appointed*? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri alijibu wakati anaeleza, naomba ujibu tena.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nilipokuwa nikijibu hoja hapa nilisema kwamba, Mwenyekiti wa Baraza ni lazima atachaguliwa au atakuwa *appointed* na *Ministry* kwa sababu haiwezekani hawa Wajumbe wao ndio wamchague Mwenyekiti. Mwenyekiti tumesema huwa anakuwa *vetted*, kwa hiyo, kuna taarifa ambazo Mheshimiwa Waziri yeye huwa anazipata kuhusiana na yule ambaye anamwona kwamba anafaa.

Kwa hiyo, haitawezekana kwamba aje tu pale halafu achaguliwe *from nowhere*. Ndio maana tumesema kwamba, huyu atachaguliwa na Mheshimiwa Waziri na wale wengine sasa kama Makamu Mwenyekiti na wengine, watachaguliwa na Wajumbe wenyewe.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kichwa cha habari

*(Kichwa cha habari kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 26

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 27 ukisoma kwenye *side note* imeandikwa *procedure for inquiry,* lakini ukienda kwenye *subsection* yenyewe 27(1) ule mstari wa mwisho kuna neno limeandikwa *enquiry*; mimi nadhani *inquiry* ni neno sahihi. Sijui kama umeliona?

**MWENYEKITI:** Ndio nimeona.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutasahihisha ni kweli *inquiry*.

**MWENYEKITI:** Unasahihisha sasa hivi; kwa hiyo, tunaandika kama ilivyo kwenye *marginal note.*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 28

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 28 pamoja na marekebisho ukisoma ile *clause* mpya *subsection number four,* ambayo imeongezwa ukurasa wa tatu, neno *inquiry* tena nadhani limekosewa linatakiwa liandikwe *inquiry* kwa kuanza na "i" badala ya "e".

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 32

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35

Ibara ya 36
Ibara ya 37

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 49
Ibara ya 50
Ibara ya 51
Ibara ya 52

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*
*(Bunge lilirudia)*

**(Muswada wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga wa Mwaka 2009 *(The Nursing and Midwifery Bill, 2009)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge imepitia Muswada wa Sheria uitwao *The Nursing and Midwifery Act, 2009* pamoja na mabadiliko kifungu hadi kifungu na kuukubali. Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Muswada wa Sheria uitwao *The Nursing and Midwifery Act, 2009* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umepitia njia zake zote katika Bunge, kilichobaki sasa ni kumpelekea Mheshimiwa Rais aweze kuweka saini yake ili uweze kufanya kazi yake kama Sheria.

Baada ya kusema hayo, naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kazi nzuri aliyoifanya na kwamba amewasilisha kwa makini sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hatuna shughuli nyingine kwa sasa, kwa hiyo, napenda kuahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho, nikiwatakia jioni njema na ninawashukuru kwa kazi ya siku ya leo. (*Makofi*)

*(Saa 11.55 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 28 Januari, 2010 Saa Tatu Asubuhi)*